# Nipashe

Alhamisi Oktoba 27, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581111

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS.1,044,303,118

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Adaiwa** kumchinja hadi kumuua rafiki yake kisa supu

UKURASA 2




UKURASA 13

# Watumishi wa vyeti feki kulipwa mafao

• **Ni** walioondolewa katika utumishi baada ya uhakiki wa mwaka 2016, serikali yawatengea mabilioni... *Endelea ukurasa 2*



Sehemu ya majengo ya mradi wa Dege Eco Village wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), uliokuwa umesimama kwa takribani miaka saba, ilivyonaswa na kamera yetu eneo la Mbutu wilayani Kigamboni, Dar es Salaam jana. **Habari zaidi Ukurasa 03. PICHA: JUMANNE JUMA**

## Sekta ya benki yaimarika baada ya janga la UVIKO-19

UKURASA 3




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya KCB, John Ulanga, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kutangaza mafanikio ya benki kufikia uzania wa mali wa Sh. trilioni moja. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa KCB, Cosmas Kimario na Mkuu wa Fedha, Willis Mbatia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

RIPOTI MAALUM

## Simulizi wanawake wa Loliondo waliogeukia mkaa kuikabili njaa

UKURASA 4

**MICHEZO** **SIMBA, AZAM MECHI VIWANGO, UFUNDI** UK.32 **KATUNI** UK.6




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akipata maelezo kuhusu huduma za kidijitali zinazotolewa na Benki ya CRDB kwa Meneja wa Tawi la Michenzani, Ahmad Aboubakar (kushoto), alipotembelea banda lao katika uzinduzi wa Mkutano wa Mwaka wa Wadau wa Sekta ya TEHAMA, Zanzibar jana. Wengine ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (wa pili kulia), Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum (wa tatu kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi wa vyeti feki kulipwa mafao

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imetangaza kurejesha michango ya watumishi 14,516 waliobainika kuwa na vyeti vya kughushi na walioondolewa kwenye utumishi wa umma, ikitenga Sh. bilioni 46.8.

Urejeshaji huo utaanza Novemba Mosi mwaka huu na utafanyika kwa michango yao tu waliyowasilisha kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya PSSSF na NSSF bila kuhusisha michango ya mwajiri.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema hatua hiyo ya serikali imetokana na ombi la Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuangalia namna ya kuwafuta jasho watumishi hao.

"Kutokana na ombi hilo, Rais Samia alielekeza kufanyika kwa uchambuzi ili kuona namna gani ambavyo serikali inaweza kuhitimisha suala hilo, baada ya uchambuzi kufanyika Rais ameridhia kuwa watumishi wote walioondolewa kazini kwa kughushi vyeti, warejeshewe michango yao tu waliyokatwa kwenye mishahara na kuwasilishwa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Mifuko ya PSSSF na NSSF itarejesha michango ya wafanyakazi iliyowasilishwa kwenye mifuko hiyo bila kuhusisha michango ya mwajiri. Marejesho ya michango ya watumishi yataanza kufanyika Novemba Mosi mwaka huu, mtumishi husika atatakiwa kwenda kwa aliyekuwa mwajiri wake," alisema.

Alifafanua kuwa mtumishi alikuwa akikatwa asilimia tano ya mshahara kuchangia mfuko wa PSSSF na kwa NSSF ni asilimia 10 bila kuhusisha malipo yoyote ya ziada.

Alieleza kuwa watumishi hao wanatakiwa kwenda na picha mbili, nakala ya taarifa za kibenki kwenye akaunti iliyo hai na nakala ya kitambulisho cha taifa au mpigakura au leseni ya udereva.

"Mtumishi atatakiwa kujaza hati ya ridhaa kwa aliyekuwa mwajiri wake, aidha waajiri watawajibika kuwasilisha kwenye mifuko hati za ridhaa pamoja na nyaraka nyingine zinazohusu ulipaji wa mafao kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya mifuko husika," alisema.

Prof. Ndalichako alisema baada ya mifuko kupokea nyaraka kutoka kwa aliyekuwa mwajiri, malipo yatafanyika kupitia akaunti za benki.

"Niwahakikishie tayari mifuko imejipanga vizuri hakutakuwa na ucheleweshwaji wa malipo nyaraka zitakapopatikana malipo yatafanyika mara moja," alisema.

Kuhusu watumishi waliofariki dunia, Waziri Ndalichako alisema: "Utaratibu upo wa kawaida wa kuwalipa warithi kulingana na mirathi ambapo kunakuwa na wategemezi wake wanaosimamia mirathi inakuwa inaonyesha malipo hayo yaende kwa nani, kwa hiyo stahiki zao zitakwenda kwa warithi wa wahusika."

Alitoa rai kwa watumishi hao kuhakikisha wanakamilisha taratibu hizo, ili kuwezesha mifuko kuwarejeshea michango yao.

"Waajiri watoe ushirikiano kwa watumishi husika kwa kukamilisha na kuwasilisha mara moja nyaraka zinazotakiwa na mifuko, niwasihi waajiri wasitengeneze urasimu, wasitengeneze mazingira ya kutafuta kukatiwa, ni wajibu wao na si kuhitaji malipo ya ziada kuwajazia watumishi, wapewe ushirikiano unaotakiwa," aliagiza na kusisitiza ulipaji huo unatarajiwa kutumia miezi miwili.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, aliwaagiza waajiri wote kuwajibika kutoa ushirikiano kwa watumishi hao huku akitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufuatilia suala hilo.

**KAULI YA TUCTA**

Muda mfupi baada ya uamuzi huo, Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, alisema jijini Mbeya jana kuwa watumishi hao baada ya kuachishwa kazi, walikuwa na maisha magumu.

Alisema tatizo hilo lilianza mwaka 2017 mpaka 2019 wakati wa uhakiki wa vyeti ambapo watumishi hao waliondolewa kwenye utumishi na kusitishiwa mishahara, jambo ambalo alisema liliwafanya waanze kuishi maisha ambayo walikuwa hawajayazoea.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukubali maombi yetu na kuridhia watumishi hao kurejeshewa asilimia tano ya michango yao kwenye mifuko ya hifadhi za jamii, sisi kama chama tunamshukuru na tutamuunga mkono," alisema Nyamhokya.

Mmoja wa watumishi hao waliokumbwa na uamuzi huo wa serikali, Robert Simbeye, akizungumza na Nipashe jijini Dodoma jana, alimpongeza Rais Samia kwa serikali yake kuona kuwa wanastahili kupata fedha hizo ambazo ni michango yao waliyoitoa katika mifuko ya hifadhi ya jamii kwa kipindi chote cha utumishi wao wa umma.

Aprili 28, 2016 Rais wa wakati huo, Hayati Dk. John Magufuli alikabidhiwa taarifa ya uhakiki wa vyeti vya watumishi wa umma mjini Dodoma na kuitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuwaondoa kwenye orodha ya utumishi wa umma na kusimamisha mishahara yao.

Idadi yao ni 15,538 (walioondolewa kazini kwa kughushi vyeti au kutoa taarifa za uongo katika kumbukumbu zao rasmi za kiutumishi kuwa wana elimu ya kidato cha nne) pamoja na watumishi hewa 19,708, uamuzi uliowezesha serikali kuokoa Sh. bilioni 19 kila mwezi.

**■Imeandaliwa na Paul Mabeja (DODOMA), Grace Mwakalinga na Nebart Msokwa (MBEYA).**

# Adaiwa kumchinja rafiki hadi kumuua kisa supu

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Mchakama, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, Jamal Shomari Mtepa (30), ameuawa kwa kuchinjwa kama kuku kwa madai ya kunywa supu ya rafiki yake.

Taarifa kutoka kwa viongozi wa vijiji vya Mchakama, Mavuji na Jeshi la Polisi, zinaeleza mauaji hayo yalifanyika usiku wa Oktoba 24, mwaka huu.

Wakielezea tukio hilo kwa nyakati tofauti, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mchakama, Mohamedi Mpinga, alisema Mtepa na Akadwii walikuwa marafiki waliokuwa na tabia ya kutembeleana na wakati mwingine kila mmoja kulala kwa mwenzake.

Alisema siku ya tukio, marafiki hao walikwenda kunywa pombe na nyumbani kwao waliacha supu.

Alisema Mtepa aliamua kurudi nyumbani na kumuacha mwenzake akiendelea kunywa pombe na kuamua kunywa supu ile waliyoiacha na kulala.

Alisimulia kuwa Akadwii aliporejea na kutoikuta supu ile alichukua gongo na kumpiga Mtepa kichwani hali iliyomshtua usingizini na kuanza kugalagala.

Mwenyekiti huyo alisema, Akadwii alipomwona mwenzake kwenye hali hiyo, alichukua kisu na kumchinja kwenye shingo mithili ya kuku, huku akiwa amebakiza sehemu ndogo kutenganisha kichwa na kiwiliwili.

"Alimkata kichwa na kuacha sehemu kidogo ya ngozi kutenganisha kati ya kichwa na kiwiliwili," alisema Mpinga.

Alisema mtuhumiwa baada ya kutekeleza unyama huo, alivua nguo za marehemu na kuzivaa kisha kuuchukua mwili na kwenda kuutelekeza kwenye Mto Mavuji, huku miguu ikiwa ndani ya maji na kichwa nchi kavu.

Mwenyekiti aliendelea kusimulia wakati Akadwii akirejea nyumbani kwake, njiani alikutana na mtu mmoja ambaye hakumtaja jina na alipomwona nguo alizovaa zimechafuka damu alimuuliza, lakini hakupewa jibu, hali iliyomfanya mtu huyo kufuatilia alikotoka Akadwii na kuukuta mwili huo mtoni.

"Huyu ndugu baada ya kuukuta mwili wa Mtepa upo kwenye mto Mavuji alitoa taarifa kwa uongozi wa Kijiji cha Mavuji," alisema Mpinga.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mavuji, Shaibu Mnula na Mwenyekiti Issa Maji, wamekiri kupata taarifa hiyo na walipofuatilia waliukuta mwili huo ukiwa umetelekezwa mtoni.

Walipiga simu kituo cha polisi wilaya na askari wakiongozana na mtaalamu wa afya walifika kushuhudia mwili huo na kuruhusu ndugu kuuzika.

Taarifa kutoka kwa viongozi wa Kijiji cha Mavuji, inaeleza mtuhumiwa huyo amekamatwa na anashikiliwa na serikali ya kijiji hicho ili akabidhiwe polisi kwa hatua zingine.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Pili Mande, alithibitisha kupata taarifa hiyo na kuwatuma askari kufanya uchunguzi wa tukio hilo.

# NSSF yasaka mwekezaji kununua nyumba za Dege

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) limetangaza kuuza kwa mwekezaji mwingine atakayevutiwa kununua mradi wake wa ujenzi wa mji mpya wa Kigamboni jijini Dar es Salaam uitwao Dege Eco Village, uliosimama kwa takriban miaka saba sasa.

Mradi huo wenye thamani ya dola za Marekani 653,436,675 (Sh. trilioni 1.3) ulianzishwa mwaka 2014 na ilipofika mwezi Januari mwaka 2016 ulisimama.

Ujenzi wake unahusisha nyumba za kifahari, hoteli, maduka makubwa, eneo la wazi la mapumziko, baa, shule, hospitali, kumbi za mikutano, nyumba za ibada na migahawa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na shirika hilo na kutiwa saini na Mkurugenzi Mkuu wa Fedha, NSSF imetangaza kutafuta mzabuni mwingine atakayeuendesha mradi huo.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa NSSF inakusudia kuuza mradi mzima wa Dege Eco Village na shirika halitowajibika tena baada ya mauzo hayo.

"NSSF inakaribisha zabuni zilizofungwa kuununua mradi huu kwa viwango vya kimataifa vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Ununuzi wa Umma zilizochapishwa kwenye Gazeti la Serikali namba 446," ilibainisha taarifa hiyo.

Vilevile, shirika hilo limetoa fursa kwa watakaovutiwa nao, wanaweza kuutembelea Novemba 3, mwaka huu, kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa saba kwa lengo la kuukagua, kujiridhisha na mandhari yake.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa zabuni zote zinapaswa kuwasilishwa hadi Novemba 14, mwaka huu, saa 9:00 alasiri kabla hazijafunguliwa mbele ya waombaji wote watakaojitokeza kwenye ukumbi uliopo ghorofa ya saba katika Jengo la Benjamin William Mkapa.

Msimamizi wa mradi huo ni kampuni ya Hifadhi Builders Limited iliyoanzishwa na Bodi ya NSSF kwa ushirikiano na kampuni ya Azimio Housing Estate Limited (Ahel) na wajenzi wake ni kampuni ya M/s Mutluhan Construction Industry Company Limited kutoka Uturuki.

# Sekta benki yaanza kuimarika baada UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu**

SEKTA ya benki imeanza kuimarika baada ya kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 mwaka 2021.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB, Cosmas Kimario, alisema hayo wakati alipokuwa akiongea na waandishi wa habari kuhusu mikakati ya benki kukuza huduma na kuimarika kwa mazingira ya biashara nchini.

Alisema benki hiyo imeweka rekodi kwa kufikia mali zenye thamani ya zaidi ya Shilingi trilioni moja hadi kufikia kipindi cha robo tatu ya mwaka 2022.

"Rekodi hii imechangiwa zaidi na ongezeko la amana za wateja kwa asilimia 105 ndani ya kipindi cha miaka mitano huku faida ikiongezeka kwa asilimia 182 hadi bilioni 22.4 kwa kipindi hicho," alisema. "Biashara nyingi ziliweka mikakati ya kujipanua hasa baada ya athari za UVIKO-19 na matunda yake yameanza kuonekana. Sisi pia imetusaidia kupata uzania imara zaidi (strong asset base) na kuwahudumia wateja wetu kwa karibu zaidi." Alisema sababu nyingine ni uwekezaji mkubwa uliofanyika katika kuimarisha uendeshaji wa benki hasa kutumia teknolojia ya kidigitali kufikisha huduma kwa wateja.

"Huduma kama Intaneti Benki, Mobile Banking, na njia za malipo (POS) zimeendelea kuongeza ufanisi wa huduma kwa wateja wetu. Mpaka sasa asilimia kubwa ya miamala ya benki inafanyika nje ya matawi yetu jambo ambalo limeongeza ufanisi."

Alitaja sababu nyingine kuwa ni kuimarika kwa hali ya uchumi nchini kutokana na sera nzuri za serikali na usimamizi na sera nzuri za Benki Kuu ya Tanzania.

Vile vile, alisema uwekezaji katika rasilimali watu ni chachu nyingine iliyosaidia kuleta mafanikio haya.

"Tumeendelea kuwekeza katika kuboresha na kukuza rasilimali watu ili kuongeza ufanisi, lakini zaidi tumefanikiwa kupunguza gharama za uendeshaji hadi asilimia 49 kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita," alisema Kimario.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, John Ulanga, alisema benki imeendelea kukua toka mwaka 1997 ilipoanzishwa. "Benki ina mipango ya kujipanua zaidi ili kuweza kuwafikia Watanzania wengi zaidi. Tuna mkakati wa kuongeza matawi matano ndani ya miaka miwili ijayo kwenye mikoa mbalimbali ambayo bado hatujaifikia," alisema.

Kadhalika alisema, benki inaendelea kuangalia fursa ya kununua benki nyingine (acquisition) endapo zitajitokeza.

**UKUAJI WA BENKI MIAKA 5**

Akizungumzia ufanisi huo Mkurugenzi wa Fedha, Willis Mbatia, alisema utoaji mikopo umeongezeka kutoka bilioni 330 mwaka 2017 hadi 623 mwaka 2022.

Pia, amana za wateja zimeongezeka kutoka bilioni 318 mwaka 2017 hadi bilioni 646 mwaka huu sawa na ongezeko la asilimia 103.

Alisema mali zimekua kutoka bilioni 508 mwaka 2017 hadi kufikia trilioni 1.04, Septemba 2022 sawa na ongezeko la asilimia 105 na uwiano wa mikopo chechefu umeshuka kutoka asilimia 17.51 mwaka 2017 hadi asilimia 3.16 mwaka huu.

Mbatia aliongeza kuwa benki inatarajia kupunguza mikopo chechefu hadi chini ya asilimia tatu kufikia mwisho wa mwaka huu.

**MAFANIKIO ROBO MWAKA**

Alisema, faida kabla ya kodi kufikia Septemba 2022 ilikuwa bilioni 22.4 na kuwa ni ongezeko la asilimia 39 ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka 2021. "Faida hii kwa kila robo mwaka imekuwa bilioni 6.9, bilioni 7.7 na bilioni 7.8 kwa robo ya kwanza, ya pili na ya tatu mtawalia," alisema.


MULTICHOICE TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

## HAKI ZA KURUSHA MATANGAZO MBASHARA FIFA WORLD CUP 2022

SuperSport International (Pty) Limited, ni moja ya kampuni tanzu ndani ya Kundi la Makampuni ya MultiChoice inayowakilishwa hapa nchini na kampuni ya MultiChoice Tanzania Limited, ambayo inasimamia huduma kwa wateja wa MultiChoice katika eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MultiChoice Tanzania inapenda kutoa TAARIFA kwa wamiliki wa mitandao ya kurusha matangazo kwa njia ya waya (Cable), makampuni ya utangazaji na umma kwa ujumla, kuwa SuperSport International (Pty) Limited, ina haki za kipekee za matangazo kwa Televisheni za kulipia (exclusive Pay Tv broadcast rights) ya mashindano ya FIFA WORLD CUP 2022. Kwa maana hiyo, SuperSport itaonyesha mbashara mechi zote 64 za mashindano hayo.

Matangazo ya aina hiyo ya mashindano hayo yanaruhusiwa kurushwa kupitia Chaneli za SuperSport pekee ambazo hupatikana katika kisimbuzi cha DStv kinachoendeshwa na MultiChoice Group (MCG). Haki hizi ni kwa ukanda wote wa Afrika – Kusini mwa Jangwa la Sahara na visiwa jirani (Sub-Saharan Africa and adjacent islands) ikiwemo Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mantiki hiyo, kurusha, au kusambaza kwa njia yoyote ile matangazo ya aina hiyo ya mashindano hayo katika eneo tajwa bila idhini ya MultiChoice ni kinyume cha sheria, kanuni na makubaliano ya haki miliki.

Tunaujulisha umma kuwa MultiChoice na washirika wake, hawatasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa yeyote atakayerusha matangazo ya mashindano hayo (kwa njia ya televisheni za kulipia) bila idhini.

***Imetolewa na:***

***MultiChoice Tanzania Limited kwa niaba ya MultiChoice Group***

***Octoba 21, 2022***

217113602

RIPOTI MAALUM

# Simulizi wanawake wa Longido waliogeukia mkaa kuikabili njaa

**Na Elizabeth Zaya,** LONGIDO

"WAKATI mume wangu anaondoka, aliniachia mbuzi ili niwauze na kununua chakula, lakini walikufa wote kwa kukosa malisho. Tangu aondoke hapa mwezi wa tatu (Machi) hadi sasa (Oktoba) hali ni mbaya, hatuna chakula," Ngoje Maso, mkazi wa Kijiji cha Otepesi wilayani Loliondo mkoani Arusha anasimulia madhila yanayowapata kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ngoje, mama wa watoto watatu anaendelea kuwasilisha kinachowasibu, akitamka: "Kwa sasa chakula tunachoona ni muhimu kwetu ni uji, tunalazimika kukoroga uji mchana na jioni kwa sababu hautumii unga mwingi. Hata ukifanikiwa kupata kilo mbili kwa jirani unaona bora ukoroge uji, uweke na chumvi kwa sababu wenyewe unakuwa mwingi, mara chache tunasonga ugali.

"Wale mbuzi nilioachiwa na mume wangu ili niwauze na kununua chakula, walikosa malisho, wakakosa nguvu na wengine wakaugua. Hata nilipotaka kuwauza, wateja waliwakataa, wakawa wanakufa mmoja mmoja mpaka wakaisha wote.

"Nimeelemewa sasa kutunza hawa watoto, maana kula kwao na mahitaji mengine yakiwamo ya shule ni juu yangu, sijui itakuwaje hali ikiendelea hivi, maana hatuna chakula.

"Mume wangu alilazimika kuondoka hapa kwenda kutafuta malisho baada ya kuona ng`ombe wanazidi kufa, tulikuwa nao wengi lakini wengi wameteketea, kila kukicha tulikuwa tunakuta wamedondoka, wamekufa, wengine wanafia machungani. Ukiamua kuwauza, hakuna wanunuzi, wateja hawawataki, wanasema wamekonda mno."

Familia hiyo ni sehemu ya jamii kubwa ya wananchi wa Loliondo waliokumbwa na ukame kutokana na mabadiliko ya tabianchi, wanaume wakilazimika kuziacha familia zao kwenda kutafuta malisho ya mifugo, huku baadhi ya wanawake wakigeukia kuchoma mkaa, shughuli ambayo ni ngeni kushuhudiwa katika jamii ya Kimasai inayosifika kwa ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Nipashe iliyopiga kambi wilayani hapa, imeshuhudia ugumu katika upatikanaji wa maji, chakula na malisho ya wanyama, wananchi wakiiomba serikali na wadau wake kuwanusuru kwa kuwapelekea huduma muhimu.

Katika udadisi wake wilayani Loliondo, Nipashe imebaini kuwa katika familia nyingi za wafugaji, waliobaki nyumbani kipindi hiki cha ukame ni kinamama na watoto wao pamoja na wanaume wachache waliokutwa katika baadhi ya kaya ni waliokula chumvi nyingi, yaani wazee.


MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

SHEHENA YA MAGARI KUHAMISHIWA KATIKA BANDARI KAVU (ICDV) KUANZIA TAREHE 24 OKTOBA, 2022.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inapenda kuwataarifu wateja, wadau na umma kwa ujumla kuwa kuanzia tarehe 24 Oktoba 2022, magari yatakayokuwa yanapakuliwa kutoka melini katika Bandari ya Dar es Salaam yatakuwa yanahamishiwa katika Bandari Kavu (ICDV). Hivyo wateja wetu watakuwa wakichukua magari yao huko pasipo gharama yoyote ya ziada.

Utaratibu huu mpya unalenga kupunguza msongamano wa mizigo katika Bandari yetu unaosababishwa na ongezeko la shehena ya magari.

Taratibu nyingine zote za uondoshaji magari zitazingatiwa.

Imetolewa na:
Mkurugenzi wa Bandari
Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
S. L. P 1130
Dar es salaam
Barua pepe: pddsm@ports.go.tz
Tovuti: www.ports.go.tz
Simu: 0800110032 na 08001147

217116902


**WANAWAKE NA MKAA**

Sandeki Yaro, mkazi wa Kijiji cha Orubomba wilayani hapa, anasema mume wake aliondoka kwenda kutafuta malisho ya ng`ombe na kumwachia majukumu ya mlezi wa kaya yenye watoto watano.

Anasema baada ya ng`ombe na mbuzi wachache alioachiwa na mume wake kufa kwa kukosa malisho, alianza kuchoma mkaa, malighafi zake zikiwa ni kinyesi cha mbuzi na magogo madogo ya miti.

"Hali ni mbaya sana hapa kama unavyoona, ukame unatisha, inatubidi tutumie akili ya ziada kutafuta namna ya kunusuru familia.

Kwa sasa tumebuni mbinu nyingine ya kutumia magogo madogo ambayo tunaokota msituni kutengeneza mkaa. Tunapoyapata, tunakata vipande vidogo, tunafunika na kinyesi cha mbuzi na tunawasha moto, unakuwa unawaka kidogo kidogo, ndani ya siku tatu tunatoa.

"Kwa kutumia mbinu hii hatuweki magogo mengi, inakuwa ni kidogo tu ambayo tunatoa debe moja au mawili ya mkaa ambalo tunauza kwa Sh. 2,000. Na ukipata hiyo unakwenda kununua unga kilo moja.

"Na hii karibu wanawake wengi wa hapa Longido wamelazimika kufanya hii kazi, kwa sababu wanaume hawapo, wamekwenda kuhangaikia mifugo huko mbali, kuna waswahili eneo la mjini ndio tunategemea wanunue, sisi wenyewe hatutumii mkaa," anasema.

Mama huyo wa watoto watano anasema kazi hiyo ya kutengeneza mkaa ni ngumu kutokana na kuwa na moshi mwingi, akitamka: "Hivi tunavyozungumza (juzi) nina wiki moja sijaifanya kwa sababu niliugua mgongo, nikilala ndio kila kitu kimelala."

**PUNJE ZA MAHINDI**

Sandeki anasema njia nyingine wanayotumia kujiokoa dhidi ya baa la njaa ni kwenda kutafuta mahali kulipo na mashine za kusaga, mahindi yanayokuwa yamedondoka chini huyaokota na kinachopatikana ndicho wanasaga kwa ajili ya chakula chao.

"Kama hivi ambavyo nimeugua mgongo, ninashindwa kutengeneza mkaa, ninaamka asubuhi kuwahi kwenda kutafuta mashine ya kusaga niokote punje ninayoiona imedondoka. Kuna siku unapata hata nusu kilo au kilo moja, lakini kuna siku nyingine hasa za Jumapili inakuwa ni vigumu kupata.

"Nikishapata hicho kidogo, ninamwomba anayesaga anipatie hata kazi ya kufagia ili anisagie nipate unga kwa kiasi hichohicho cha mahindi nilichookota. Na ukikosa kwenye mashine moja kama hawajadondosha ni mara chache ukienda kwenye mashine nyingine upate kwa sababu kote huko unakuta na wenzio nao wameokota, wengi wamegundua, wanafanya hivyo," anasimulia.

**BIASHARA YA MKAA**

Katandee Tobiko, mkazi wa Kijiji cha Kimotoro, anasema jitihada zao kukabiliana na baa hilo, wakati mwingine zimekuwa zikikwaza maofisa wa serikali wanaowapoka mkaa.

"Mara nyingi tunapotengeneza huu mkaa huwa tunapeleka katikati ya Mji wa Longido kwa sababu pale kuna waswahili wengi ili wanunue. Tukiwa tumeupanga, unashtukia watu wamekuja na gari lao wanauchukua, wanamiminia kwenye gari wanaondoka wa wanaturushia viroba vitupu, hatujui wanatoka wapi ila gari lina namba za serikali na huwa wanatuambia hatutakiwi kuuza mkaa.

"Yaani pamoja na hali mbaya tuliyonayo, hawatuonei huruma, wanatubebea mkaa bila huruma, tunarudi nyumbani mikono mitupu na watoto wetu wanalala njaa," anawasilisha.

**MAHINDI YA SERIKALI**

Kiongozi wa Mila Wilaya ya Longido, Mutel Laizer anasema hali ya njaa ni mbaya katika vijiji vingi vilivyopo kwenye wilaya hiyo iliyosababishwa na ukame.

"Familia nyingi zinalia njaa, hazina chakula. Tumeshuhudia serikali ikileta chakula kwa bei nafuu katika wilaya hii lakini kinauzwa kwa bei kubwa ambayo wengi wanashindwa kumudu. Hata kinapoletwa, wanawaambia wanunue kuanzia gunia moja, wengi hawana uwezo huo.

"Mimi kama kiongozi wa mila, nimeliongelea sana hili lakini haijasaidia, wananchi wana njaa, wanashindwa kumudu bei ya chakula, lakini hata kile kinacholetwa na serikali nacho kinauzwa kwa bei kubwa, tena kuanzia gunia. Je, hapa kuna nia ya kuwasaidia kweli?.

"Tunachoona ni kwamba serikali inaleta chakula kwa ajili ya kupunguza makali ya wananchi, lakini wanaonufaika watu wenye uwezo, hasa wafanyabiashara, kwa sababu wao wana uwezo wa kununua gunia au zaidi na mwisho wa siku wao watakiuza kwa bei kubwa kwenye maduka yao. Tunaomba serikali iangalie hili," Laizer anasema.

Anabainisha kuwa debe la mahindi kwa sasa linauzwa na wafanyabiashara wa kawaida kwenye maduka yao kwa Sh. 22,000.

"Kwa hiyo kila mahali unakogeukia unakuta kugumu. Kwa wafanyabiashara bei iko juu zaidi, ukija kwa serikali ambako bei yao ni angalau kidogo, nao wameweka masharti magumu upatikanaji wa chakula chenyewe. Wanamwambia mwananchi ambaye hata uwezo wake wa kununua kilo moja ni mgumu, eti anunue gunia, hii ni hatari.

"Tunachoomba kama ikiwezekana, wapunguze zaidi bei hii ya chakula na kwa wale wasio na uwezo kabisa wawaangalie namna ya kuwasaidia hata wakiwapatia chakula kidogo itasaidia," anawasilisha.

Ni hoja inayoungwa mkono na Marya Oreteiti, mkazi wa Kijiji cha Longaiki, anayesema familia nyingi zinashindwa kumudu kununua chakula kinachouzwa na serikali.

"Sisi chakula cha serikali hatujakinusa hata kidogo. Ukienda kule wanakuambia eti ununue gunia moja. Unaona bora uende ukanunue kule kwa wafanyabiashara wa kawaida ambao wanapima hata kidogo ili familia ipate kula," anasema.

*ITAENDELEA KESHO



Mwenyekiti wa Kamati ya Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu nchini (CVCPT), Prof. Yohana Mashalla, akizungumza wakati wa mkutano wa 30 wa kamati hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni wajumbe wa kamati hiyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tanzania kunufaika zaidi tril. 16/- mradi LNG

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inatarajia kunufaika kiuchumi kutokana na mradi wa gesi asilia iliyochakatwa (LNG) na kuongeza Pato la Taifa (GDP) kwa Dola za Kimarekani bilioni saba kwa mwaka (sawa Sh. trilioni 16.388).

Takwimu hizo ni matokeo ya utafiti huru wa

Benki ya Stanbic Tanzania wa makadirio ya matokeo ya mradi huo kwenye uchumi.

Taarifa iliyotolewa na benki hiyo ilisema, utafiti huo ni wa hivi karibuni katika mfululizo wa ripoti zinazoelezea matokeo ya kijamii na kiuchumi yanayoletwa na miradi mikubwa ya nishati kwa nchi za bara la Afrika, pamoja na watu wake.

Utafiti wa awali uliotolewa na Benki ya Stanbic uliangalia uchumi wa Msumbiji na athari zinazoweza kuletwa na miradi ya LNG.

Ripoti hiyo ilizinduliwa jijini Dar es Salaam katika hafla iliyohudhuriwa na Waziri wa Nishati January Makamba, viongozi wakuu wa serikali na wawakilishi kutoka Wizara ya Nishati.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Benki hiyo, Tanzania inatarajia kunufaika kiuchumi kutokana na mradi huo na inaaminika baada ya kukamilika, mradi huo wa nishati utakuwa mkubwa zaidi kwenye historia ya Afrika katika suala la uwekezaji wa mitaji.

"Mradi huu unatarajia kuongeza Pato la Taifa (GDP) kwa dola bilioni 7 kwa mwaka. Kwa kulinganisha, Pato la Taifa la Tanzania mwaka 2020 lilikuwa dola bilioni 62 kwa mujibu wa Benki ya Dunia (WB)," ilisema taarifa hiyo.

Vile vile, taarifa ilisema ukubwa wa matokeo ya kiuchumi unahusiana na bei inayotarajiwa baada ya utekelezwaji wa mradi wa LNG. "Benki imeunda mfumo tofauti ya bei za siku zijazo, kuanzia na dola 5.50 MMBTU, kama bei ya kuanzia na kupanda hadi dola 12."

Baadhi ya matokeo muhimu ya ripoti hiyo ni matokeo ya mabadiliko ya kiuchumi, kati ya 270,000 hadi 600,000 fursa za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja za kitaifa katika maisha yote ya mradi, ushuru kati ya dola bilioni mbili hadi sita katika michango ya fedha kwa Serikali ya Tanzania kwa mwaka.

Waziri Makamba, aliipongeza Stanbic kwa kuzindua ripoti hiyo na kusema mchanganuo huo ni muhimu katika kutoa uelewa wa matokeo ya mradi wa LNG katika uchumi.

Akizungumzia ripoti hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield, alisema: "Tunafuraha kutoa uchambuzi muhimu wakati huu ambao Tanzania inakusudia kuwa taifa la viwanda. Bila shaka kupitia utekelezaji mzuri wa mradi wa LNG tunaweza kukuza viwanda na uchumi wa nchi. Uchambuzi wetu unaonesha kuwa mradi huu unaweza kuleta matokeo chanya katika mabadiliko ya kiuchumi; kuchochea ongezeko la mzunguko wa fedha na mapato ya mabilioni ya dola za kimarekani."

Mkuu wa Kitengo cha Biashara na Uwekezaji wa Benki hiyo, Manzi Rwegasira alisema: "Mradi huu wa LNG hauwezi tu kuinua matarajio ya kiuchumi ya nchi, bali utasaidia Tanzania katika mabadiliko ya mfumo wa vyanzo vya nishati, kwenda kwenye vyanzo vya nishati safi na wakati huo huo kufikia lengo lake la maendeleo ya viwanda."

Ripoti hiyo iliyoandaliwa na Benki ya Stanbic kwa msaada na michango kutoka kwa Conningarth Economists na Taasisi ya Utafiti ya Kuondoa Umaskini (REPOA), ni utafiti wa kwanza huru unaoangalia faida za kiuchumi za mradi wa LNG kwa Tanzania.

Ripoti hii inasisitiza umuhimu wa serikali kuchukua jukumu kubwa katika kuandaa mazingira rafiki ya kibiashara, kifedha na kisheria ili kuwezesha maendeleo ya mradi huo kwa wakati na kuhakikisha kuwa unakua na unabaki kuwa wa ushindani wa kimataifa.

# NMB: Benki kinara wa usawa wa kijinsia Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

UBAGUZI wa kijinsia ni mwiko kwa Benki ya NMB na juhudi zake za kutokomeza unyanyapaaji huo nchini zimeipa heshima duniani, ikithibitishwa rasmi kimataifa.

Jana jijini Dar es Salaam, benki hiyo ilitunukiwa hati maalum ya kutambulika duniani kama kinara katika mgawanyo wa kiuchumi kwenye suala la kijinsia (EDGE Certification) miongoni mwa taasisi za kifedha barani Afrika.

Akitangaza mafanikio hayo, Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa NMB, Emmanuel Akonaay, alisema wao ndiyo taasisi ya kwanza ya kifedha barani Afrika kupata uthibitisho huo unaotolewa na taasisi inayoitwa The EDGE (Economic Dividends for Gender Equality) Certified Foundation.

NMB ni ya kwanza kupata mafanikio hayo kitaasisi kwenye nchi zote zilizoko kusini mwa Jangwa la Sahara. Akonaay alisema zipo taasisi zingine mbili ambazo si za kifedha zenye hati hiyo za kaskazini mwa Afrika (Moroco na Misri).

"Leo (jana) tumeandika historia ya kipekee sio tu hapa Tanzania, bali kwa Bara la Afrika. Hii ni mara ya kwanza benki kutoka Bara la Afrika kutunukiwa cheti cha 'EDGE Assess'.

"Hili ni jambo la heshima sana kwetu na tuna kila sababu ya kujivunia mafanikio haya makubwa," ofisa huyo aliwaambia waandishi wa habari, akitamba kuwa hilo linathibitishwa na ukweli wa takwimu za The EDGE Certified Foundation.

Shirika hilo la Uswisi ndilo linaloongoza duniani kwa mbinu za tathmini na uthabiti wa viwango vya kibiashara katika suala zima la usawa wa kijinsia kazini.

Utaalamu wake huo ndio uliotumika kubainisha kuwa uwiano wa kijinsia katika Benki ya NMB hauishii tu kwa wafanyakazi wake wa ndani, bali hata kwa wanawake inaowahudumia sokoni na kushirikiana nao katika ujenzi wa taifa.

Takwimu za The EDGE Certified Foundation zinaonyesha kuwa dunia ikiendelea kuendekeza ubaguzi wa kijinsia, hasa mahali pa kazi, itapata hasara ya kiuchumi ya dola za Marekani kati ya Sh. bilioni 12 na Sh. bilioni 28 ifikapo mwaka 2025. Kiasi hicho kwa fedha ni karibu Sh. trilioni 28 na Sh. trilioni 65 mtawalia ambazo ni rasilimali fedha nyingi.

"Kampuni yenye uwiano wa kijinsia, mara nyingi ni yenye mafanikio kibiashara na kiuendeshaji," Akonaay alibainisha kuonyesha sababu kuwekeza katika eneo hilo kunalipa na ni faida kubwa kiuchumi na nyeti kimaendeleo.

Alisema utafiti umedhibitisha kuwa uwiano wa kijinsia ni kichocheo kizuri cha ubunifu na ukuaji wa kiuchumi, kuimarika kwa shughuli za uzalishaji mali na kuwapo utulivu wa kifedha na uwiano wa kipato.

Alisema NMB inatambua kuwa suala hili ni miongoni mwa vipaumbele vya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) ya Umoja wa Mataifa, akisisitiza umuhimu wake kimaendeleo ni pamoja na kuzingatia ukuaji wa biashara za kibenki.

Alibainisha faida nyingine za cheti cha EDGE Access ambayo ni hatua ya kwanza ya taasisi kuelekea kufanikiwa kuutokomeza kabisa ubaguzi wa kijinsia ni pamoja na NMB kutambulika kama mwajiri anayezingatia masuala ya usawa wa kijinsia kazini.

"Cheti hiki kutoka The EDGE Certified Foundation kinaiweka Benki ya NMB katika ramani ya kimataifa kama gwiji wa usawa wa kijinsia huku pia kikitambua dhamira na juhudi zetu katika nyanja ya usawa wa kijinsia mahali pa kazi.

"Kwetu usawa wa kijinsia sio tu katika utendaji kazi wetu, bali hata katika utoaji wa huduma zetu na ndio maana tunaendelea kuibua masuluhisho maalum kwa ajili ya wanawake ili kuwainua zaidi kiuchumi," alisema.

Aliongeza kuwa NMB pia imepiga hatua kubwa katika suala zima la kuongeza uwiano wa usawa wa kijinsia kwa kushirikiana na wadau hata wa kimataifa kama Shirika la International Finance Corporation (IFC).

Mwakilishi wake mkazi, Frank Ajilore alisema usawa wa kijinsia kazini una faida nyingi kibiashara na kiuchumi kwa kuwa kinamama wakiwezeshwa, wanachangia vizuri kasi ya maendeleo.

"Ni faraja kwetu kwa NMB kama mshirika wa IFC kuwa taasisi ya kwanza ya kifedha nchini, Afrika Mashariki na kote Afrika kutunukiwa Cheti cha EDGE kitakachoiwezesha kufanikiwa zaidi kibiashara na kutumika kama mfano wa kuigwa na kufuatwa na taasisi nyingine," "Ujumbe wangu mkubwa ni kwamba usawa wa kijinsia ni jambo la msingi na muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taasisi na uchumi wa nchi kwa ujumla," alisema.

Benki ya NMB yenye wafanyakazi zaidi ya 3,500 imepiga hatua kwenye eneo hilo na uwiano wake wa kijinsia umepanda kutoka asilimia 45 wanawake na asilimia 55 wanaume mwaka 2015 hadi asilimia 48 na 52 mtawalia mwaka huu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuanze sasa kukabili uhaba huu wa maji

**WATANZANIA** takribani milioni 60 wanaliona jua linavyozidi kuongezeka kila uchao na tatizo la maji likianza kutamalaki. Takwimu za mtandao wa water.org, zinaeleza kuwa huenda watu milioni nne wanakosa maji salama ya kunywa na kutumia kwa matumizi mengine hasa ya nyumbani kwenye maeneo mengi nchini.

Uhaba au ukosefu wa maji ni tatizo kubwa na yanapokauka watu wanakosa cha kunywa, au wanapata kidogo kisichotosha kwa mahitaji muhimu. Yanapokosekana hakuna usafi wa mavazi, vyombo na makazi. Lakini hakuna kumwagilia mazao mashambani hasa kwenye skimu za umwagiliaji na kuongeza mashaka ya upatikanaji wa vyakula. Ukosefu wa maji ni hatari hasa kwenye usafi wa mazingira, tatizo linatokana na uwezekano wa kusababisha magonjwa hatari ya kuhara, kuhara damu, kipindupindu na homa ya matumbo. Shida inaweza kuwa kubwa shuleni, vyuoni, kwenye maeneo ya mikusanyiko ya kutoa huduma kama hospitalini na hata magerezani wanakohudumiwa wafungwa.

Ukame huu wa sasa na uhaba wa maji unaonukia unatoa ujumbe kwa serikali na wadau kuwa kumekucha. Ni muda wa kuangalia miundombinu ya kufanikisha kupatikana majisafi kwa urahisi, mfano matangi ya kuyahifadhia, mabomba ya kuyasambaza, vifaa vya kuvuna maji ya mvua, vya kuchimbia visima vya ardhini na sementi ya kuvijenga visima na utaalamu wa kuyasambaza.

Tunaona kama ni mambo yanayohitaji nguvu kubwa na uwekezaji. Uhaba wa maji ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha ukame, jua kali na upepo ambavyo vyote vinakausha maji, mtoni na ardhini hivyo kuongeza ugumu wa kupata huduma hiyo. Uhaba wa maji unamaanisha ugumu si kwa familia hata wanyama pia. Tatizo liko kwa mifugo midogo kama kuku, bata, mbuzi na kondoo wachache ambao watu wanawafuga ili kuongeza kipato cha familia zao.

Ni wakati serikali na wadau kuangalia bei za vifaa au miundombinu ya kupata maji hayo kuanzia mapipa ikiwezekana zipungue ili Watanzania hasa wa kipato cha chini wamudu kununua. Jambo jingine ni kuangalia na kubuni teknolojia nyepesi ya kuvuna maji ya mvua yenye miundombinu isiyo na gharama kubwa ili itumike vijijini. Ni wazi kuwa licha ya kuwapo na ukame mkali kuna wakati nchi inaneemeka kwa mvua lakini maji yake hayavunwi kutokana na kukosekana miundombinu hasa kwa familia zisizo na kipato kikubwa. Ni vyema Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuanza kufikiria na kuishauri serikali namna bora ya kufanikisha masuala ya teknolojia rahisi ya kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi, lakini kushirikiana na wataalamu wa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijinini (CAMARTEC), kusaidia kutoa utaalamu na kuzalisha vifaa au miundombinu ya kuchimba, kuhifadhi na kusambaza maji kwa gharama nafuu vijijini.

Aidha, wataalamu hao waone jinsi ya kusaidia kupata teknolojia ya kusafisha maji ambayo si safi yanayopatikana kwenye mabwawa na madimbwi lakini kutokana na kukosekana kwa teknolojia ya kuyasafisha hakuna anayeweza kuyatumia.

Kwa mfano maeneo mengi jijini Dar es Salaam, yana mabwawa ya asili kama eneo la Mbezi Msumi, lakini maji hayo hayawanufaishi wananchi kutokana na kushindwa kuyasafisha kwa kuondoa matope, vimelea vya magonjwa na kuyasambaza majumbani.


Maji hayo yanabakia kutumika kwenye bustani badala ya kusaidia jamii kubwa inayokabiliwa na uhaba wa maji ya kunywa na matumizi muhimu kama kupika na usafi.

Tunaona wakati umefika wa kubuni na kufanya juhudi zote badala ya kusubiri mambo yawe mabaya hasa kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Uvuaji wa samaki kwa bomu kamwe usipewe nafasi

**HILI** la wale wavuvi wanaotumia njia haramu ya kutumia mabomu kujipatia samaki, kuanza kurejea tena linapaswa kukemewa mapema ili kulinda samaki wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa na mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Na sio kukuza uchumi wa nchi pekee, bali hata kuongeza ajira kwa vijana kwa sababu vijana wengi wamejiajiri huko wakifanya shughuli mbalimbali zinazohusiana na uvuvi.

Ukienda sehemu mbalimbali ambako zinafanyika shughuli za uvuvi utakutana na watu mbalimbali wakijishughulisha mahali hapo hii yote ni kutokana na uwepo wa samaki eneo hilo.

Picha inayonijia inaniambia suala hili la wale wanaovuna samaki kwa njia ya bomu kama halitakemewa mapema litaenda kumaliza mazalia mapya ya samaki hali itakayopelekea kupungua kwa samaki kwa miaka ya baadaye.

Juhudi za Nipashe kubaini kuwapo kwa wavuvi wanaotumia njia ya bomu zilianza pale waandishi wake walipotembelea bahari ya hindi katika soko la samaki msasani, na kuzungumza na mmoja wa wasimamizi wa mazingira ya bahari na fukwe, anayeshughulika na masuala ya takwimu, Juma Kichaka, alibainisha kuwapo kwa wavuvi haramu wanaotumia njia ya bomu wanaofanya shughuli hiyo kwa siri.

"Uvuaji wa samaki kwa njia ya bomu sasa umeanza kurudi sisi tuliopo hapa baharini huwa tunasikia mlio wa bomu lakini wanafanya kwa siri kwa sababu wao huwa wanaenda mbali zaidi kwa kuwa vifaa wanavyotumia vina uwezo mkubwa wa kuwafikisha mbali zaidi.

Kwa hiyo tumeshatoa taarifa kwa wakubwa wetu wa juu na mamlaka husika na ufuatiliaji umeanza lakini suala hili linatakiwa lipewe kipaumbele kwa sababu kuna madhara makubwa sana mtu anapotumia njia hiyo kujipatia samaki.

Madhara yake ni kwamba wanavunja matumbawe, samaki wanakimbia wanapatikana mbali na kupata shida katika kupata samaki, lakini kuna mambo mengi ambayo sio rahisi kuyaelezea kwa sasa lakini kikubwa tunaiomba serikali kuweka nguvu katika kukemea suala hili.

Katika mahojiano hayo na Juma Kichaka mmoja wa wasimamizi wa mazingira ya bahari na fukwe, pia alikemea wale wenye tabia ya kukata miti aina ya mikoko inayoota pembezoni mwa bahari akifafanua kuwa ina faida kubwa sana katika kustawisha samaki.

"Miti aina hiyo ina faida kubwa sana kwa samaki kwa sababu kuna samaki wengi ambao hawawezi kuishi bila mikoko kwa kuwa inatoa oksijeni kwa wingi ambayo ina mchango mkubwa kwenye ustawishaji wa samaki.

Kwa hiyo baada ya kukata miti hiyo kwa shughuli mbalimbali tunapaswa kuiongeza kwa kuipanda ili itusaidie katika kuhakikisha samaki wanaotegemea miti hiyo hawaadimiki"

Madhara ya kutumia njia hiyo kujipatia samaki ni mengi lakini kwa uchache wake ni kwamba huharibu mazalia ya samaki na kusababisha samaki kusogea mbali na hivyo kupelekea uhaba wa samaki.

Inasemekana kuwa mlipuko mmoja wa bomu una uwezo wa kuuwa viumbe wote walioko umbali wa mita za mraba 20 na kuuwa samaki wapatao 400 kwa wakati mmoja, kwa maelezo hayo mafupi unabaini uvuvi huo haramu ni kikwazo katika kustawisha samaki.

**TANGAZO**

# Letshego Bank — LETSHEGO BANK (T) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka/ Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 644 | 1,005 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 876 | 920 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | – | – |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 9,257 | 10,538 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 7 | 3 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | – | – |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | – | – |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | – | – |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | – | – |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | – | – |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo (Baada ya tengo la mikopo) | 14,764 | 15,957 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,580 | 2,966 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | – | – |
| 14 | Akaunti za Udhamini | – | – |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,594 | 852 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **30,723** | **32,241** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,167 | 2,668 |
| 18 | Amana za Wateja | 8,535 | 8,468 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa fedha Tslimu | – | – |
| 20 | Amana Maalumu | – | – |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za kuhamisha | – | – |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | – | – |
| 23 | Limibikizo za Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 330 | 108 |
| 24 | Dhima la Tozo Kwaajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Meneja | – | – |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | – | – |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | – | – |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,355 | 585 |
| 28 | Madeni | 3,200 | 5,200 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **14,587** | **17,029** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 20)** | **16,136** | **15,213** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | – | – |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 53,489 | 51,571 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | – | – |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (33,187) | (33,187) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | (4,166) | (3,171) |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa Chache | – | – |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **16,136** | **15,213** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | – | – |
| 39 | Mikopo chechefu (Zaidi ya Siku 90) | – | – |
| 40 | Mikopo chechefu (Zaidi ya Siku 30) | 10,050 | 9,488 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,362 | 6,219 |
| 42 | Mali nyingine chechefu | – | – |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 53% | 47% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 46.7% | 42.0% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 222% | 203% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 70% | 70% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 78% | 82% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -13% | 6% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -5% | -3% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka Sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka wa Sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 919 | 1,335 | 2,652 | 4,083 |
| 2 | Gharama za Riba | (281) | (302) | (794) | (1,145) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **638** | **1,033** | **1,858** | **2,938** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 1 | (462) | (20) | (598) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la Tengo katika Mikopo | (90) | (11) | (1,274) | 217 |
| **6** | **Mapato yasiyo na Riba** | **144** | **167** | **326** | **665** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1 | (2) | 48 | (5) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 114 | 112 | 248 | 495 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 29 | 57 | 30 | 175 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba** | **(1,675)** | **(1,762)** | **(5,027)** | **(5,680)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (785) | (968) | (2,349) | (3,061) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gawio | (890) | (794) | (2,678) | (2,619) |
| **8** | **Faida / (Hasara) ya Uendeshaji** | **(982)** | **(1,035)** | **(4,138)** | **(2,458)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (9) | (14) | (28) | (41) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Hasili Baada ya Kodi ya Mapato** | **(991)** | **(1,049)** | **(4,166)** | **(2,499)** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 77 | 83 | 81 | 124 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | (0) | (0) | (0) | 0 |
| 13 | Mapato ya Hisa zilizochujwa | (0) | (0) | (0) | 0 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 5 | 5 | 5 | 5 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -3% | -2% | -14% | -3% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa fedha za wanahisa | -6% | -4% | -26% | -6% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 158% | 112% | 169% | 117% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazo Zalisha | 1% | 3% | 1% | 3% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.09.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya Sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka Iliyopita 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka wa Sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I.** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (982) | (1,423) | (4,138) | (2,459) |
| | **Marekebisho Kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | 89 | 385 | 1,294 | 381 |
| | -Hasara Katika Mali za Kudumu | 260 | 187 | 592 | 200 |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji kabla ya Mabadiliko ya Mtajikazi** | **(633)** | **(851)** | **(2,251)** | **(1,877)** |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mikopo | 1,104 | 1,249 | 4,618 | 4,500 |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali nyingine | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,434) | 606 | (593) | (4,646) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za muda mfupi | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana Inayohitajika Kisheria | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 992 | (192) | 731 | (1,554) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (614) | (643) | (1,343) | 647 |
| | -Kodi iliyolipwa | (9) | (9) | (28) | (41) |
| | -Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **(594)** | **158** | **1,134** | **(2,970)** |
| **II.** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawiwo Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,002) | (65) | (702) | (265) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(1,002)** | **(65)** | **(702)** | **(265)** |
| **III.** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (2,000) | - | (2,106) | (1,500) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Madeni ya Muda Mrefu | 1,918 | - | 5,658 | 870 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawiwo Lililipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(82)** | **-** | **3,552** | **(630)** |
| **IV.** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | | | |
| | **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(1,678)** | **94** | **3,984** | **(3,865)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka | 12,466 | 12,372 | 6,801 | 7,141 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka** | **10,784** | **12,466** | **10,785** | **3,285** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2022
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa Sasa** | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **39,311** | **8,520** | **-** | **105.00** | **(33,288)** | **14,648** |
| 1 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 5,657 | - | - | - | - | 5,657 |
| 2 Mapato Mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | | - | - |
| 3 Miamala na wanahisa | - | - | - | | - | - |
| 4 Gawio lililolipwa | - | - | - | | - | - |
| 5 Ziada ya Kisheria | - | - | - | | - | - |
| 6 Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | | (4,166) | (4,166) |
| 7 Mengineyo | - | - | - | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **44,968** | **8,520** | **-** | **105** | **(37,453)** | **16,136** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **36,487** | **8,520** | **-** | **-** | **(28,202)** | **16,805** |
| 1 Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 2,824 | - | - | - | - | 2,824 |
| 2 Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | 105 | (105) | - |
| 3 Miamala na Wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| 4 Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| 5 Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| 6 Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | (4,981) | (4,981) |
| 7 Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **39,311** | **8,520** | **-** | **105** | **(33,288)** | **14,648** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uendeshaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikuwa na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,

| Jina/ Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Omar S. Msangi **(Mkurugenzi Mtendaji)** | | 20-Oct-2022 |
| Isaack Chahe **Meneja wa Fedha na Utawala)** | | 20-Oct-2022 |
| Rashid Sendoro **(Mkaguzi wa ndani)** | | 20-Oct-2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo juu chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benk na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, nazinaonesha hali halisi.

| Jina/ Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Simon Jengo **(Mwenyekiti wa Bodi)** | | 20-Oct-2022 |
| Noel Sangiwa **(Mkurugenzi)** | | 20-Oct-2022 |






## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

LBT PRICE LIST FOR Q4 - 2022

| Charge Type | Product / Service | TZS | USD |
|---|---|---|---|
| Minimum Opening Balance | LetsGo Flexi- Business Account | 100,000 | N/A |
| | LetsGo Flexi Dunduliza Account | 20,000 | N/A |
| | LetsGo Flexi- Group Account | 50,000 | N/A |
| | LetsGo Flexi -KIDS Account | 10,000 | N/A |
| | LetsGo Personal Account | 20,000 | 20 |
| | LetsGo Business Account | 100,000 | 100 |
| | LetsGo Mjasiriamali Account (Entreprenuer) | 15,000 | N/A |
| **Charge Type** | **Product / Service** | **TZS** | **USD** |
| Minimum Operating Balance | LetsGo Flexi- Business Account | 50,000 | N/A |
| | LetsGo Flexi Dunduliza Account | 20,000 | N/A |
| | LetsGo Flexi- Group Account | 50,000 | N/A |
| | LetsGo Flexi -KIDS Account | 10,000 | N/A |
| | LetsGo Personal Account | 10,000 | 10 |
| | LetsGo Business Account | 50,000 | 50 |
| | LetsGo Mjasiriamali Account (Entreprenuer) | 5,000 | N/A |
| **Charge Type** | **Product / Service** | **TZS** | **USD** |
| Monthly Maintenance Fee | LetsGo Flexi- Business Account | 2,000 | 2 |
| | LetsGo Flexi Dunduliza Account | 2,000 | 2 |
| | LetsGo Flexi- Group Account | 2,000 | 2 |
| | LetsGo Flexi -KIDS Account | Free | Free |
| | LetsGo Personal Account | 2,000 | 2 |
| | LetsGo Business Account | 8,000 | 8 |
| | LetsGo Mjasiriamali Account (Entreprenuer) | 2,000 | 2 |
| **Charge Type** | **Product / Service** | **TZS** | **USD** |
| Account Closing Fee | Saving accounts | 5,000 | 5 |
| | current accounts | 10,000 | 10 |
| **Charge Type** | **Product / Service** | **TZS** | **USD** |
| Balance Enquiry Fee | Umoja ATMs | 400 | N/A |
| | Other Local Banks ATMs (Within the country) | 700 | N/A |
| | Other Bank ATMs outside the country | 2,000 | N/A |
| | LetsGo Mobile | 300 | N/A |
| | LetsGo Wakala | 300 | N/A |
| **Charge Type** | **Product / Service** | **TZS** | **USD** |
| Account Statements Fee | Mini Statement Umoja ATMs | 400 | N/A |
| | Mini Statement Other Local Banks ATMs (Within the country) | 700 | N/A |
| | Mini Statement Other Bank ATMs outside the country | 2,000 | N/A |
| | Mini Statement LetsGo Mobile | 300 | N/A |
| | Mini Statement LetsGo Wakala | 300 | N/A |
| | Statement at the Branch (per page) | 1,000 | N/A |
| | Monthly E-Statement | Free | Free |

| Charge Type | Product / Service | TZS | USD |
|---|---|---|---|
| Cash Windraw ATM and Over the Counter | ATM Withdrawal at Umoja ATMs | 100 to 99,999=1500<br>100,000 to 400,000=1700 | N/A |
| | ATM Withdrawal at other Domestic banks | 3,500 | N/A |
| | ATM Withdrawal outside Tanzania | 5,000 | N/A |
| | Teller Withdrawal up to TZS 500,000 (For Flexi Accounts) | 3,000 | 3 |
| | Teller Withdrawal above TZS 500,000 (For Flexi Accounts) | 3,000 plus 0.15% of excess Amount Max charge: 50,000 | $3 plus 0.15% of excess Amount Max charge: $100 |
| | Teller Withdrawal - excess of third time in a month (For Flexi Accounts) | 8,000 | 8 |
| | Teller Withdrawal up to TZS 500,000 (For LetsGo Accounts) | 3,000 | 3 |
| | Teller Withdrawal above TZS 500,000 (For LetsGo Accounts) | 3,000 plus 0.15% of excess Amount Max charge: 50,000 | $3 plus 0.15% of excess Amount Max charge: $100 |
| **Charge Type** | **Product / Service** | **TZS** | **USD** |
| Cash Deposit Wakala | TZS 1,000 - 5,999,999 | Free | N/A |
| Cash Withdraw Wakala | From: TZS 1,000 - 4,999 | 400 | N/A |
| | From: TZS 5,000 - 9,999 | 700 | N/A |
| | From: TZS 10,000 - 19,999 | 1,200 | N/A |
| | From: TZS 20,000 - 39,999 | 1,500 | N/A |
| | From: TZS 40,000 - 49,999 | 1,800 | N/A |
| | From: TZS 50,000 - 99,999 | 2,200 | N/A |
| | From: TZS 100,000 - 199,999 | 3,500 | N/A |
| | From: TZS 200,000 - 299,999 | 4,700 | N/A |
| | From: TZS 300,000 - 399,999 | 5,800 | N/A |
| | From: TZS 400,000 - 599,999 | 6,300 | N/A |
| | From: TZS 600,000 - 799,999 | 6,500 | N/A |
| | From: TZS 800,000 - 999,999 | 7,000 | N/A |
| | From: TZS 1,000,000 - 1,999,999 | 7,200 | N/A |
| | From: TZS 2,000,000 - 2,999,999 | 7,500 | N/A |
| | From: TZS 3,000,000 - 3,999,999 | 8,000 | N/A |
| | From: TZS 4,000,000 - 4,999,999 | 9,500 | N/A |
| | From: TZS 5,000,000 - 5,999,999 | 9,800 | N/A |
| **Charge Type** | **Product / Service** | **TZS** | **USD** |
| Card Fee | Visa Card Issuance | 15,000 | TZS equivalent |
| | Visa Card Replacement | 15,000 | TZS equivalent |
| | Visa Card Annual Maintenance Fee | 6,000 | TZS equivalent |
| | Umoja Card Issuance | 10,000 | TZS equivalent |
| | Umoja Card Replacement | 10,000 | TZS equivalent |
| | Umoja Card Annual Maintenance Fee | Free | Free |

| Charge Type | Product / Service | TZS | USD |
|---|---|---|---|
| MoneyTransfer | Teller Money Transfer (intrabank same customer) | - | - |
| | Teller Money Transfer (intrabank different custoners) | - | - |
| | Alternative Channels Money Transfer (intrabank same customer) | 300 + Government Levy | TZS equivalent |
| | Alternative Channels Money Transfer (intrabank different custoners) | 300 + Government Levy | TZS equivalent |
| | Money Transfer (Umoja Banks) | 100 to 99,999 =1300<br>100,000 to 399,999 =1700<br>400,000 to 499,999 =2500<br>500,000 to 599,999 =3000<br>600,000 to 699,999 =3500<br>700,000 to 999,999 =4000<br>1,000,000 to 1,999,999 =5000<br>2,000,000 to 2,999,999= 6000<br>3,000,000 to 1,999,999 =7000<br>4,000,000 and above =8000 | TZS equivalent |
| | Money Transfer (TISS) | 10,000 | TZS equivalent |
| | Money Transfer (Western Union) | From TZS 6,500 | TZS equivalent |
| | Money Transfer (TT) | USD 65 | USD 65 |
| | All Incoming Transfers | Free | Free |
| **Charge Type** | **Product / Service** | **TZS** | **USD** |
| Bank to Wallet | From Bank to Mobile | 1,300 | N/A |
| **Interest Rates** | **Deposit Product / Service** | **TZS** | **USD** |
| Deposit Products | Savings accounts | 0-499,999 = 0%<br>500,000 -5,000,000 = 2.5%<br>5,000,001-20,000,000 = 3.0%<br>20,000,001-100,000,000=5.0%<br>100,000,001- 200,000,000 = 6.0%<br>200,000,001 - 300,000,000 = 7.0%<br>Above 300,000,000 = 10% | N/A |

| FOR SIGN OFF | | | |
|---|---|---|---|
| **NAME** | **ROLE** | **SIGN** | |
| LEAH PHILI | Ag. H.S.P.M | | |
| OMAR MSANGI | C.E.O | | |

**TANGAZO**

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka Mwaka iliyopita 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 13,489 | 15,985 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,577 | 11,727 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 45,554 | 44,496 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,245 | 405 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 22 | 41 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 26 | 35 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 84,546 | 80,187 |
| 12 | Mali Nyingine | 13,949 | 14,255 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 39 | 39 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 13,998 | 14,301 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **182,444** | **181,469** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 2,138 | 1,134 |
| 18 | Amana za Wateja | 119,738 | 123,718 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 654 | 61 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 6 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,340 | 4,728 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazoli | 1,301 | 958 |
| 27 | Dhima Nyingine | 16,137 | 16,484 |
| 28 | Madeni | 9,614 | 6,823 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **153,924** | **153,912** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **28,521** | **27,557** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 27,797 | 27,797 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (11,561) | (10,819) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (353) | (1,317) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 12,637 | 11,896 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **28,521** | **27,557** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,099 | 765 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 13,306 | 13,303 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 5,463 | 6,591 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 73 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15.6% | 15.2% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 14.9% | 15.4% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 71.3% | 67.9% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 49.0% | 47.6% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 72.0% | 68.9% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.9% | 0.0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.5% | 0.0% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-22 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 6,748 | 6,031 | 20,149 | 17,846 |
| 2 Gharama za Riba | (1,701) | (2,059) | (5,093) | (6,408) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,046** | **3,972** | **15,056** | **11,439** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (239) | (598) | (2,095) | (2,587) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,706** | **1,472** | **5,027** | **4,025** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 104 | 151 | 289 | 304 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,245 | 837 | 3,680 | 2,529 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 357 | 484 | 1,057 | !"#$%& 1,192 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,550)** | **(6,060)** | **(18,341)** | **(18,389)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,590) | (3,288) | (9,713) | (9,444) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,960) | (2,772) | (8,628) | (8,945) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **964** | **(1,214)** | **(353)** | **(5,512)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (0) | 0 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **964** | **(1,214)** | **(353)** | **(5,512)** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **964** | **(1,214)** | **(353)** | **(5,512)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 388 | 413 | 388 | 413 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 35 | (54) | (13) | (246) |
| **15 Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.1% | -4% | -0.3% | -5% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 13.7% | -27% | -1.7% | -34% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 82.2% | 123% | 91.3% | 123% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 15.7% | 14% | 15.7% | 15% |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2022

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Silvest Arumasi ***(Mkurugenzi Mtendaji)*** | | |
| Mr. Arnold Makanda ***(Afisa Mkuu wa Fedha)*** | | |
| Mr. Chemo Mutani ***(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)*** | | |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Miss.Catherine Nchanasaa Kimaryo | | |
| 2. Prof. Josephat Daniel Lotto | | |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.09.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 964 | (1,903) | (353) | (5,512) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Hasara Katika Mali | 478 | 487 | 1,449 | 1,793 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (4,359) | (1,205) | (6,937) | 2,933 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (0) | 0 | (0) | (1) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (2,383) | 4,685 | (158) | 1,497 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (1,058) | 2,355 | (4,412) | (7,230) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 2,821 | 2,447 | 4,898 | 4,249 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,017) | 1,285 | 8,347 | (1,893) |
| - Kodi Iliyolipwa | 0 | (127) | (127) | (157) |
| - Mengineyo (bainisha) | (403) | (411) | (1,250) | 1,142 |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(4,957)** | **7,613** | **1,455** | !"#$%&**(3,178)** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (153) | (168) | (320) | (267) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(153)** | **(168)** | **(320)** | **(266)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | (17) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | (586) | (556) | (1,142) | (1,132) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(586)** | **(556)** | **(1,142)** | **(1,149)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (5,695) | 6,890 | (7) | (4,593) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 26,084 | 19,195 | 20,395 | 31,972 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **20,389** | **26,084** | **20,389** | **27,379** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2022

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022** | **27,797** | **2,432** | **(12,101)** | **4,857** | **5,888** | **28,874** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (353) | 0 | 0 | **(353)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | -72 | 0 | 72 | - |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 611 | -611 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.09.2022** | **27,797** | **2,432** | **(11,914)** | **4,246** | **5,960** | **28,521** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **10,984** | **2,432** | **(5,627)** | **3,684** | **16,992** | **28,465** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (4,298) | 0 | 0 | **(4,298)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 11,427 | 5,565 | 0 | 0 | (16,992) | **(0)** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,225) | 1,225 | 0 | **(0)** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.09.2021** | **22,411** | **7,997** | **(11,151)** | **4,909** | **(0)** | **24,167** |




217115502



Kamishna wa Tume ya Utumishi nchini, Balozi Adadi Rajabu (wa sita kulia), akijadiliana jambo na viongozi na wadau mbalimbali, baada ya kukagua jengo la maabara ya Shule ya Sekondari ya Muheza Muslim, wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wizara yaonya wananchi uharibifu vyanzo vya maji

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, amewataka wananchi kuacha kuvamia na kuharibu vyanzo vya maji.

Pia amekemea tabia ya baadhi watu kufanya makazi katika maeneo yasiyostahili, ikiwamo kwenye vyanzo vya maji, hali inayochangia uharibifu wa mazingira.

Khamis alitoa angalizo hilo jana katika mkutano wa hadhara na wananchi wa eneo la Ubaruku, Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wakati wa ziara ya Kamati ya Mawaziri Wanane wa Wizara za Kisekta.

Alionyesha kutofurahishwa na uharibifu wa vyanzo hivyo baada ya kutembelea eneo la Mto Ruaha na Mnazi katika Kijiji cha Mwanavala vilivyomo ndani ya hifadhi.

Naibu waziri huyo alionya tabia ya baadhi ya wananchi kufanya shughuli za kibinadamu, ikiwamo kuingiza mifugo na kufanya makazi katika maeneo yenye vyanzo vya maji.

"Tumeshuhudia vyanzo vya maji vimeharibiwa sana, maji yale ndio yanayotusababishia sisi kuishi, maji yale ndio yanayosukuma umeme ukapatikana, maji yale ndio viumbe hai wanaishi, sasa tumeliona lile bonde kule hali ni mbaya, tukikaa kimya tutaelekea pabaya," alitahadharisha.

Khamis alisema hajafurahishwa na tabia ya ukataji miti holela inayofanyika katika baadhi ya maeneo nchini hali inayosababisha uharibifu wa mazingira.

Alisema endapo wananchi wataendelea na tabia ya ukataji miti, mvua itakuwa ni ndoto, hali itakayosababisha ukame ambao ni chanzo cha ukosefu wa maji kwa ajili ya mifugo na shughuli za kilimo.

"Ndugu zangu ninaomba niwaambie mazingira ndio kila kitu tusipoyatunza mazingira hayatatutunza, cha msingi ninataka nitoe wito Tanzania nzima watu wapande miti, watunze vyanzo vya maji, watunze mazingira, watu waheshimu sheria na taratibu zote zinazohusiana na masuala ya mazingira," alisema.

Kamati hiyo imeshatembelea mikoa mbalimbali na inaendelea na ziara yake kwenye mikoa mingine ya Iringa, Njombe na Ruvuma.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA NISHATI**

**Telegramu "NISHATI".**
**Simu Namba: +255 26 2322018**
**Nukushi: +255 26 2320148**
**Barua pepe: ps@nishati.go.tz**

**Mji wa Serikali-Mtumba,**
**Mtaa wa Nishati,**
**S. L. P. 2494,**
**40474 DODOMA.**

**TAREHE: 27.10.2022**

**UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

Kwa mujibu wa kifungu cha 8(2) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, Waziri wa Nishati, Mhe. January Y. Makamba (Mb) amewateua wafuatao kuwa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa **miaka minne** kuanzia tarehe **20 Oktoba 2022.** Hatua hii inakuja baada ya Rais kumteua Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Profesa, Mark J. Mwandosya, tarehe **15 Agosti 2022.**

1. Bw. Fadhili J. Manongi – Mjumbe
2. Bi. Victoria M. Elangwa – Mjumbe
3. Bw. Haruna S. Masebu – Mjumbe
4. Dkt. James A. Mwainyekule – Mjumbe
5. Mha. Ngosi X. Mwihava – Mjumbe
6. Mha. Modestus M. Lumato – Mjumbe na Mkurugenzi Mkuu

**IMETOLEWA NA**
**MHA. FELCHESMI J. MRAMBA**
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA NISHATI**

SENSA TANZANIA 2022

217115202


# Wachangia milioni 70/- ujenzi wa shule

**Na Steven William,** MUHEZA

WADAU wa elimu nchini wamejitokeza na kuchangia Sh. milioni 70 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya Shule ya Sekondari Muheza Muslimu iliyoko wilayani Muheza mkoani Tanga.

Harambee ya kuchangia ujenzi huo ilifanyika wakati wa sherehe za mahafali ya kidato cha nne shuleni huko, wanafunzi 111 wakihitimu kidato cha nne huku mgeni rasmi akiwa Kamishna wa Tume ya Utumishi nchini, Balozi Adadi Rajabu.

Wadau hao walichangia fedha hizo baada ya Balozi Adadi kuwaomba wachangie ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo, huku naye akichangia tani tano za saruji.

Balozi Adadi alisema ametafuta wadau kuchangia shule hiyo hususani kuendeleza ujenzi wa maabara ili watoto wasome kwa bidii na kufanikiwa kuendelea na masomo ya elimu ya juu.

Alisema kuwa baada ya shule hiyo kuwafurahisha wadau hao kwa kufaulisha wanafunzi kwa miaka mitatu mfululizo, waliamua kuchangia Sh. milioni 70 kwa ajili ya ujenzi wa maabara na miundombinu mingine.

Alisema katika shule hiyo wana mpango wa kupanua miundombinu yake ili ianze kudahili wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba Tanzania, Neemia Mchechu, alisema kuwa kutokana na umuhimu wa elimu anachangia Sh. milioni sita kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo ili watoto wasome katika mazingira ubora.

Mkurugenzi wa TSN, Faroughu Baghoza, alisema ametafuta wadau mbalimbali wa kuchangia ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo na wamefanikiwa kupata Sh. milioni 70 na Kamishna wa Tume ya Utumishi, Balozi Adadi amechangia saruji tani tano.

Wadau wa Elimu Wilaya ya Muheza, Makame Seif, Mohamed Maghoza na Said Bahgoza kwa nyakati tofauti waliwashukuru wadau hao kwa kuchangia fedha hizo na kuonyesha nia ya kuendeleza elimu wilayani hapo.

Mkuu wa Shule hiyo, Ramadhani Makea, alibainisha kuwa shule yao inajivunia mafanikio makubwa kielimu, akitoa mfano kwamba mwaka 2019 wanafunzi 94 walifaulu kwenda kidato cha tano na vyuo mbalimbali, mwaka 2020 walifaulu wanafunzi 89 na mwaka 2021 walifaulu wanafunzi 78.

Meneja wa shule hiyo, Mohamed Kijunge, alisema shule hiyo pia inakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo kutokuwa na jengo la maabara, kutokuwa na miundombinu ya maji na ufinyu wa eneo.



# DC ageuka mbogo kampuni kuchelewesha mradi wa maji

**Na Oscar Assenga,** LUSHOTO

MKUU wa Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, Kalist Lazaro, amewataka wakurugenzi wa Kampuni ya M/S PNR Services ya jijini Dar es Salaam waliopewa zabuni ya kuvuta maji kutoka Hifadhi ya Msitu wa Magamba hadi katika Mji wa Lushoto kujisalimisha ofisini kwake.

Amesema kampuni hiyo hadi sasa wameifanya kazi kwa asilimia 20 tu wakati mradi huo wanapaswa kuukabidhi kwa Mamlaka ya Maji Lushoto (RUWASA) Januari mwakani.

Alitoa agizo hilo juzi alipkuwa katika chanzo cha maji cha msitu huo, kwamba alisikitishwa kuona mkandarasi huyo amelipwa zaidi ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya kazi hiyo lakini hakuna kazi iliyofanyika.

Hivyo alimwagiza msimamizi wa mradi wa kampuni hiyo, Singo Omari, aliyemkuta eneo la mradi kuwataarifa wakurugenzi wake kuwa anawahitaji ofisini kwake Oktoba 27, mwaka huu, majira ya asubuhi wajieleze kwa nini wasichukuliwe hatua.

Alisema tangi ya maji lenye uwezo wa kubeba lita 600,000 bado halijajengwa, usambazaji wa bomba za maji za umbali wa km 14 kutoka Msitu wa Magamba hadi Mjini Lushoto bado mtaro haujachimbwa wala mabomba hayajafika eneo la mradi.

Alisema dharau za wakurugenzi wa kampuni hiyo waliyoifanya hawatavumiliwa, lazima waeleze ni kwa nini muda wote hawajafanya kazi na pesa wameshalipwa.

Meneja wa RUWASA katika Wilaya ya Lushoto, Erwin Sizinga, alisema kuwa Mkurugenzi wa Kampuni hiyo hana ushirikiano na ofisni yake kwani wamekuwa wakifanya kazi wanavyotaka na kutoa sababu nyingi zisizokuwa na msingi tangu walipopewa kazi hiyo.

Alisema Mji wa Lushoto unahitaji sana maji kutoka chanzo cha Msitu wa Asili wa Magamba na mradi huo ukikamilika utakuwa na uwezo wa kutoa lita 150,000 hadi 160,000 kwa saa.

Meneja wa Kampuni ya M/S PNR SERVICES, Omari Singo, alikiri kutokamilika ndani ya muda kwa mradi huo na kumwomba Mkuu wa Wilaya kumpa muda zaidi ili aweze kuzungumza na wakurugenzi wake.

## Wananchi walalamikia uchafuzi Mto Mkurumuzi

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKAZI wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga wamesema wapo hatarini kupatwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na watu wasiojulikana kutupa taka katika Mto Mkurumuzi ambao maji yake yanatumika katika shughuli za nyumbani.

Hali hiyo imelalamikiwa na baadhi ya wananchi ambao wanatumia maji hayo kwa matumizi ya nyumbani pamoja na kufua nguo.

Akizungumza na Nipashe, mkazi wa Kijiji cha Sega wilayani Muheza, Sada Ramadhani, alisema kuwa vitendo vinavyofanywa na baadhi ya watu wanaoishi kando kando ya mto huo kutupa taka ambazo zinachanganyika na uchafu kunahatarisha afya zao.

Ramadhani alisema kuwa watu hao wanaharibu mazingira katika mto huo ambao ni chanzo cha maji kwa kufanya jalala la kutupa takataka.

Simon William mkazi wa Mtaa wa Mbaramo alisema kuwa katika kipindi hiki cha kiangazi wanatumia maji hayo kwa matumizi mbalimbali ya nyumbani lakini sasa baadhi ya watu ambao nyumba zao zipo karibu na mto huo wanachafua mazingira.

Hivyo waliiomba Idara ya Afya na wale wanaohusika kutunza mazingira kuhakikisha wanafuatilia suala hilo, kwamba watakaobainika wawachukule hatua kali za kisheria ikiwamo kukamatwa na kufunguliwa mashtaka ya kuchafua mazingira.

**Hali hiyo imelalamikiwa na baadhi ya wananchi ambao wanatumia maji hayo kwa matumizi ya nyumbani pamoja na kufua nguo.**



Ofisa ugani wa kampuni ya dawa za mifugo na vyakula (AFRIFARM), Emanuel Senge (wa pili kushoto), akitoa maelezo kuhusu huduma zao kwa wananchi katika maonyesho ya mkutano mkuu wa tisa wa chama cha wataalamu wazalishaji wa bidhaa za wanyama na samaki jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# TEMDO yagundua teknolojia ukaushaji mihogo muda mfupi

**Na Woinde Shizza** ARUSHA

TAASISI ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO), imegundua teknolojia mbadala ya kukausha mihogo kwa muda mfupi.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonyesho ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo(SIDO), yaliyofanyika jijini Arusha, Ofisa Uhusiano na Masoko wa TEMDO, Dk.Sixbert Mmasi, alisema teknolojia hiyo ni mpya ambayo imetokana na uvumbuzi wanaoufanya kwenye taasisi hiyo.

Alisema wakulima wa muhogo mara nyingi wamekuwa wakipata hasara kubwa kutokana na zao hilo kuharibika hasa wakati wa mchakato wa ukaushaji.

Akizungumzia kuhusu teknolojia hiyo alisema awali wakulima hao walikuwa muda na siku nyingi kufanya shughuli ya ukaushaji na wakati mwingine mazao yao kuharibika.

Dk.Mmasi alisema uwapo wa teknolojia hiyo utawezesha kurahisisha kazi kwa wakulima wakati wa usindikaji kwa kuwa watatumia siku moja kamaliza kazi nzima tofauti na ilivyokuwa mwanzo walitumia siku zaidi ya 10 na nishati ya jua kama chanzo cha kikuu cha ukaushaji.

Alisema: "Kwa kutumia teknolojia hii, wakulima watavuna mihogo yao na kuikausha siku hiyo, kadhalika na kufungasha unga kwenye vifungashio tayari kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kwa kweli imekuwa ni mkombozi mkubwa kwa kuwa sasa tutaweza kutoa thamani halisi ya zao la mhogo,"alisema.

Licha ya kuzungumza hayo pia aliwataka wajasirimali ambao ni wamiliki wa viwanda kuhakikisha wanaitumia taasisi hiyo, hasa teknolojia hiyo na mashine mpya walizozivumbua kwa kuwa zinalenga kuinua uchumi wa Taifa.

Alisema wamekuwa wakiwawezesha wadau mbalimbali wa viwanda kwa kuwapa elimu ya njia sahihi ya kutumia mashine kwa ajili ya matumizi ya ndani ya viwandani.

Alisema: "Lengo letu ni kuhakikisha sekta ya viwanda inakuwa kwa kuwapo kwa mapinduzi makubwa kwa kuwa tuna uwezo wa kutengeneza vitu ambavyo awali viliagizwa na kuzalishwa nje ya nchi, lakini kwa sasa tunazalisha na kubuni kwa umahiri unaotakiwa, rai yangu kwa Watanzania na wamiliki wa viwanda watumie taasisi hii kuwa wabunifu".





# Halmashauri ya Jiji Tanga yawaita wawekezaji

**Na Oscar Assenga,** TANGA

HALMASHAURI ya Jiji la Tanga imewaita wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuchangamkia fursa za uwekezaji zilizoko katika Jiji hilo kutokana na uwapo wa maeneo yanayotosha kwa ajili ya viwanda.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Jiji hilo, Dk. Sipora Liana, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu fursa za uwekezaji zilizoko katika Jiji hilo, namna walivyojipanga kupokea wawekezaji.

Aliyataja maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya madini katika Jiji hilo yapo katika eneo la Maere, Chumvini, Kisosora, Ndaoya, Machui, Tongoni, Chongoleani, Mwarongo.

Alisema katika maeneo hayo yana hekta 212 na yanafaa kwa ajili ya maeneo ya viwanda vya saruji, chokaa, chumvi pamoja na rangi.

"Katika maeneo ya madini tunawaalika wawekezaji wakubwa na wadogo wa madini na chumvi hivi sasa uzalishaji ni mdogo sana unakuta wazalishaji wadogo wanazalisha kama tani 6000 ambazo hazitoshi, hivyo tunawaalika kuja kuwekeza na tumeahidi hakutakuwa na urasimu wa kupata maeneo hayo ambayo tayari yameshapimwa," alisema Dk. Sipora.

Alisema pia katika maeneo hayo yanayofaa kwa ajili ya sekta ya uvuvi yaani uchumi wa buluu kutokana na uwapo wa bahari kuna fursa ya kufanya uvuvi na kuwaalika wawekezaji wanaoweza kuja kufanya uvuvi.

"Lakini unenepeshaji wa majongoo bahari, kilimo cha mwani hao wote tunawaita lakini ufugaji wa samaki kwenye vizimba na uvuvi wa kutumia vyombo vya kisasa," alisema.

Alisema wameamua kuwaita wawekezaji hao kwa ajili ya shughuli za uwekezaji na viwanda ambavyo ni muhimu.

Aidha, aliwataka wawekezaji ambao wanakwenda kuwekeza visiwani Zanzibar kupitia uchumi wa buluu wanaweza kuja Tanga ambako nako kuna fursa ya uwekezaji huo ambao ni muhimu kwa maendeleo.




Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhandisi Richard Luyangu, akizungumza wakati akifunga maonyesho ya 17 ya Kanda ya Kaskazini ya wajasiriamali wadogo na wa kati yaliyoandaliwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) katika viwanja vya Makumbusho jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## RC awaagiza wakurugenzi kusimamia miradi kwa weledi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri saba za mkoa huo kuhakikisha wanasimamia miradi inayokelezwa na serikali inakamilika kwa wakati na ubora.

Alitoa agizo hilo jana alipokuwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule la Msingi Kikwe, iliyoko wilayani Arumeru pamoja na Zahanati ya Kijiji cha Maksoro.

Mongela alisema serikali inafanya jitihada ya kuwaletea wananchi maendeleo kwa kutoa fedha za miradi, hivyo ni vyema kila mkurugenzi akasimama ipasavyo kwenye eneo lake ili miradi hiyo ikamilike na kuleta tija kwa wananchi.

Alisema katika ukaguzi wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Msingi Kikwe iliyoko Halmashauri ya Meru serikali imetatua kero ya uhaba wa madarasa kwa kutoa Sh. milioni 60 kwa ajili ya ujenzi.

Aidha, aliupongeza uongozi wa wilaya hiyo kwa ushirikiano mzuri na wadau wa maendeleo ambapo mwekezaji RIJKZWAAAN QSEM alichangia Sh. milioni 163 katika ukamilishaji wa Zahanati ya Maksoro.

"Pia nawapongeza wananchi nao wamechangia nguvu kazi zao na zahanati hii ikikamilika itahudumia watu zaidi ya 600 wa Kijiji cha Maksoro na vijiji vingine vya jirani, hivyo siyo jambo dogo hili,"alisema.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wawekezaji katika suala la maendeleo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma.

Mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Kikwe, John Mbise, aliishukuru serikali kwa kutoa Sh.milioni 60 ya kujenga madarasa matatu.

# Watu wenye ulemavu waomba kukumbukwa katika jamii

**Na Allan Isack,** MONDULI

WATU wenye ulemavu wameomba kukumbukwa katika jamii hasa kwenye nafasi za vyombo vya utoaji wa uamuzi kwa kuwa bado kuna tatizo la ushirikishwaji makundi hayo.

Rai hiyo ilitolewa na Kiongozi wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Wilaya ya Monduli, Dora Msuya, wakati wa hafla ya wiki ya AZAKI, kusema kuwa kundi hilo limekuwa halipewi kipaumbele au kushirikishwa kwenye baadhi ya mambo hasa kwa mabaraza ya kutoa uamuzi.

"Ushirikishwaji wetu ni mdogo sana kwenye mabaraza na shughuli za upangaji wa bajeti, hivyo tunaomba kila mtu atambue kuwa sisi tunahaki kama makundi ya watu wengine,"alisema Dora.

Alisema mikopo ya asilimia mbili wanayokopeshwa na halmashauri ni midogo na wakati mwingine inacheleweshwa, hivyo aliomba utaratibu wa uboreshwaji kufanyika ikawamo kuongeza kiwango cha ukopeshaji.

Dora alisema pia kuna umuhimu wa kundi hilo wakapewa msaada wa kupatiwa elimu kwa kuwa baadhi yao hawajasoma.

"Tunaomba kupewa fursa ya elimu ya kawaida na ile ya ujasiriamali kwa kuwa baadhi yetu hawakufanikiwa kusoma na hilo likifanyika litasaidia kuongeza wigo wa kipato cha familia kutoka na kazi wanazofanya," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Rose Mhina, alisema mpango wa ushirikishwaji wa makundi hayo unaanzia katika mikutano ya vitongoji, vijiji na kata, lakini wako wananchi hawafahamu kinachoendelea katika maeneo yao kwa kuwa hawahudhurii kwenye mikutano hiyo.

Alisema suala la utoaji wa mikopo na urejeshaji una utaratibu wake na wamekuwa wakiwajali ila vijana wamekuwa wakisuasua katika urejeshaji, kwamba wamekuwa wakitumia vyombo vya dola.

"Nusu ya vijana hawarejeshi mikopo kwa wakati hadi tutumie vyombo vya dola kuwasaka, lakini wanawake wamekuwa waaminifu wanarejesha kwa wakati," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Foundation For Civil Society, (FCS), Francis Kiwanga, alisema wiki ya AZAKI kwa mwaka huu imekuwa ya kipekee kwa kuwa wamefanya maonyesho na kwenda kwa wananchi kusikiliza matatizo yanayowakabili na kutafuta njia mbadala za utatuzi.

Alisema shirika hilo limekuwa likifadhili mashirika mengine na vikundi kwenye wilaya mbalimbali nchini kwa ajili ya mafunzo na kutekeleza miradi.



Ukurasa 14

**Simulizi; ubunifu vyoo vya kuhamisha ndani ya mageuzi makubwa ya wakati**



Ukurasa 16

Kilimo hifadhi suluhu kunusuru hatari milima Lyamba lya Mfipa



Ukurasa 20

**Wanaafya, wanahabari Dar waingia ubia operesheni chanjo Uviko 19 mkoa**

VITA UKATILI JINSIA

# Waziri Dk. Gwajima 'mguu kwa mguu' mtaani kusaka amani afya

- Asema: Wanaonishangaa, nami nawashangaa

**Na Yasmine Protace**

MATUKIO ya ukatili katika jamii yamekuwa yakiripotiwa kila mara nchini, baadhi ya wanaofanyiwa ukatili huo wamekuwa wakitoa taarifa, huku wengine wakibaki kimya pale wanapofanyiwa ukatili huo.

Kukaa kimya kwa watu wanaofanyiwa ukatili kunaelezwa kuna mchango wa matukio ya ukatili kuongezeka, kwa sababu wanaowafanyia ukatili hawachukuliwi hatua, kutokana na uhalisia wanaotendewa wanakaa kimya.

Hali ya kuongezeka matukio hayo ya ukatili, serikali sasa imejipanga kuendelea kuwachukulia hatua kwa wanaoripotiwa kufanya ukatili, mojawapo ya mikakati ni kwa serikali kuweka madawati ya jinsia katika maeneo mbalimbali, lengo ni kutumia wananchi pale wanapofanyiwa ukatili.

Hivi karibuni, Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, ameahidi kutokaa ofisini wakati hali hiyo inaendelea; badala yake atadumu kutembelea maeneo ya kijamii kusikiliza vilio vyao na matukio ya kikatili.

"Wasionielewa, wanaona kama nakosea kuzurura nje. Mimi naenda kila uchochoro kujionea mambo yaliyopo mitaani," anaeleza waziri, akitaja kwamba ni hali ya kusikiliza kero za wananchi waliko, ambako kunasaidia kujua aina za magumu wanajamii wanakutana nazo katika maeneo yao.

Waziri anafafanua kwamba, matukio ya ukatili kijinsia yanazidi kuongezeka kila mwaka na



Wakazi wa jijini Dar es Salaam, wakiwa katika picha ya pamoja, baada ya kuzindua ofisi ya Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni. **PICHA: YASMINE PROTACE**

nchini Tanzania, takwimu za mwaka uliopo zinaonyesha watoto 11,499 walilawitiwa.

Pia, anaongeza kwamba, asilimia 60 ya watoto walibakwa wakiwa majumbani watendaji wakiwa ndugu zao, huku asilimia 40 ni waliolawitiwa wakiwa njiani kuelekea shule.

Dk. Gwajima aliyekuwa akizindua ofisi za Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni, Dar es Salaam, anatanguliza mtazamo wake kwamba, matukio ya ukatili yanapaswa kukemewa jamii iachane nayo, ana angalizo:

"Pamoja na kufanyiwa ukatili watoto hao, ni asilimia 12 tu ndio walioripoti katika madawati ya kijinsia kuwa wamefanyiwa ukatili."

Anasema, licha ya kuwepo kamati za kijamii zilizoundwa kusaidia kuondoa ukatili katika jamii, bado matukio hayo yanaendelea kutokea ndani ya jamii, hata kuwa sehemu ya vigezo vinavyompeleka mitaani kwenye jamii akivafanyie kazi.

Waziri anaainisha mizunguko yake,kwamba amepanga kujumuisha vikundi vya wajane, akavione na kusikiliza kero zao, vilevile kupambana na matukio ya kikatili, hata hospitali ambako kuna madawati ya kijinsia yanayowasaidia wale waliofanyiwa ukatili.

Maeneo mengine ambayo amepita anataja ni kwenye vikundi vya soko la Machinga, Dar es Salaam, akiwa na lengo mahsusi kupata ngazi ya ukatili wa kijinsia wanayokutana nao katika shughuli zao.

"Wasiojua wajibu wangu kupitia idara yangu,wananishangaa ninavyotumia muda mwingi kwenda mitaani kutatua kero za wananchi. Siwezi kukaa ofisini bila ya kuzunguka mitaani na kuzisikiliza kero za wananchi,' anasema.

Kwa mujibu wa waziri, dira na mwelekeo ni kutembelea maeneo ya shule, vyuoni kuangalia uwepo wa madawati ya kijinsia na jinsi yanavyofanya kazi.

**SALAMU KIPUNGUNI**

Waziri Gwajima akiwa ziarani katika Kata ya Kipunguni, jijini Dar es Salaam, anampongeza mkazi Mariam Chacha, aliyekuwa anatumikia ukeketaji wa mabinti, ambaye sasa ameacha kufanya ukeketaji, baada ya kuwezeshwa kifedha na elimu kutoka kituo cha taarifa na maarifa.

"Mariam alikuwa akiwakeketa watoto na kulipwa ujira, kutokana na kufanya kazi ya ukeketaji kwa watoto hao," anasema Waziri Gwajima, akisema kilichomuingiza mama huyo katika kazi hiyo ni hali ya kukosa kipato na baada ya kupatiwa shughuli mbadala ya kipato ameuacha ukeketaji.

Katika hilo, anaipongeza asasi ya TGNP Mtandao kwa kujitoa kwa hali na mali, kuwapatia mafunzo ya aina mbalimbali katika vituo vya taarifa na maarifa.

"TGNP Mtandao mmefanya kazi kubwa katika kuviwezesha vituo vya taarifa na maarifa. Kwa sasa, matunda yanaonekana," anaeleza waziri.

Mariam Chacha, mama aliyejitoa katika ukeketaji, anaeleza kilichomfanya ajikite sana katika kazi hiyo, kikuu ni kukosekana elimu yoyote juu ya ukatili kijinsia kwa watoto hao wa kike.

" Baada ya kupatiwa elimu juu ya masuala ya ukeketaji na athari zake, niliweza kuacha kufanya kazi hiyo. Kwa sasa nimewezeshwa mtaji na nimeweza kujiingizia kipato," anasema Mariam.

MAZINGIRA

MTAALAMU AFANYA YAKE...

# Simulizi; ubunifu vyoo vya kuhamisha ndani ya mageuzi makubwa ya wakati

**Na Beatrice Moses**

HARUFU mbaya ni kero katika jamii. Ni kati ya mambo yanayoweza kuharibu utulivu wa akili ya binadamu, pia ni ishara kuwa mazingira ya eneo husika siyo salama kiafya.

Kero hiyo ya harufu katika baadhi ya maeneo ikiwemo ukutani inazua maswali ya kutosafishwa eneo; harufu ya mikojo kwenye majengo, vichochoro, hata pembezoni mwa vituo vya daladala.

Katika kero hiyo ya harufu mbaya na uchafuzi wa mazingira, ndipo mbunifu Peter Marealle, anaona fursa kwa kupata wazo la kutafuta suluhisho, akibuni vyoo vinavyohamishika.



Mtaalamu Peter Marealle, akiwa na choo kinachohamishika, maalum cha kumsaidia mlemavu. **PICHA: BEATRECE MOSES.**

### UBUNIFU NA TUZO

Ni wazo, mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Caps, Peter Marealle, analifanyia kazi na sasa linampa mafanikio makubwa hata kampuni yake kutunukiwa tuzo tatu tofauti.

Tuzo walizopata ni: Kampuni bora kitaifa, kati ya ndogo na za kati za 2021; tuzo ya kitaifa ya huduma bora kitaifa, katika kampuni ndogo na kati kwa mwaka 2021 wakati mwaka huu 2022, pia imepata tuzo ya kampuni bora kati ya ndogo na kati kwa Afrika Mashariki.

Mkurugenzi Marealle, anaisimulia Nipashe namna hali ilivyo kero kutokana na harufu mbaya, binafsi akiifanya kuwa fursa, japo anakiri kukumbana na changamoto kadhaa katika utekelezaji wake.

"Nilibaini kwamba, kumekuwa na uchafuzi wa mazingira katika baadhi ya maeneo, hasa kwenye maeneo ya ujenzi wa majengo mapya, kwenye sherehe na misiba.

"Nikajiuliza jinsi gani naweza kutengeneza choo ambacho nitakuwa nakodisha kwenye maeneo hayo, ili kushawishi matumizi ya vyoo?"anahoji mkuu huyo.

### MWANZO WA MAONO

Hapo ana simulizi ya mwaka 2000, kulifanyika shindano la urembo Tanzania katika ukumbi wa Yatch Club, Masaki jijini Dar es Salaam na akatakiwa kwenda kutoa huduma ya choo.

Ilikuwa kwenye kambi ya mazoezi, anasema akapewa sharti kuhakikisha anatoa huduma nzuri ya choo cha muda kambini hapo.

Akaitekelezaje? Marealle anasema, hatua ya kwanza akaomba tofali na akazipanga vyema, kisha akaweka mbao na choo cha kisasa, huku chini kukiwekwa jaba walilolazimika kulibadilisha kila lilipojaa.

Mkurugenzi huyo anasimulia, ndipo ukawa mwanzo wa safari

> Nilibaini kwamba, kumekuwa na uchafuzi wa mazingira katika baadhi ya maeneo, hasa kwenye maeneo ya ujenzi wa majengo mapya, kwenye sherehe na misiba.

yake kutoa huduma ya choo na baada ya hapo, akaanza kupokea maombi kuhitaji vyoo na akalazimika kuviandaa kwa kutumia uzoefu wa ufundi, aliyojifunza wakati akisomea kilimo na ufugaji. Anasema, akaanza kwa kutengeneza vyoo vinavyohamishika akitumia mbao na akaziweka za pande mbili, kwa wanaume na wanawake.

Marealle anasema, ni ubunifu ulioendana na changamoto, kwani mbao zilipatikana kwa shida, hivyo akatafuta mbadala wa kutumia bati, ambazo nazo hazikuwa imara kwa kuwa ziliharibiwa kwa ukali wa mkojo.

### HADI AFRIKA KUSINI

Anasimulia hatua nyingine ya mafanikio, akaenda kwenye Mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), wakati wa uongozi wa Rais Dk. Benjamin Mkapa, ambako akanunua vyoo hivyo na hata alipofikisha sokoni nchini, akakuta hitaji ni kubwa sana.

Marealle anasifu ni hali iliyomuongezea mtaji na akainua biashara, huku ikisaidia kuboresha huduma hiyo, binafsi akieleza: "Wakati huo sikuwa na wafanyakazi wa kutosha, vyoo vilikuwa 15. Idadi hii ilikuwa ni vichache kulinganisha na mahitaji.

"Nakumbuka, nilikuwa nalala kwenye gari ili niweze kuvibadili kulingana na mahitaji. Tuliweka kwenye maeneo tofauti ikiwamo kwenye maegesho ili madereva nao waweze kupata huduma hiyo muhimu,"

Anasema katika wazo la kujitanua kibiashara ya vyoo, akaenda kwenye maonyesho ya Sabasaba nchini, alikokutana na raia wa Afrika Kusini, aliyekuwa anauza vyoo vya kapu, vikiwa ni vya staili tofauti.

Marealle anafafanua, ni vyoo vyenye chemba ndogo na juu yake kuna viroba sita kwenye kifaa cha duara chenye gurudumu inayoruhusu kuzunguka ili kusogeza viroba, vinachuja mkojo kwenda chini.

Marealle anaelezea choo hicho kwamba, katika hatua hiyo kinyesi kinapojaa kwenye kiroba duara kinachozungushwa kuruhusu kingine, kilichojaa kinakaushwa kwa dawa maalum, hata kinaweza kutumika kama mbolea shambani.

Anakiri kuvutiwa nayo, hata akawaomba wakala wa vyoo hivyo nchini, lakini ikawa ngumu kupata mteja, akimaanisha watu hawakuvielewa, pia hawakuvutiwa kwa matumizi yao, hivyo mkataba ukaisha.

Anasema, katika harakati zake kuboresha huduma hiyo ya vyoo, akajiongeza kwa kutafuta kwenye mtandao, ndipo akapata kampuni inayouza vyoo vya kisasa vya kuhamishika, hata akaagiza vinne. Anakiri, akahamasika hata akaongeza idadi kwa kuagiza vyoo 20.

### ANAKOKWAMA

Marealle anaanza na utambulisho kwamba, kuna dawa maalum inayotumiwa kumwagwa chooni na kutokana na ukali wake, inaua wadudu na kudhibiti harufu kwa siku 10, iwapo hakuna matumizi ya maji.

"Tumekumbana na changamoto. Nafikiri inachangiwa na utamaduni wa watu wengi hapa nchini mazoea ya matumizi ya maji ni makubwa, hivyo husababisha dawa hiyo ambayo ni ya gharama kubwa kutumika kwa kiwango kikubwa.

"Kuna mahali ambako tumeweka vyoo vyetu kwenye soko, ikiwa ni kuhakikisha tunashiriki kwa namna moja katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira, lakini cha ajabu ni kwamba wanaoenda kutumia ni wachache, huku unashagaa wengine wanajisaidia kwenye chupa za maji zilizotumika," anasema.

Mareale anaeleza, wamebaini baadhi ya watu wanaogopa hata kunywa maji, tahadhari ni kutokuwepo huduma ya choo, jambo analoamini linahatarisha afya, kwa kuwa wataalamu wa afya wanasisitiza katika, unywaji maji ya kutosha.

Kutokana na kukua huduma hiyo na mahitaji kuongezeka, wamelazimika kutafuta mkopo kwenye benki kadhaa, nako anasema akapata changamoto ya dhamana.

"Baada ya kuhangaika sana kuna benki ilitukubalia kukopa kwa dhamana ya mali zetu tulizokuwa nazo ambayo ilikua ni samani na vyoo husika, walitukopesha milioni 10 kwa riba ya asilimia 49,"anasema.

Analalamika kuwa riba hiyo ilikuwa kubwa, lakini hawakuwa na mbadala katika jitihada za kuboresha huduma yao, kwa maana ya hitaji la gari la kusafirisha vyoo na kununua dawa kulinda afya za wateja wao.

### USTAWI WA KAMPUNI

Marealle anasema, kampuni hiyo imekuwa na kustawi kwa kuwa sasa ina waajiriwa 49, pia imekuwa ikitoa ajira za muda, kulingana na eneo wanakohitajika kupeleka vyoo hivyo, hata kufika mikoa tofauti. Hadi sasa anasema, kuna jumla ya vyoo 250, vilikuwemo vilivyo rafiki kwa wenye ulemavu.

Mbunifu huyo anaitafsiri shughuli hiyo katika hisia aina mbili, upande mmoja biashara na nyingine huduma, ambako maeneo kama penye msiba amefanya kwa bei nafuu zaidi.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

KARAGWE DISTRICT COUNCIL

## THE FINANCIAL STATEMENTS FOR THE KARAGWE DISTRICT COUNCIL FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE 2021

217115502

AFYA

# Kilimo hifadhi suluhu kunusuru hatari milima Lyamba lya Mfipa



Shughuli za kilimo ukanda wa Lyamba la Mfipa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MAISHA ya Watanzania wengi walioko vijijini yametawaliwa na shughuli kuu mbili kiuchumi; kilimo na ufugaji. Ni rahisi kukutana na wakulima ambao pia ni wafugaji, au wafugaji wanaofanya kilimo. Vyote kwa ujumla, vimeajiri sehemu kubwa ya watu; zikizalisha pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Kimsingi, ufugaji na kilimo hutumia ardhi kama mtaji wa awali, ufugaji ukihitaji nyasi za malisho, huku kilimo kikihitaji ardhi kupanda na kukuza mazao.

Hitaji la ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji hushindana na mahitaji mengine ya kiuchumi. Ardhi ni rasilimali muhimu kuhifadhi misitu na wanyamapori. Kuwepo kwa hifadhi za taifa, mapori ya akiba, mapori tengefu, hifadhi za jumuiya, maeneo ya mtapanyo na shoroba za wanyamapori hutokea juu ya ardhi.

Kwa ujumla, ardhi inabaki kuwa rasilimali muhimu kwa uchumi wa watu na uhifadhi wa rasilimali za nchi. Hivyo, uendelezaji shughuli za kiuchumi na usimamizi wa rasilimali za maliasili, unazua swali muhimu kwa jamii ambalo ni; "je, nini kifanyike ili kukuza kilimo na uchumi, na kwa wakati huohuo kulinda rasilimali za asilia kama misitu na wanyamapori?"

**MAREJEO MAKUU**

Shughuli zinazoathiri utunzaji mazingira; licha ya kilimo na ufugaji kuwa shughuli kuu kiuchumi nchini, ni bahati mbaya bado zinafanyika kwa kukata miti kupata mashamba na kuna wakati hufanyika ndani ya maeneo oevu.

Kusafisha mashamba na kulima kwenye maeneo chepechepe (mfano vinyungu mkoani Iringa),

> **LEAT, inayotekeleza miaka mitano ya Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili, inataja mtazamo wake ni kuona mbegu ya kilimo- hifadhi iliyopandwa katika vijiji vya mradi, inakua chachu ya kilimo bora.**

kumesababisha wadau wa uhifadhi kuona kilimo kisichofuata taratibu kama shughuli haribifu na adui wa maendeleo ya uhifadhi.

Uharibifu unaojitokeza kwenye kilimo; Kilimo cha vijijini bado kinatajwa kutawaliwa na kuhama. Wengi hulima maeneo yaliyoinuka kipindi cha mvua na kuhamia mabondeni na pembezoni mwa vyanzo vya maji, kipindi cha kiangazi.

Hiyo inaangukia athari kuu mbili. Moja, kilimo cha kuhama hukata miti mingi na ya thamani kwa mazingira ya vijiji, huku ikiondoa makazi ya wadudu kama nyuki wanaofanya zaidi ya asilimia 70 ya kuchavusha mazao.

Pili, kilimo hasa cha mabondeni, kinaharibu vyanzo vya maji, kwa kujaza tope kwenye chanzo, kuondoa uoto muhimu unaolinda vyanzo vya maji na kujaa sumu za viuawadudu.

**MLIMANI LYAMBA LYA MFIPA**

Lyamba lya Mfipa ni safu zinazopatikana mikoa ya Songwe, Rukwa, na Katavi, ambako kulitafitiwa. Ni safu zinazoendelea kuvutia na kuvamiwa makundi ya wafugaji na wakulima, hasa kwa sababu upande wake wa chini unapakana na Ziwa Rukwa na kuna uwanda unaofaa kwa ufugaji.

Upande wa milimani, hutumika kama kimbilio pale mvua zinaponyesha. Wafugaji hupendelea kupandisha mifugo yao juu ya mlima, kupisha kilimo cha mahindi, mpunga, alizeti, mtama, na ufuta ambacho hufanyika mvua zinaponyesha.

Hali kadhalika, upande wa juu wa safu za milima unahifadhi jamii za wakulima. Kilimo cha kuhama, kifanyikacho pembezoni mwa mito na miferejini, pamoja na kilimo kifanyikacho nyakati za kiangazi kimesababisha kulegea kwa ardhi.

Ardhi na udongo uliolegea, husombwa na maji kipindi cha mvua na kusababisha kutengenezeka kwa tope ambalo hujaza Ziwa Rukwa inayofanya kupungua kina cha maji.

Kutokana na uharibifu wa safu za milima Lyamba lya Mfipa, mito imeendelea kupanuka kwa kiasi kikubwa na kuharibika kwa miundombinu hasa madaraja na barabara. Mawasiliano hukatika na kuna wakati, kulishuhudiwa kusababisha hasara kubwa kipindi cha mvua.

Sehemu kubwa ya uoto huo sasa inapotea, kutokana na kuongezeka shughuli za kiuchumi, shughuli hizo zimeendelea kuondoa rasilimali za misitu, hivyo kutoweka faida za kiikolojia ambazo watu wamekuwa wakizipata.

**HATUA ZINAZOFAA**

***Je nini kifanyike kunusuru?***

Kitaalamu inaelezwa, ili kunusuru safu za Milima ya Lyamba lya Mfipa dhidi ya uharibifu tajwa, jamii inatakiwa kugeukia ufugaji na ukulima rafiki na mazingira, hasa kwa sababu kilimo na ufugaji wa Tanzania hutegemea kudra za kimazingira kama mvua, uchavushaji, na utengamano wa kimazingira.

Hivyo wakulima na wafugaji, sasa wanatakiwa kuwa wadau wa kwanza wa usimamizi wa mazingira, hasa kwa maliasili kwa sababu ufugaji na ukulima hutaka mvua, rutuba, nyasi, na kadhalika.

**KILIMO HIFADHI**

Kuhifadhi misitu, ardhi na wanyamapori huathiriwa na shughuli za kiuchumi hasa kilimo na ufugaji. Ni bahati mbaya kuwa shughuli hizo hazizuiliki ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

Kinachoweza kufanyika ni kuelekeza na kuweka taratibu kwa watu walime na kufuga, huku wakiheshimu taratibu na sheria na kuogopa madhara ya kiafya, kiikolojia endapo kilimo hakitafuata taratibu za sheria na misingi ya uhifadhi.

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili unatambua kuwa Watanzania ni wakulima na wafugaji. Uzoefu ndani ya vijiji pembezoni mwa safu za Lyamba lya Mfipa, unaonyesha vijiji havijawahi kutenga ardhi za kuchunga mifugo. Viko vichache vilivyotenga maeneo madogo ambayo hayawiani na wingi wa mifugo iliyopo.

Asasi za LEAT na mshirika wake RUSUDEO, sasa zimeamua kutoa elimu ya kilimo -hifadhi, kuwawezesha wananchi kulima, kupata mazao kwa uhakika na kulinda mazingira, dhidi ya changamoto kama kumomonyoka ardhi, mabadiliko ya tabianchi, na matumizi madogo ya mbolea.

**KWINGINEKO KULIVYO**

Maeneo mengi nchini hadi sasa yana mashamba darasa, yakilenga kufundisha wananchi kilimo rafiki, hali inayopiganiwa na wadau wa mazao mbalimbali kwa kipindi kirefu.

Mtazamo kutoka asasi ya LEAT ni kwamba ni busara sasa kutumia matokeo ya mafunzo, kuhakikisha jamii na vizazi vinalindwa.

Pia, inaelezwa, uhusiano wa safu za milima ya Lyamba lya Mfipa na uwanda wa Ziwa Rukwa unafundisha kuwa shughuli zote juu ya safu za milima huathiri maisha, uoto, na uchumi wa maeneo chini ya mlima.

Pia, kilimo kinachofanyika juu ya mlima husababisha mmomonyoko wa udongo unaozalisha tope chini. Hali kadhalika, kukata miti na uoto pembezoni mwa mito, kunasababisha mmomonyoko wa ardhi, na kuchukua mazao, nyumba hata na watu.

LEAT, inayotekeleza miaka mitano ya Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili, inataja mtazamo wake ni kuona mbegu ya kilimo- hifadhi iliyopandwa katika vijiji vya mradi, inakua chachu ya kilimo bora.

Pia, inasimama katika matarajio kuona shughuli za kilimo zinaheshimu mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji, huku wananchi wake wakiendelea kuzalisha kwa kilimo na ufugaji, bila kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Eneo lingine la kunuia, ni hali ya kuwafanya wananchi kuachana na shughuli hatarishi kama kukata kuni kwenye milima ya Lyamba lya Mfipa, kwa kupanda miti kuzunguka makazi yao iwasaidie nishati, wanapoweza kutumia majiko banifu ambayo LEAT imewafunza.

Eneo lingine inasisitizwa ni kwenye kilimo bora bila ya kuathiri uharibifu wa mazingira.

MAZINGIRA

# Mwenye miaka 30 majini afunguka bahari ni nini, uvuvi unavyofanyika

- Ratiba maji isivyopoteza dakika, upekee wa samaki kamba

**Na Pilly Kigome**

UNAPOMTAJA kwa jina Mshame, leo hii ana umri miaka 47. Lakini, katika taaluma yake ya uvuvi anayodumu nayo, kujinasibu na hata kumpatia riziki, yumo tangu mwaka 1990, sasa ni mwenyeji hasa.

Akiwa yu mtaalamu kamili wa uvuvi, pia anaijua vyema bahari na kwa kina, hapo Mshame kwa ujuzi wake binafsi katika mazunguzo na Nipashe, anaitafsiri bahari kuwa ni "mkusanyiko wa maji tofauti kutoka mtoni na chemchem, chini ya ardhi, yenye ladha ya chumvi, yanayoungana na kusafiri katika mfumo wa kutiririka na haufahamiki mwanzo wala mwisho wake."

Mkongwe Mshame anaeleza kuwa bahari mara zote ni 'kubwa kuliko nchi kavu; ikitafsiri kwa msemo 'haina mwisho'. Hivyo, anafafanua ni 'kubwa kuliko ardhi' na kutokana na sababu hizo, chini yake kunakuwapo ardhi, ikirejea nadharia kwamba ikichimbwa tena kunapatikana bahari nyingine chini yake.

Pia, anataja maji ya bahari katika mifumo miwili katika mfumo wake wa kila siku, ambao ni maji kupwa (kutoka) na maji kujaa (kuingia),akieleza kwamba, katika mfumo huo, maji huwa yana kupwa na kujaa kwa kupishana katika saa 24 na dakika 45, kila siku na daima hakuna mabadiliko.

Hapo anafafanua kwa mfano, kwamba siku moja maji yanapojaa saa 7.00 mchana, huwa yanakupwa kesho yake saa 7. 45 mchana; au yakijaa saa 1.00 asubuhi, basi kesho yake yataondoka saa 1.45 asubuhi.

Pia, ana ufafanuzi mwingine wa ziada kwamba, vitendo vya kupwa na kujaa hutokea mara mbili kutwa.

**ILIVYOGAWANYIKA BAHARI**

Mshame anaeleza bahari imegawanyika katika vipindi vinne ndani ya miezi 12, vivyo hivyo ndani ya vipindi hivyo, kila kipindi kimoja kimegawanyika tena katika vipindi viwili.

Vipindi hivyo anavitaja kuwa ni: Kusini, Kaskazini, Mashariki na Magharibi, lakini anavitaja katika lugha ya kivuvi vinafahamika kwa majina ya; Kusi (Kusini), Kaskazi (Kaskazini), Matalai (Mashariki) na Mande (Magharibi).

Kitaalamu anasema; Kusi ina jumla ya miezi minne katika kipindi chake, ambacho inatoa vipindi viwili baharini, miezi miwili bahari inakuwa imetulia na miezi miwili bahari inakuwa haijatulia yaani kuchafuka.

Hali kadhalika katika Kaskazi; kuna jumla ya miezi minne, ikitoa miezi miwili bahari inakuwa imetulia na miezi miwili mingine, bahari inachafuka.

Anaeleza kwamba, bahari ikichafuka kwa upande wa Kaskazi inakuwa na dhoruba (kimbunga) na makadirio ya dhoruba inakadiriwa ni mwezi wa 12 hadi Machi.

Pia, Mshame anaeleza miezi ya Machi bahari huwa inachafuka kiasi na makadirio ya kuanzia Aprili hadi mwezi Julai, inakuwa siyo sawa baharini.

**VIUMBE BAHARINI**

Mshame, anasema bahari ina maumbile ya miamba na tambarare ambayo imebeba tope, mchanga mawe na majani ambavyo hivyo vyote ni vizalia vya makazi ya viumbe.

Anasema, bahari huzalisha viumbe hai pekee na kila kinachopatikana ndani yake, kuna sehemu yake maalum anakopatikana na kuweka makazi, ikiwemo pa kuzaliana, ambako wapo wanaoishi kwenye matope, mchangani na wanaodumu katika majani.

Viumbe hai wanaopatikana baharini, anasema nao wamegawanyika katika makundi makuu mawili; la kwanza ni wenye makazi na pili, wasio na makazi.

Anafafanua kwa wenye makazi, ni samaki wanaokaa sehemu moja, wanajenga miji ama nyumba zao maalum kwenye miamba hawahami na kuna sehemu moja za mazalia na pa kuishi.

Kwa mujibu wa mvuvi huyo, samaki hao huwa hawahami na hata wao wavuvi wanawajua ni samaki wa aina zao, wanawakuta katika eneo hilo, hapo anakuja na mifano halisi kwa samaki hao, ni sehewa, jodari, change, kolekole na tasi.

Pia, anawataja wasio na makazi maalum wana tabia ya kuhama, hawakai sehemu moja, kama vile papa, chuchunge, mbaasi ni baadhi ya mifano ya samaki wasio na makazi maalum.

Samaki hao nao kwa ujumla, wamegawanyika katika makundi tofauti, wanaokula majani tu, akitoa mfano pono na chuchunge.

Pia, mvuvi huyo anataja wapo wanaokula wadudu, mchanga na mawe kwa, mfano change, 'redfish' na kolekoleo.

Kundi lingine analifafanua ni wanaokula samaki wenzao tu na daima hawali kitu kingine zaidi. Hapo kuna mifano anayotoa ya samaki; papa, mzia, chewa na hata jodari.



Kulivyo ufukwe wa bahari. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Samaki kamba.

> **Samaki aina ya kamba, anatajwa kuwa na msimu, ambaye hapatikani kwa miezi yote baharini kutokana na mazalio yake yanayotokana na mifumo ya mito kutoka kwenye tope.**

**UPEKEE WA KAMBA**

Kwa samaki aina kamba, mvuvi Mshame anakiri anapendwa sana nchini na nje, kulingana na wapenzi wakivutiwa, akiwa na asili inayompa ladha ya ziada na ni samaki anayevuliwa na kupatikana baharini, chimbuko ni katika maji baridi mtoni, kuingia baharini.

Mshame anamueleza kwamba anapatikana kwa mfumo wa mvua katika mwingiliano wa bahari na mto. Katika kipindi hicho cha mvua,wanatoka mtoni kuingia baharini.

Samaki aina ya kamba, anatajwa kuwa na msimu, ambaye hapatikani kwa miezi yote baharini kutokana na mazalio yake yanayotokana na mifumo ya mito kutoka kwenye tope.

Samaki huyo anapatikana baharini, asili yake hasa ni mtoni ambako anaingia baharini kwa mfumo wa maji mengi hasa kipindi cha mvua kunapokuwa na makutano ya mwingiliano wa mito akitoa mfano wa mito Ruvu, Pangani na Rufiji, pale maji yake yanakutana na njia ya bahari.

Kamba anakadiriwa kuishi miezi mitatu hadi sita, katika uhai wake inakadiriwa hawezi kuishi kupita miezi hiyo hadi sita na upatikanaji wake uko katika kipindi cha miezi Aprili hadi Julai kila mwaka.

Hicho anakitaja ni msimu wa mavuno kwa samaki aina hiyo, kwa kuwa hali ya hewa ina baridi na samaki hao wanatoka kwenye mkondo wa maji, wanakuja juu kwa ajili ya kutafuta malisho.

Mshame anaeleza, ndio inakuwa neema kwa wavuvi wafanyabiashara na watumiaji wapenzi, kukikadiriwa aina zipatazo saba za samaki kamba, ya kwanza kwa mujibu wa mvuvi Mshame, wana jina Kamba Kochi (Robosta).

Ni aina anayoitaja inashi chini ya miamba na kwenye kina kirefu, ikikadiriwa urefu wastani wa mita 30 hadi 20 kutoka chini ya bahari.

Anasema wanaishi muda mrefu na inakadiriwa uzito wao ni kati ya kilo moja hadi 15; wa pili wana jina Jumbo; wa tatu 'Tiger Weusi'; nne, Kamba Weupe (White); tano ni 'Kamba Weusi' sita Dagaa Kamba; na wa mwisho ni Uduvi.

Mshame anawapa sifa ni adimu na ladha yake ina mvuto kwa wengi. Huwa na kawaida anapoingizwa jikoni, anabadilika rangi kuwa rangi ya chungwa, mithili amepakwa rangi.

Wana asili ya kuishi kwenye pori la mikoko baharini, akisema wako tofauti na samaki wengine wenye asili ya moja kwa moja kuzaliwa baharini.

Ni samaki wanaovuliwa kwa nyavu na Tanzania wanapatikana kwa wingi, wakiwa na soko kubwa nchi kama Botswana, Afrika Kusini, Kenya na Dubai.

Nchini kuna viwanda kadhaa ambavyo ni wakala wa kusindika samaki huyo, ikiwemo Dar es Salaam na Mafia.

AFYA

# Ukatili wa watoto Moro washitua Chuo kikuu, chabuni kituo cha vita

• Waziri naye 'anunua kesi', aungana nacho vitani




Tukio la kufunguliwa kituo cha Mkono kwa Mkono cha Chuo Kikuu cha Jordan, mahsusi kupamabana dhidi ya ukatili katika jamii.
**PICHA ZOTE: ASHTON BALAIGWA**

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

Nchini Tanzania kunatajwa kuwepo ukatili dhidi ya watoto, ikigusa vitendo kama udhalilishaji kijinsia mkoani Morogoro na hasa katika manispaa ya Morogoro limekuwa juu, hata Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan cha mjini hapo, kinaamua kujikita katika harakati za kuvalia njuga suala hilo.

Katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015, inaelezwa wanafunzi wa Idara ya Sheria na Ushauri Nasihi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan walienda kufanya mafunzo kwa vitendo katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro na kuleta taarifa ya kuwepo vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Hilo lilifanya chuo hicho kutafuta ufadhili na kuendesha warsha maalum kwa viongozi na watendaji wa serikali za mitaa kutoka katika kata tatu za Kichangani, Bigwa na Tungi, katika Manispaa ya Morogoro, ikiwa na jumla ya washiriki 180.

Mkuu huyo wa Chuo Kikuu cha Jordan, Profesa Mapunda, anasema warsha hiyo ilikusanya viongozi wa jamii,wenyeviti na watendaji wa kata,Maofisa Ustawi wa Jamii,viongozi wa dini, polisi jamii na maofisa elimu, waliofunzwa wajibu wao kwa mtoto kupitia Sheria ya Mtoto ya Tanzania.

Pia, anasema ikaangalia majukumu yao katika kuwalinda na kuwatetea watoto, aina za ukatili na madhara yake kwa watoto na hapo kukaibuliwa mambo makuu kadhaa.

> **Utafiti mwingine uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba, Tehran huko Iran nao ulionyesha kuwa kuchua misuli kwa mafuta ya mizeituni wakati wa ujauzito, hupunguza uwezekano wa kupata michirizi ya ngozi.**

Anasema walikiri kuwapo ukatili dhidi ya mtoto upo katika jamii walikotoka na wanaofanya vitendo hivyo ni watu walio karibu nao, kama vile wana familia, majirani na walimu.

### KUZALIWA KITUO

Mkuu wa Chuo hicho Kikuu kishiriki cha Jordan Profesa Mapunda, anasema kutokana na matokeo ya taarifa zilizopatikana katika kongamano la viongozi, wataalamu kutoka idara ya sheria na saikolojia na wote walitoka na wazo la kuwa na huduma endelevu kwa ajili ya kumsaidia mtoto.

Anasema, ni wazo lililofikishwa kwa shirika la Wasalvatori na kukaagizwa kufanyika utafiti wa kupima uzito wa tatizo katika jamii ya Morogoro mwaka 2018, ambako chuo kilitafuta watafiti binafsi wenye uzoefu na matatizo ya watoto, wakawachunguza kwa kina hata kubainisha mambo mazito.

Profesa Mapunda, anasema katika kipindi cha mwaka 2016/17 matukio 444 yaliripotiwa kwenye dawati la jinsia, ikigusa ukatili kimwili, pamoja na wa kijinsia.

Anafafanua kuwa ukatili kimwili uliobainika ukajumuisha wanafunzi kuchapwa viboko,kupigwa vibao na makofi, kunyimwa chakula na kupewa kazi ngumu.

Profesa Mapunda anasema sababu kubwa ya ukatili huo ilionekana ni ugomvi wa wazazi, kukosekana mbinu bora za malezi na utukutu wa watoto, ulevi uliopindukia na msongo wa mawazo kwa wazazi.

Anasema upande wa ukatili kingono, ilionekana zaidi ubakaji wa watoto, ulawiti kwa wavulana, hata walionyanyaswa kuathirika kisaikolojia na kihisia.

Mkuu huyo wa chuo kikuu, anasema pia utafiti ulibainisha ukatili wa watoto upo kwa asilimia 60 ukimaanisha kuna wastani wa kila watoto 10, wako watoto sita wanaokumbuna na ukatili kila siku.

Profesa Mapunda anasema, walianza kutafuta fedha na ilipofika mwaka 2020 ujenzi wa kituo hicho ulianza kwa kufuata miongozo yote ya serikali, pamoja na Kurugenzi ya Manispaa ya Morogoro, hatimaye umekamilika mwaka jana.

### MRATIBU KITUO

Mratibu wa Mradi wa Kituo hicho cha Mkono kwa Mkono,Virginia Bamurange,anasema wamebaini sababu kuu ya kuwepo vitendo vya ukatili dhidi ya watoto mojawapo ni mfumo wa utafutaji riziki na wazazi kutowajibikia malezi ya watoto wao, vyote akitaja vinachangia kuongezeka kwa vitendo hivyo.

Rai ya Mratibu Bamurange, anawataka wanawake kuwajibika katika malezi ya watoto ili kupunguza vitendo vya ukatili kwa watoto, kwa kuwa kutowajibikia watoto kunaonyesha mchango mkubwa dhidi ya usalama na malezi yao.

### MKAKATI WA KITUO

Mratibu wa Mradi wa Kituo hicho, Bamurange anaeleza sasa wametoa baiskeli kwa wadau waliojikita katika mapambano hayo katika Manispaa ya Morogoro, ili kuwarahisishia huduma za usafiri.

Anasema msaada huo wa baiskeli una thamani ya jumla Sh.milioni 38.5 zilizotolewa na mashirika ya kimisionari kutoka nchi za Ujerumani na Ireland. Pia, anasema kabla ya kukabidhiwa baiskeli hizo wahusika hao jumla yao 188 katika mitaa na kata 15 za Manispaa Morogoro, walipatiwa mafunzo ya kubaini watoto wanaofanyiwa ukatili.

"Hawa wanajitolea na wamekuwa na jukumu la kufuatilia nyendo za watoto kwenye mitaa yao na hivyo, baiskeli hizi walizopewa zitakuwa chachu kubwa ya kutekeleza majukumu yao," anaeleza Mratibu Bamurange.

Mratibu wa Huduma za Kituo cha Mkono kwa Mkono, Esther Andrew, anasema mradi umejikita katika kufanya kazi katika kata 15 kati ya 29 za Manispaa ya Morogoro, kusaidia katika sehemu mbili; Tiba na Kinga kwa jumla watoto 700.

Anaeleza sehemu ya tiba, itaunganisha afya ya kisaikolojia inayotolewa na wataalamu wake na tiba ya majereha ya mwili, itakayotolewa na madaktari wa magonjwa ya binadamu, pia tiba ya kisheria.

Mratibu huyo anasema kwa upande wa tiba ya kinga itahusu kuelimisha jamii juu ya haki za watoto ,aina na madhara ya ukatili kwa watoto na kwamba walimu waliopo katika shule hizo za kata 15 watatumika pamoja na machampioni kutoka katika kila mtaa.

Anasema, kuwa kituo hicho hadi sasa kinatoa msaada wa kisheria, tiba ya kisaikolojia na ushauri nasaha, matibabu ya awali na huduma za kisaikolojia na unasihi kwa wazazi na walezi, kikiwa na safu ya madaktari na polisi kutoka Dawati la Jinsia la watoto.

### MGANGA WA KITUO

Mganga wa kituo hicho cha huduma ya Mkono kwa Mkono,Dk. Elias Mtungilwa, anasema ukatili kwa watoto umekuwa ukichangiwa na wazazi au walezi kukimbizana katika kutafuta riziki za kila siku na kukosa muda wa kuwa karibu na watoto kujua matatizo yao.

Anasema, jamii nyingi zinaingia katika janga kubwa kutokana na utandawazi na vitu vingine ambavyo vinawafanya baadhi ya wazazi na walezi kupata ugumu wa kuwatunza na kuwalea watoto wao ambacho ndicho kizazi cha baadaye.

### POLISI JAMII

Inspekta Msaidizi wa Polisi Mwanaidi Lwena,kutoka Dawati la Jinsia na Watoto la Jeshi la Polisi mkoa wa Morogoro, mjini hapa anasema ukatili kwa watoto umekuwa ukishamiri na

INAENDELEA UK.19

MAZINGIRA

DARASA LINGINE 'SHAMBA' LA KAMBA'...

# Ukataji mikoko unavyosambaratisha upatikanaji wa samaki baharini

**Na Halfani Chusi**

LICHA ya umuhimu wa samaki, lakini shughuli za kibinadamu zinatajwa kuwa moja ya sababu zinazochangia kupungua kwao. Hapo dodoso za Nipashe, zinabaini kuwa wapo watu wanaofanya shughuli hizo kwa kujua na kutojua.

Imebainika sababu kubwa inayochangia kupungua samaki ni pamoja na ukataji miti ovyo, ikiwamo mikoko inayotajwa kuwa na msaada mkubwa kwa ustawishaji wa samaki.

Ni uwezo unaotokana na miti hiyo kuvuta hewa ya ukaa na kutoa hewa ya oksijeni, ambayo ni mchango mkubwa kwa kukuza samaki.

Lakini, kwa kutokulijua hilo, inatajwa baadhi ya wakazi hukata miti hiyo inayoota kando ya bahari na kuigeuza kuni, wengine hutumia kwa kuchonga vitanda, kuchoma mkaa na shughuli nyingine za kibinadamu

Mtu anapolitazama hilo kwa undani, anabaini hata tarehe zinavyosonga mbele, kukosekana bidhaa hiyo adimu hasa katika mlo, sababu kubwa ni uhaba wa miti ya mikoko.

Katika kutafuta ukweli wa kina, Nipashe ilikutana na Katibu Mkuu wa Taasisi Inayosimamia Mazingira ya Usafi wa Fukwe (BMU), Juma Abdallah, anayekiri kuwapo baadhi ya wananchi wanaokata miti hiyo bila ya kujua athari zilivyo.

"Kuna watu wanapenda kwenda katika fukwe za bahari na kukata mikoko iliyoota pembezoni humo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibinadamu, lakini athari yake ni kubwa kwa samaki.

"Kamba kochi na Prons, ni aina ya samaki wanaoishi kwa kutegemea mikoko. Hawa samaki ni ghali sana na wanatumika sana katika hoteli kubwa, maisha yao kwa kiasi kikubwa yanategemea mikoko, kwa hiyo ili kuzalisha samaki, wengi tunapaswa kuituza.



Mikoko iliyostawi ufukweni. **PICHA: MTANDAO.**

> **Kuna watu wanapenda kwenda katika fukwe za bahari na kukata mikoko iliyoota pembezoni humo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibinadamu, lakini athari yake ni kubwa kwa samaki.**

"Ina uwezo mkubwa wa kuzalisha oksijeni kwa wingi ambayo inawezesha samaki kuzaliana, kwa hiyo usafi wa fukwe ni muhimu na kuna mambo mengi sana yanayosababisha viumbe wa majini kupata shida ikiwamo mifuko ya plastiki," anaeleza Abdallah.

Mtaalamu huyo ana ufafanuzi wa kuhimiza jamii kuweka utaratibu wa kupanda miti ya mikoko na kusafisha kando ya bahari, ili kuepuka kujiweka katika hali ya kukosa samaki.

Mwenyekiti wa Vikundi Vilivyotengezwa na Wizara ya Uvuvi, kwa ajili ya kutunza na kusimamia rasilimali za bahari, Mohamedi Njuga, anakiri kuwapo shida hiyo ya kuharibiwa mikoko.

"Ukataji wa mikoko unaathiri vitu vingi. Kwanza, unaathiri samaki wenyewe kuna baadhi ya samaki wengine wanazaliwa kwenye sehemu za mikoko, na samaki wanaozaliwa sana ni kagogo, kama kule maeneo ya Tanga na maunga pia wanazaliwa sana,' anafafanua.

Njuga anatahadharisha hatari ya kukata mikoko, inasababisha wavuvi kwenda kuwatafuta samaki mbali, kwa sababu wanaenda sehemu nyingine ambako kuna mikoko, matokeo yake serikali inakosa manufaa yanayotokana na samaki kwa sababu samaki wengi wanatokana na mikoko.

## FAIDA ZA MIKOKO

Wataalamu wanaeleza kuwa mikoko ina faida kubwa sana, wakianza na namna inasaidia kupunguza kasi ya mawimbi makubwa ya bahari ambayo yanaweza kuleta uharibifu mkubwa katika pwani ya bahari, pia inatajwa kuweka mazingira bora kwa samaki kuzaliana, wakieleza kasi ya mawimbi makali ya bahari na maji kwa jumla.

Lingine, ambalo ni la kiafya na kimazingira, mikoko inanyonya hewa ya ukaa (carbon dioxide) kutoka angani na kuzalisha oksijeni kupitia kitendo cha mmea kiitwacho "photosynthesis".

Oksijeni inayozalishwa, kiafua inatumiwa na mwanadamu na viumbe hai wengine katika mfumo wa kupumua na kuchuja maji ya chumvi na kuondoa asilimia 90 ya chumvi inayopatikana katika maji ya bahari na kuingia kwenye mizizi yake.

Pia, mikoko husababisha mazalia mazuri ya wadudu ambao kwa kiasi kikubwa ndio chakula cha samaki, vilevile inasaidia kuzuia mmomonyoko wa ardhi kando ya bahari.

## JICHO LA UNESCO

Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limetoa wito huo katika siku ya kimataifa ya uhifadhi wa mfumo wa mikoko inayoadhimishwa kila mwaka, Julai 26.

Mikoko, na aina zingine za miti zinazoota ufukweni mwa bahari na kwenye mito inasaidia kuimarisha uhakika wa chakula, kuendeleza uvuvi na bidhaa zingine za msituni.

Pia inajukumu muhimu na la kipekee la kukusanya na kuhifadhi kiasi kikubwa cha gesi ya ukaa kutoka hewani na baharini, ambacho ni muhimu kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Takribani asilimia 67 ya mikoko imetoweka hivi leo na karibu mikoko yote ambayo hailindwi inaweza kutoweka katika miaka 100 ijayo. UNESCO inaitaka jumuiya ya kimataifa kubadili mwenendo huo wa uharibifu, kwa sababu ya jukumu muhimu la mikoko katika kuhakikisha dunia inakuwa na afya muafaka.

# Ukatili wa watoto Moro washitua Chuo kikuu, chabuni kituo cha vita

**INATOKA UK.18**

anawataka viongozi kutoa elimu ya kupinga masuala ya ukatili.

Anasema viongozi hao wa dini wamekuwa wakiwafikia watu wengi na haraka zaidi, kutokana kuaminiwa na kukubalika kwao kwenye jamii na endapo watafanya hivyo watasaidia kumaliza tatizo hilo.

" Tunawaomba viongozi wetu wa dini kutumia madhabahu yenu kutoa elimu ya masuala ya kupinga vitendo vya ukatili, kwani nyie mna nafasi ya kuwafikia watu wengi na haraka kutokana na mnavyoaminika kwenye jamii zetu, " anasema Lwena.

## KIONGOZI WA DINI

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Umoja wa Mitume na Manabii Tanzania, Jimmy Matamwe anasema vitendo vya ukatili, mauaji na uhalifu mwingine chanzo chake ni kukosekana maadili katika baadhi ya jamii.

Anawaomba viongozi wenzake wa dini kutumia nafasi zao kuhubiri na kufundisha matendo mema yanayompendeza Mungu, yatakayowezesha kupunguza ukatili wa kijinsia na uhalifu katika jamii.

## WAZIRI GWAJIMA

Waziri wa Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalumu,Dk. Dorothy Gwajima,akizindua kituo hicho cha Mkono kwa Mkono, ameahidi kushirikiana na Ofisi ya Rais ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kupambana na matukio ya ukatili kwa watoto katika mikoa ambayo hali hiyo inashamiri, ili kuhakikisha vitendo hivyo vinakoma katika maeneo hayo.

Dk Gwajima anaahidi kuanza na mkoa wa Morogoro kuungana na uongozi wa mkoa kupiga vita hivyo, kutokana na takwimu za ukatili kwa watoto kuwa juu.

"Nataka kukuhakikishia Mkuu wa Mkoa wa Morogoro,tutaanza na mkoa wako kuweka kambi hapa. Mimi pamoja na Waziri wa Tamisemi, tutapita kata zote za wilaya zenye matatizo ya ukatili wa aina zote na wahusika wote tutachukua hatua kali ili kukomesha kabisa tatizo hili la ukatili " anasema Dk Gwajima.

Pia, waziri anafafanua kuwa madawati ya Jeshi la Polisi ya Jinsia nchini, yamepokea na kushughulikia jumla ya mashauri 20,025 ya ukatili, ikilinganishwa na mashauri 18,270 yaliyoripotiwa mwaka 2019/20.

Anasema katika kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021 kuna waathirika 1,857 wa ukatili wa kijinsia walipata huduma; kati yao wavulana ni 412, wasichana 660 na wanawake wakiwa 785 .

AFYA

# Wanaafya, wanahabari Dar waingia ubia operesheni chanjo Uviko 19



Baadhi ya wanahabari kutoka vyombo vya habari, wakizungumza na wenzao wa afya. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE.**

**Na Yasmine Protace**

KIAFYA shughuli za chanjo zinamsaidia mtu kujikinga na kuwakinga wengine wasiambukizwe magonjwa. Katika kupambana na maradhi corona, nchini Tanzania nako jamii imetakiwa kwa hiari kujitokeza katika maeneo yaliyotengwa, ili waweze kupata chanjo.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Dar es Salaam Dk. Ezenael Ayo, anasema mkoa ulianzisha chanjo ya Covid 19 mnamo Agosti mwaka jana, katika mkutano uliowakutanisha wataalamu wa afya na Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC).

Kwa mujibu wa Dk. Ayo, ni mkutano ulio chini ya Mradi wa Kuboresha Habari, uliobainisha kwamba Sensa ya Watu ya Mwaka 2012, mkoa Dar es Salaam, umetathmini kuwapo watu zaidi ya milioni sita.

Anasema, Dar es Salaam walianza kwa kutoa chanjo kwa vituo vitatu, huku akifafanua 'mkoa ulianza kupanua wigo, sasa vituo vipo 318 vya kutoa huduma ya chanjo,"

Katika hilo, anataja kwamba awali mapokeo ya chanjo kwa wananchi, mwamko wao ulikuwa mdogo, ila kwa sasa huduma za mkoba zimeweza kutumika kwa kuwafuata wananchi, ambapo malengo yao ni kufikia asilimia 70.

Anaongeza kuwa, mkoa wa Dar es Salaam unakadiriwa kuwa na watu zaidi ya milioni sita sasa na ambao malengo yao ni kuchanja watu zaidi ya milioni tatu, huku hadi sasa wameshawachanja wananchi wa mkoa Dar es Salaam, kwa asilimia 85.

> **Muwaelimishe jamii na wanaume wasiogope kuchanja na waachane na maneno ya kizushi kwamba ukichanja 'nguvu za kiume zinapotea' na kuwa zombi.**



Ofisa Afya wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Enezael Ayo, akizungumza jambo na waandishi wa habari.

Dk. Ayo anasema katika kuchanja, walianza na makundi maalumu ikianzia na afya, kwa kuwa ndio watoa huduma. Anaongeza kuwa kundi la pili lilikuwa la wazee na wakafuatiwa na vijana na mpaka sasa hatua hiyo ya kuchanja inaendelea, akiwapo wadau waliojitolea kusaidia kuchanja.

Anasema mkoa wa Dar es Salaam, mapema wakawawashauri watu kujitokeza kuchanja, pia wenyeviti wa serikali za mitaa walisaidia kuhamasisha wananchi katika suala hilo la kuchanja na ufanikishaji wake.

Kuhusu maendeleo yaliyopo, anafafanua kwamba chanjo bado inaendelea mkoani Dar es Salaam, ingawa anakiri kuwapo baadhi ya wananchi ambao wamekuwa wakiipotosha hatua hiyo.

Pia, anataja changamoto nyingine inagusa uhaba wa rasilimali watu na fedha kutolewa kidogo, hata akitaja 'zinasaidia' chanjo zote zitolewe kwa usalama, akieleza: "kila eneo tunasisitiza watu waende kuchanja.".

Vilevile, Ofisa Afya wa Mkoa wa Dar es Salaam huyo anaongeza kuwa jamii nayo inapaswa kuchukua hatua stahiki ya kunawa mikono, kwani suala ni la wajibu na kufanywa endelevu.

Mtaalam wa Afya, Dk. Christina Mdingi, anaieleza chanjo ya UVIKO-19 ni salama dhidi ya virusi hivyo na anavisihi vyombo vya habari kusimama katika nafasi yao ya kuelimisha na kutoa taarifa sahihi namna ya uelimishaji kwa umma wa Watanzania, ili waweze kupata chanjo.

Daktari Christina, anaelekeza ujumbe wake kwa jamii, kwamba ni suala la kufanyika kwa haraka na linapaswa kupitia njia ya vyombo vya habari, ili wananchi wajitenge dhidi ya uzushi anaoutafsiri kuwa sio sahihi kupitia chanjo hiyo.

"Muwaelimishe jamii na wanaume wasiogope kuchanja na waachane na maneno ya kizushi kwamba ukichanja 'nguvu za kiume zinapotea' na kuwa zombi," anasema.

**SAUTI YA WANAHABARI**

Samson Kamalamo, Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC,) anaishukuru asasi 'Internews' kwa kuratibu mafunzo hayo yaliyogusa sekta ya afya na anawataka waandishi hao wa habari kuzingatia taaluma yao na kuandika habari zenye weledi.

Anaongeza kuwa, mafunzo hayo yamewajengea uwezo na maarifa wanahabari ambayo watayatumia kuielimisha jamii katika masuala yanayohusu ugonjwa corona.





## Tani 30 za mbolea kutoka Kenya zaingia nchini

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

ZAIDI ya tani 30 za mbolea ya kupandia na kukuzia zimeingizwa kutoka nchini Kenya kupitia Kampuni ya Mbolea ya SBL itakayotolewa bure kwa baadhi ya wakulima Mkoa wa Mbeya katika msimu huu wa kilimo.

SBL imeingia ubia na Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara mikoa ya Nyanda za Juu Kusini sambamba na uhakika wa masoko nchini Kenya.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya mbolea hiyo juzi, Kaimu Meneja wa TFC, Kanjela Mroba, alisema tayari tani 30 zimeingia nchini huku matarajio ni kuagiza tani 3,000 kulingana na mahitaji ya wakulima kwa sasa.

"Kwa sasa tumepokea tani 30 za majaribio ambayo itatolewa bure kwa baadhi ya wakulima na tayari tumefanya utafiti ni mbolea inayofanya vizuri katika uzalishaji hususan kwa zao la mahindi," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kampuni ya SBL, Joe Kariuki, alisema ujio wa mbolea ni fursa kwa wakulima kwa kuwa ina uwezo wa kuzalisha mazao na kurejesha ubora wa udongo ulioathirika kwa matumizi ya mbolea isiyo sahihi.

Alisema pia watatoa elimu kwa wakulima huku TFC ikiwa inasimamia usambazaji na masoko kwa nchi ya Kenya watatumia mfumo wa kubadilishana mbolea na mazao kwa asilimia 100.

"Mbolea hii inafanya vizuri sana katika uzalishaji na tayari tuna vituo 150 nchini ambavyo vinasambaza mbolea ambayo itauzwa kwa gharama nafuu ili mkulima aweze kumudu," alisema Mroba.

Mkulima wa Kijiji cha Iwindi, wilayani Mbeya, Fredy Aloyce, alisema kuwa ujio wa kampuni za mbolea utasaidia wakulima kurejesha matumaini na kuzalisha mazao ya kimkakati.

"Tunaomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo iongeza ushindani wa kampuni za pembejeo za kilimo pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei kwa mawakala ambao wamekuwa mwiba kwa wakulima na kutukatisha tamaa katika uzalishaji.

# Wamiliki viwanda mafuta ya alizeti watoa kilio cha umeme

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAMILIKI wa viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti katika soko la Sido jijini hapo wameiomba serikali kutafuta ufumbuzi wa tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara unaoathiri kazi zao na kuwasababishia hasara.

Wakizungumza na gazeti hili, baadhi ya wamiliki hao walisema katika siku za hivi karibuni imeibuka tabia ya umeme kukatika mara kwa mara bila taarifa na kukwamisha shughuli zao.

Mmoja wa wamiliki wa viwanda hivyo, Jumanne Mwakasole, alisema tangu umeme uanze kukatika bila mpangilio amepata hasara kubwa ikiwa ni pamoja na kusimamisha uzalishaji kutokana na kukosekana kwa nishati hiyo.

"Kazi yetu ya kukamua mafuta kwa sasa sio ya uhakika, unaweza kuandaa malighafi na vibarua, lakini umeme ukakatika bila taarifa, kwa vile unakuwa umeshaajiri vibarua inabidi tu uwalipe bila kufanya kazi iliyokusudiwa, jambo ambalo kwetu limetusababishia hasara kubwa," alisema Mwakasole.

Alisema endapo umeme utaendelea kukatika, kuna uwezekano mkubwa wa Jiji la Mbeya na maeneo ya jirani kukumbwa na uhaba wa mafuta ya kupikia.

Kwa upande wake Julius Kapunga alisema wanachohitaji ni kupewa taarifa kabla ya kukata umeme ili wajiandae kukabiliana na hali hiyo.

"Tunaiomba serikali iingilie kati ili kama kuna umuhimu wa kukata umeme, basi taarifa itolewe ili tufanye maandalizi ya kukabiliana na ukosefu wa umeme, wanapokata bila taarifa wanatusababishia hasara ambayo tungeweza kuiepuka kama wangetoa taarifa," alisema Kapunga.

Naye Gwakisa Boniface, alisema anasikitishwa na tabia ya kuanza kukatika kwa nishati hiyo, wakati hali hiyo ilishakomeshwa kwenye uongozi wa awamu ya tano.

"Kwa kweli tulishasahau habari ya umeme kukatika, kwa sababu Rais wa awamu ya tano alijitahidi kuhakikisha umeme haukatiki, lakini tunasikitika TANESCO wameturudisha nyuma kwa kuanza kukata ovyo umeme tena bila kutoa taarifa, hivyo tunaomba Rais Samia aingilie kati kukomesha tabia hii," alisema Gwakisa.

Katika siku za hivi karibuni, TANESCO wamekuwa wakikata umeme katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya wakidai kuwa kuna upungufu wa maji kwenye vyanzo vya kuzalisha umeme unaotokana na hali ya ukame iliyokithiri nchini.



Mdau wa Elimu nchini, Ndele Mwaselela, akivalishwa skafu na vijana wa skauti wa Shule ya Sekondari ya Wazazi Mbalizi, mkoani Mbeya katika mahafali ya kidato cha nne shuleni hapo, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waomba kujengewe barabara waliyoilima kwa mikono

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

WANANCHI wa Kata ya Ikuti, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kujenga barabara yao waliyoilima kwa mkono miaka mingi iliyopita ili vyombo vya usafiri ikiwamo magari na bodaboda viweze kupita.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mkuu wa Wilaya Rungwe, Dk. Vicent Anney, wananchi hao walisema kuwa barabara pekee inayoingia kwenye vijiji hivyo waliilima wenyewe kwa mikono miaka mingi iliyopita na haijawahi kukwatuliwa na greda.

Deus Mwaijumba alisema barabara hiyo ilivyolimwa na wazee wao miaka mingi iliyopita, magari hayawezi kupita na kuvifikia vijiji vyao nakuomba msaada wa serikali iiboreshe ili iweze kupitika.

"Barabara hii ambayo ndiyo inaingia kwenye vijiji vyetu vya Kyobo Juu haijawahi kutumiwa na magari tangu nchi ipate uhuru, hii ni kwa sababu ililimwa kienyeji na wazee wetu kwa kutumia jembe la mkono miaka mingi iliyopita, tunaomba sasa serikali itusaidie kuilima kwa greda ili magari yapite na kufika kwenye vijiji vyetu," alisema Mwaijumba.

Alisema katika vijiji hivyo wanazalisha mazao mengi ya biashara na chakula kama kamae ndizi, iliki, kahawa, magimbi na mihogo, lakini hawawezi kuyasafirisha kwa wingi kwenda kuyauza.

"Tunayo mazao yetu tunayolima kwa wingi, ingawa tunajua yana soko kubwa nje ya vijiji vyetu, lakini tunashindwa kuyasafirisha kwa wingi na hata wanunuzi wanashindwa kuja kuyanunua kwa sababu hakuna barabara, baadhi yetu tunalazimika kuyabeba kichwani kwenda kuyauza ili tupate fedha za kujikimu, tunaomba tusaidiwe barabara kuondokana na kero hizi," alisema Mwaijumba.

Kwa upande wake, Lucia James alisema kuwa ukosefu wa barabara pia una athari kubwa kwa wanawake hasa wajawazito wanapohitaji kujifungua na wanapotaka kwenda kwenye vituo vya afya.

Alisema usafiri pekee unaowasaidia wajawazito kwenda kujifungua kwenye vituo vya afya ni pikipiki, usafiri aliodai kuwa sio rafiki kwa baadhi ya wajawazito hasa ambao wanakuwa na matatizo ya uzazi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, aliungana na wananchi hao kuomba msaada wa ujenzi wa barabara hiyo, akisema kuwa Serikali Kuu inapaswa kutenga bajeti ya kuwasaidia wananchi hao katika mwaka ujao wa fedha.

Mwakilishi wa Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Senyange, Kayoka alisema jukumu lao ni kufungua barabara kwenye maeneo yote ili wananchi wazitumie kwa shughuli za maendeleo.

Aliahidi katika mwaka ujao wa fedha barabara hiyo itakuwa ya kwanza kuingizwa kwenye bajeti ya TARURA ili iweze kujengwa na kumaliza kero ya wananchi hao.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Anney alisema atasimamia kikamilifu kuhakikisha barabara hiyo inapitika kwa gari kwa manufaa na maendeleo ya wananchi wa vijiji hivyo.

Alisema kuwa barabara hiyo ikifunguka anaamini wananchi hao watapata maendeleo ya haraka kwa vile ni wazalishaji wazuri wa mazao ambayo yanapendwa na yenye soko la uhakika ndani na nje ya Wilaya ya Rungwe.





# TBA yashauriwa ujenzi wa maghorofa nyumba za makazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imeuelekeza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kujenga maghorofa kwenye miradi yake ya nyumba za makazi inayotekeleza katika maeneo mbalimbali nchini.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Selemani Kakoso, alitoa ushauri huo juzi baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa TBA katika robo ya mwaka 2022/23.

Alisema TBA, imekuwa ikitekeleza miradi yake kwa ufanisi na kushauri kuanza kuangalia ujenzi wa maghorofa badala ya nyumba za chini ili kuwa na matumizi mazuri ya ardhi.

"Tumeipokea taarifa ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na tunawapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya katika kutekeleza kazi ya ujenzi wa nyumba, sasa tuwashauri badala ya kuendelea kujenga nyumba za chini, jengeni maghorofa kama ilivyofanya pale Magomeni Kota," alisema.

Aidha, Kakoso aliitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuwatafutia TBA watumishi wa kutosha kwa kuomba kibali cha kuajiri hasa kutokana na miradi inayotekelezwa na taasisi hiyo kuhitaji usimamizi wa karibu.

"Nakuombeni nendeni mkalisimamie, tafuteni kibali ili muajiri watu watakojua kufanya kazi, kwasababu kazi za TBA zinahitaji sana usimamizi na mkifanya hivyo kutakuwa na mapinduzi makubwa sana kwenye sekta ya unjenzi," alisisitiza Kakoso.

Alisema, kwa kuwa wizara inapelekewa fedha nyingi ni vyema kuangalia namna ya kuitumia TBA ambayo ina fursa ya uwekezaji ili kuwekeza na kusisitiza kuwa kwa kufanya hivyo, fedha nyingi zitarudi serikalini kupitia uwekezaji huo.

"Naamini wizara mnapata fedha nyingi, zingine zipitisheni TBA kwasababu wana nafasi ya uwekezaji, kwa mipango na uwezo wa TBA wana nafasi kubwa ya kufanya ujenzi, mfano mkiwawezesha hata pale Magomeni Kota wanaweza kujenga mall (maduka makubwa) na kuleta mabadiliko makubwa sana kwenye Jiji la Dar es Salaam na kuwa na uwekezaji mkubwa utakaoleta faida kwa serikali," alisema.

Alisema wakati wa maandalizi ya bajeti ya mwaka 2023/24, wizara ihakikishe inaitengea TBA bajeti ya kutosha ili kutekeleza miradi mingi ambayo italeta tija kwa serikali.

"Mkianza maandalizi ya kuandaa bajeti ya wizara hakikisheni TBA inatengewa bajeti ya kutosha, maana TBA wenyewe wamesema wakipewa Sh. bilioni 50 ambazo kwa serikali ni fedha kidogo na zitafanya ujenzi mkubwa ambao watu wataweza kukodi na kuishi na pia fedha hizo zitarudi ndani ya serikali," alisema.

Mtendaji Mkuu wa TBA, Daud Kondoro, aliahidi kwenda kutekeleza maagizo ya kamati na kusisitiza kuwa wakala umejipanga kutekeleza miradi yake kwa kasi, ubora na haraka.

"Wakala tumejipanga kuhakikisha miradi yetu yote tunaitekeleza kwa kasi, haraka ikiwa na ubora," alisema.

Hata hivyo, alisema katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/23, wizara imeipatia TBA zaidi ya Shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi yake.

"Tunaishukuru wizara katika robo ya mwaka tumepewa shilingi bilioni nane kwa ajili ya kutekeleza miradi yetu na hii ni sawa na moja ya tatu ya fedha tulizokuwa tumetengewa kwa ajili ya utekelezaji miradi," alisema.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo (katikati), akipanda mmoja kati ya miti 1,000 iliyotolewa na Benki ya Standard Chartered katika Shule ya Msingi Mtoni, wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani juzi. Kushoto ni Ofisa Tawala Bagamoyo, Casilda Mgeni na (kulia) ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Herman Kasekende. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wasichana 3,333 waliokwama masomo warudi shuleni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha mwaka 2021/2022 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), imehamasisha kurejea shuleni wasichana 3,333 walioshindwa kuendelea na elimu ya sekondari kwa sababu mbalimbali.

Baadhi ya sababu hizo ni pamoja na mazingira magumu, kupata ujauzito au ndoa za utotoni kwa wenye umri kati ya miaka 13 hadi 21 ikiwa ni sawa na asilimia 111 ya lengo lililowekwa kupitia vituo 131 vinavyo hudumiwa na walimu 803.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Michael Ng'umbi, alibainisha hayo juzi alipokuwa akijibu maswali ya waandishi wa habari baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za elimu ya watu wazima nchini.

Alisema taasisi hiyo imepanga kuanzisha programu maalum ya kutoa kisomo cha watu wazima, mafunzo ya ufundi wa awali na ujasiriamali kwa watu wa jamii ya kabila la Wahadzabe kupitia mradi wa IPOSA.

Alisema kupitia mradi wa IPOSA unaojihusha na kutoa kisomo kwa watu wazima, mafunzo ya ufundi wa awali na ujasiriamali kwa watu wote wanaotaka kupata ujuzi wameandaa programu maalum kwa Mkoa wa Manyara.

"Wahadzabe ni Watanzania wenzetu na wao ni kama jamii nyingine nchini hivyo hizi huduma zinazotolewa na Taasisi yetu na wao wanayo haki kuzipata kupitia mradi wa IPOSA tumeandaa programu maalum kwa Mkoa wa Manyara ambako wapo watu wa kabila hili na maeneo mengine," alisema.

Akizungumzia kazi zilizofanywa na taasisi hiyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, alisema wameandaa na kuendesha mafunzo katika kampasi zake tatu Dar es Salaam, Morogoro na Mwanza.

Programu tatu za mafunzo zilitolewa kwa njia ya ujifunzaji wa kawaida, huria na masafa.

"Programu hizo ni Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi, Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii, na Elimu Masafa kwa ngazi za astashahada, stashahada na shahada," alisema.

Kadhalika, alisema jumla ya wanafunzi 8,093 kati yao wanawake 4,644 walipata mafunzo hayo.

Pia alisema taasisi hiyo illifanya usajili wa wanafunzi wapya 3,426 walisajiliwa katika programu tatu za TEWW kwa mwaka wa masomo 2021/22.

Aidha, jumla ya walimu na wasimamizi wa elimu ya watu wazima 2,355, walihitimu masomo yao katika mwaka 2021/22.

Vilevile, alisema katika kipindi hicho taasisi hiyo iliandaa mtaala wa mafunzo ya walimu wa elimu ya watu wazima katika maeneo ya ufundi na teknolojia.

Mafunzo hayo yanatarajiwa kuanza kutolewa kwa ngazi ya astashahada na stashahada katika mwaka wa masomo 2023/24 baada ya kuidhinishwa na NACTVET.

# Serikali kutoa kipaumbele mafunzo kwa wafanyakazi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kutoa kipaumbele cha mafunzo kwa wafanyakazi nchini ili kuwajengea uwezo kiutendaji utakaowasaidia katika majukumu yao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alibainisha hayo jana wakati akielezea dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan tangu ameingia madarakani.

"Rais Samia tangu aingie madarakani amedhamiria kuendelea kutoa kipaumbele cha kuwapatia mafunzo viongozi ili kuwajengea uwezo kiutendaji, utakaowezesha kuwasaidia kutekeleza vyema majukumu yao ya kuwatumikia wananchi na kuwaletea maendeleo," alisema Mhagama.

Waziri Mhagama alielezea dhamira hiyo ya Rais Samia wakati akifunga mafunzo ya Sanaa ya Uongozi kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI), yaliyotolewa na Taasisi ya Uongozi jijini hapo.

Mhagama alisema baada ya Rais Samia kuapa na kuanza kulitumikia taifa, moja ya eneo ambalo alielekeza lipewe kipaumbele ni kutoa mafunzo kwa viongozi akitambua kuwa ndiyo njia pekee ya kuwawezesha viongozi kuwa na ufanisi kiutendaji.

Alisema, Ofisi ya Rais-Utumishi, imekuwa ikitekeleza kwa vitendo agizo hilo la Rais kwa kuwapatia mafunzo wajumbe wa kamati ya USEMI.

Alisema, Rais Samia ana maono na ndiyo maana anatambua kuwa waliopewa dhamana ya kuwa viongozi wanahitaji kujengewa uwezo ili kupata ujuzi utakaoendana na mazingira yaliyoko ikiwa ni pamoja na kwenda sambamba na maendeleo ya teknolojia.

Wajumbe wa Kamati ya USEMI, Festo Sanga, alisema toka awe mbunge hajawahi kupata mafunzo mazuri ya uongozi kama ambayo Taasisi ya Uongozi imewapatia na yamemjengea uelewa kwenye eneo la akili hisia.

Sanga ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Makete alisema, mafunzo hayo yaliyomjenga akihisi yatamwezesha kuzungumza vizuri na wananchi na kupokea yale ambayo wananchi anaowaongoza wanahitaji kutekelezewa.

"Mafunzo haya kama mbunge na mjumbe wa kamati ya USEMI yamekuwa na manufaa makubwa kwani yamenipatia elimu ya namna ya kuisaidia serikali katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema Sanga.

Pia mafunzo hayo yatamsaidia kusimamia matumizi ya fedha za umma ambazo serikali inazitoa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.





# Polisi yakamata watu watatu wakiwa na dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Kusini Unguja linawashikilia watu watatu kwa kukutwa na kete 330 za dawa za kulevya za aina mbalimbali.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Tunguu visiwani humo, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Hamisi Lisse Mwampelwa, alisema watu hao walikamatwa Oktoba 23, mwaka huu, majira ya saa 4:30 usiku.

Aliwataja kuwa ni Msomi Ali Haji (26) mkaazi wa Kibele, Salum Ame Hassan (28) mkaazi wa Tunguu na Msafiri Juma (34) mkaazi wa Kidimni.

Mwampelwa alisema vijana hao walikamatwa wakati wa operesheni maalum ya kuwasaka watumiaji, wasambazaji, wauzaji wa dawa za kulevya na wahalifu wengine mkoani humo.

Akifafanua tukio hilo, ACP Mwampelwa mtuhumiwa Haji alikamatwa na kete 238 zinazodhaniwa kuwa ni dawa za kulevya aina ya heroin zilizohifadhiwa katika mafurushi tofauti.

“Kijana huyo alikamatwa akiwa anasafirisha dawa hizo kwa usafiri wa pikipiki yenye namba za usajili Z. 264 RZ akitokea mjini kuelekea barabra ya Makunduchi, na alipofika Tunguu alikamatwa baada ya kutiliwa shaka na askari waliokuwa doria kituo cha Tunguu,” alisema.

Alimtaja mtuhumiwa mwengine Salum Ame Hassan, katika maeneo hayo ya Tunguu majira ya saa tano usiku alikamatwa akiwa na kete 17 za heroni.

Kaimu Kamanda huyo alimtaja mtuhumiwa wa tatu kuwa ni Msafiri Juma, aliyekamatwa na kete 75 dawa za kulevya mithili ya sampuli ya vijiwe huko Kidimni Oktoba 22, mwaka huu, majira ya 12:00 jioni.

Aidha, alisema watuhumiwa wote wanashikiliwa na upelelezi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Kamanda huyo aliwataka wananchi hasa vijana kuachana kujihusisha na biashara hiyo haramu na badala yake kutafuta kazi za halali zitakazowasaidia kupata kipato halali.



Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid (kulia), akikagua bidhaa za wajasiriamali nje ya ukumbi wa hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## DC ataka wazee kurejesha malezi ya pamoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya Magharibi ‘A’, Suzan Peter Kunambi, amewataka wazee kurudisha utamaduni wa malezi ya pamoja ili kuwajengea maisha bora watoto wao.

Akizungumza na wazee wa shehia za wilaya hiyo ofisini kwake Mwera Zanzibar, alisema kuna baadhi ya wanajamii hawaupi kipaumbele mfumo huo hali inayosababisha kuibuka kwa vitendo viovu vikiwamo vya kutupa watoto wachanga, udhalilishaji na biashara ya dawa za kulevya.

Alisema endapo wazee wakikaa pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya malezi kwa watoto kunaweza kupatikana vijana wenye mwenendo mzuri wa maisha na kuwa viongozi bora.

“Inasikitisha kuona baadhi ya wazazi na walezi huwatetea watoto wao wanapofanya vitendo vya kihalifu na kuunga mkono yale wanayofanya jambo ambalo limekuwa likiikosesha jamii watoto wenye maadili mazuri,” alisema Suzan.

Hivyo aliwataka kushikamana na kuhakikisha mtoto anapofanya kosa na kupelekwa katika vyombo vya sheria, washirikiane na mamlaka zinazohusika kumrekebisha ili awe na vitendo vyema katika jamii.

Wakizungumza wakati wa kikao hicho, wazee hao walimpongeza mkuu huyo wa wilaya kwa kukutana nao na kuvitaka vyombo vya ulinzi na usalama kusimamia sheria kwa vijana wanaofikishwa mikononi mwao.

Mmoja wa wazee hao, Juma Haji, alisema hakuna mzazi anayetaka mtoto wake aharibike ila hutokana na mazingira mbalimbali yakiwamo ya umaskini yanapelekea baadhi ya vijana kufuata mkumbo.

# Maofisa ununuzi waagizwa kufuatilia utendaji wa mfumo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa mali za Umma Zanzibar, Othman Juma Othman, amewaagiza maofisa ununuzi na mapato kufuatilia namna mfumo wa kielektroniki wa matumizi kwa kuwa ni sehemu ya mabadiliko ya kidunia.

Akifungua mkutano wa kutathmini utendaji wa mfumo wa kielektroniki wa matumizi jana Mzizima mkoani Mjini Magharibi, Unguja, alisema maboresho hayo yatasaidia malipo kufanyika kwa haraka na wakati sahihi.

Alisema hatua hiyo itawarahisishia kufanya taratibu za malipo kwa wakati hasa kwenye zabuni, ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya kidunia pamoja na kusaidia udhibiti wa upotevu wa mali ya umma.

Othman alisema bado baadhi ya watendaji hawajabadilisha mitazamo yao kutoka utaratibu waliouzoea wa kutumia karatasi, na kwamba mfumo wa kielektroniki utaleta mabadiliko makubwa ikiwamo ya kiuchumi.

Alisema mamlaka itahakikisha inawaongezea uwezo watendaji wake, ili kuona matumizi ya mfumo huo yanaleta manufaa kwa jamii na nchi kwa ujumla kama ilivyokusudiwa.


Kwa upande wao Maofisa Manunuzi wa Taasisi za Serikali, waliishauri kuunganisha Mfumo wa Malipo (IFMS), uwe mmoja kwa kuwa lengo ni kudhibiti mapato ya serikali.

Mmoja wa maofisa hao kutoka Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC), Hussein Msanif Haji, alisema lengo la kuwepo kwa mifumo hiyo kwa taasisi za serikali ni kuondokana na urasimu katika utoaji wa huduma na kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Aidha, waliiomba serikali kutengeneza utaratibu maalumu utakaoruhusu kampuni za wasambazaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi kusajiliwa kiurahisi, kwa kuwa mfumo wa sasa unatoa fursa inayoongeza mapato.

Pia alisema kuna baadhi ya wasambazaji bidhaa waliopo nje ya nchi kufanya kazi bila ya kusajiliwa katika mfumo huo jambo linalowapa ugumu wanapotaka kuagiza bidhaa nje ya nchi.

Barke Abdallah Juma, kutoka Baraza la Jiji la Zanzibar, alisema mfumo huo ni mzuri, na kwamba ukitekelezwa itakuwa rahisi kwa wahasibu ukishaunganishwa na mfumo wa manunuzi.





# Ujenzi barabara lami Tabora-Kigoma wafikia asilimia 66

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

MRADI wa ujenzi wa barabara ya lami inayounganisha mikoa ya Tabora na Kigoma kipande cha Kazilambwa-Chagu chenye yenye urefu wa km 36 umefikia asilimia 66 huku utekelezaji wake unaendelea kwa kasi.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Raphael Mlimaji, alisema mradi huo unaotekelezwa na kampuni ya STECOL kutoka China kwa ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Kimataifa (OPEC) na serikali unaendelea vizuri na unaelekea kukamilika.

Alisema utekelezaji mradi huo unatarajiwa kukamilika mapema mwakani na kwamba hadi kukamilika kwake utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 32.

Aidha, barabara hiyo inatarajiwa kuongeza mzunguko wa fedha kutokana na ongezeko la wafanyabiashara kutoka maeneo mbalimbali.

Mlimaji alieleza kuwa jumla ya km 26 za mradi huo zipo upande wa Tabora eneo la Kaliua na km 10 upande wa Kigoma huku akatoa wito kwa jamii inayoishi kando kando ya eneo la mradi huo kutunza miundombinu itakayowekwa ikiwamo alama za barabarani na taa.

Mhandisi Mlimaji alisisitiza kuwa mradi huo ni muhimu kwa kuwa utamaliza kero ya usafiri na usafirishaji wa mazao na bidhaa kwa muda mrefu kwa wakazi wa mikoa hiyo.

Katika hatua nyingine, mhandisi alieleza kuwa kwa sasa anaendelea na mazungumzo na mfadhili, ili kuangalia uwezekano wa kuongeza km 11.4 za barabara ya mchepuko kipande cha Ugansa-Usinge km 7.4 na kipande cha barabara ya zamani ya Chagu-Ugansa km 4.

"Kama tukiafikiana vizuri kiasi cha Sh. bilioni 14 ambazo ni salio la gharama nzima ya mradi zitatumika kujenga vipande hivyo viwili kwa kiwango cha lami, ili kuwezesha wakazi wa maeneo hayo kunufaika na mradi huo.

Kwa mujibu wa mhandisi huyo, serikali inaendelea na mchakato wa ujenzi wa km 172 za barabara ya lami kutoka Ipole, Tabora hadi Rungwa, itakayounganisha mikoa ya Tabora na Mbeya.

Jumanne Husseni, mkazi wa Kazilambwa aliieleza Nipashe kuwa maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo yanatia hamasa, ikiwa barabara hiyo inatarajiwa kuwa mkombozi katika shughuli za kiuchumi.

"Ubovu wa barabara hii umekuwa tatizo la muda mrefu katika shughuli zetu za usafirishaji, lakini muda sio mrefu tutakuwa na uhakika wa safari zetu za kibiashara pamoja na usafirishaji wa mizigo kwenda maeneo mbalimbali ya kigoma," alisema.



Diwani wa Kata ya Bupamwa, Stephania Cheo (kulia kwenye msingi), akishiriki na wananchi katika uchimbaji wa msingi wa ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Sekondari Bupamwa, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza utakaogharibu Sh. milioni 80 iliyotolewa na serikali. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Serikali yajipanga kukamilisha miradi viporo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MANISPAA ya Shinyanga inatarajia kukamilisha miradi yote ya viporo ya zahanati kupitia fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo kutoka kwenye mapato ya ndani kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma.

Akizungumza juzi, wakati wa ziara ya Kamati ya Uhamasishaji Ukusanyaji Mapato ya Ndani, Mganga Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga, Dk. Elisha Robert, alisema kupitia fedha za mapato hayo wameshatenga fedha Sh. milioni 60 za kumalizia ujenzi wa miradi kiporo ya Zahanati katika Kijiji cha Mwamagunguli na Sh. milioni 30 Zahanati ya Bugweto.

"Zahanati hizi zilianzishwa kwa nguvu za wananchi mpaka hapa zilipofikia usawa wa lenta, na katika bajeti yetu ya manispaa ya Shinyanga kupitia fedha za mapato ya ndani tayari tumezitengea fedha, ili kuzikamilisha na kuanza kutoa matibabu,"alisema Dk. Elisha.

Alieleza kuwa licha ya Zahanati ya Bungweto kutengewa Sh. milioni 30 kupitia fedha za mapato ya ndani, vilevile serikali kuu imetenga Sh. milioni 50 zitakazoongeza nguvu ya kuimarisha utoaji huduma.

Elisha aliongeza kuwa kukamilika kwa zahanati hizo zilizoko pembezoni mwa mji wa Shinyanga, kutasaidia kwa kiasi kikubwa kutoa huduma za matibabu kwa wananchi hasa wajawazito na kupunguza vifo vya uzazi.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, alisema manispaa hiyo katika mwaka wa fedha 2021/2022 imekusanya Sh. bilioni 5.06 sawa na asilimia 125, huku ikiibuka kinara wa ukusanyaji mapato nchi nzima hivyo kujihakikishia kuwa na uwezo wa kukamilisha miradi hiyo.

Kwa upande wake, Mkazi wa Kijiji cha Mwamagunguli, Naomi Maige, aliipongeza serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa zahanati ambazo walianza kujenga kwa nguvu zao, ili wapate huduma za matibabu karibu na kuokoa maisha yao.

# Wananchi washauriwa kuweka akiba ya chakula

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Halmashauri ya Ushetu wameshauriwa kuweka akiba ya chakula, ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wake kutokana na mvua za masika kuchelewa kunyesha ili wanusuru familia zao kipindi kigumu.

Diwani wa Nyamilangano Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, Robert Mihayo, alibainisha hayo jana, akizungumza na gazeti hili na kusema kuwa kwa kushirikiana na kamati ya maendeleo ya kata wameanza kutoa elimu ya utunzaji wa chakula, ili kuepusha kuzuka kwa baa la njaa.

Alisema wakulima mkoani humo wamezoea kuanzia Septemba kuendelea kuwa ni miezi ambayo mvua zinakuwa tayari zimeanza kunyesha, lakini kipindi hiki kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi bado hazijanyesha hali ambayo inatia wasiwasi kwa familia ambazo hazina akiba ya chakula.

Mihayo alisema mwaka jana mvua pia zilikuwa chache na wakulima walilima mazao na kupata chakula kidogo ukilinganisha na vipindi vilivyopita na kwamba wanapaswa kutunza kwa umakini vyakula vilivyoko kwa kuwa hali inaonekana sio nzuri.

Alidai kuwa tayari wameanza kutembea katika vijiji mbalimbali vya kata hiyo kama Mitonga, Hundi, Nyamilangano na Ididi kutoa elimu ya kutunza chakula na kuacha kuuza kiholela, ili kuepukana na upungufu wa chakula kwa msimu ujao ndani ya familia.

Hata hivyo, aliwasisitiza wananchi wa kata hiyo kuhakikisha wanaandaa mashamba yao mapema katika msimu huu wa kulimo kwani mvua za kwanza ndio zinazotumika katika kupanda mazao hasa ya chakula na biashara na kuweka mbolea ili kupata mavuno mengi.

Naye mkazi wa kata hiyo, John Mabula, licha ya kuwa na mvua chache msimu uliopita bado pembejeo zilikuwa na bei juu hali iliyofanya wakulima wengi kushindwa kumudu gharama na kulima bila mbolea.

Alisema sasa mbolea zimeshuka bei na wameshapatia elimu ya namna kufuatilia raslimali za umma na chama cha watu wasiona na wahatakikisha wanafuatilia, ili kupata pembejeo nyingi za kuzielekeza katika kilimo chenye tija, nakusihi maofisa ugani kuwafikia na kuwapatia elimu ya kulima kisasa.

Naye Mwasiti Hamisi alisema wanunuzi kutoka nchi za jirani wamekuwa wakiwafuata katika makazi yao na kuwashawisha kuuza chakula na kwamba kwa tamaa zao wanalazimika kuuza, kupata fedha na kuzitumia kwa kipindi kifupi na familia kubaki zinateseka kwa kukosa chakula.

HABARI KITAIFA

# Dola 600,000 zatengwa uhifadhi wa Mto Ruvu

**Na Joseph Mwendapole**

MFUKO wa Uhifadhi Wanyamapori na Mazingira Duniani (WWF) umetenga dola za Marekani 600,000 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uhifadhi wa Mto Ruvu, ikiwa ni jitihada za kuhakikisha unakuwa na maji wakati wote.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkazi wa WWF, Dk. Amani Ngusaro, wakati wa mkutano wa kujadili usalama wa maji ulioandaliwa kwa mfuko huo kwa kushirikiana na Kiwanda cha Bia (TBL) na Shirika la Kimataifa la AB InBev.

Kwa pamoja mashirika hayo yanaendesha mradi wa usalama wa maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuweka miundombinu ya kuboresha ubora wa maji, wingi wa maji na kulinda vyanzo vya maji hususan kwenye mito mbalimbali.

Dk. Amani alisema wameamua fedha zote hizo zielekezwe kwenye uhifadhi wa mto Ruvu kwa kuwa unakabiliwa na vikwazo vingi ambavyo huenda vikasababisha kukauka kwa vyanzo vya maji na kuleta shida kubwa kwa wananchi.

"Kila mtu anajua umuhimu wa maji kwenye maisha ya binadamu na juzi tu mlisikia Mto Ruvu ulipungua maji kukawa na taharuki, sasa lazima tuwekeze nguvu kubwa kuulinda ili uendelee kuwa na maji kwa sababu bila maji hakuna kilimo, viwanda wala ufugaji," alisema.

Andre Fourie kutoka Shirika la AB InBev, alisema Tanzania imebahatika kuwa na maji mengi kutokana na idadi kubwa ya mito, maziwa na ardhi oevu lakini inashangaza kuona kuna watu ambao hawana uhakika wa majisafi na salama kwa matumizi yao ya kila siku.

Alisema umefika wakati mwafaka kwa wadau wote duniani kuweka mikakati itakayofanikisha upatikanaji wa maji kwenye maeneo mengi kwa kuweka miundombinu itakayolinda vyanzo vya maji na kuwachukulia hatua wale wanaochezea vyanzo hivyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TBL, Jose Moran, aliishukuru WWF na serikali kwa jitihada wanazofanya kuhakikisha kunakuwa na usalama wa maji muda wote nchini kwa kuwa yakikosekana, shughuli nyingi za uzalishaji mali zitasimama.

Alisema sio kwamba jitihada hizo zinasaidia kulinda vyanzo vya maji pekee, bali zinasaidia katika kudhibiti mabadiliko ya tabianchi kwa kuondokana na mabalaa kama ukame.

"Maji ni maisha na tunafahamu kwamba bila maji hakuna maisha na maji yamekuwa yakitoa mchango mkubwa sana kwenye maendeleo ya uchumi na yanasaidia sekta nyingi kama utalii, kilimo, viwanda na baada ya hewa kwa umuhimu hapa duniani kinachofuata ni maji," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na umuhimu huo kuna haja kwa serikali, wadau wote wa maendeleo na watumiaji wa maji kuchukua hatua madhubuti kulinda vyanzo vya maji, ili kuweka na uhakika kwa sasa na kwa vizazi vijavyo.

# Mganga wa jadi ahukumiwa kunyongwa kisa kuua watoto

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Sumbawanga imemuhukumu kunyongwa hadi kufa mganga wa jadi, James Kapyela (57) baada ya kumtia hatiani kwa kosa la mauaji ya watoto wawili wenye umri wa miaka saba na minne.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji wa Mahakama hiyo, Thadeo Menempazi baada ya mahakama hiyo kuridhika na ushahidi uliotolewa na mashahidi 11.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na mawakili Marieta Maguta na Saimon Peres ambao walidai mahakamani huko kuwa tukio hilo lilitokea Machi 23, 2019 katika Mtaa wa Vuta mjini Sumbawanga.

Wakili Peres alidai kuwa kabla ya kuthibitika kuwa watoto hao wameuawa, walipotea na kusababisha wazazi na majirani kuwatafuta na hata kutoa taarifa kituo cha polisi mjini Sumbawanga.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa, siku iliyofuata kuna binti alikuwa anakwenda mtoni kuchota maji na alimwona mtoto mmoja kati ya wale watatu waliopotea na akatoa taarifa kwa wazazi wake ambao baada ya kumwona aliwaeleza wazazi wake alikokuwa na kuacha wenzake ambao waliambatana naye kwa lengo la kwenda kuwatafuta.

Wakili huyo alidai kuwa walipofika kwenye nyumba ya mtuhumiwa, wazazi hao walikuta gari bovu ambalo lilikuwa limeegeshwa nje na walipofungua mlango wa gari hilo walikuta ndani kukiwa na kinyesi cha binadamu na harufu kali iliyowavuta nzi wengi.

Ilidaiwa kwamba baada ya kushuhudia hali hiyo, wazazi na majirani waliingia kwenye moja ya nyumba za Kapyela na ndani yake waliikuta miili ya watoto hao ikiwa imetupwa ndani ya nyumba hiyo iliyochakaa.

Inadaiwa baada ya uchunguzi wa kitabibu, ilibainika kabla ya kunyongwa watoto hao walilawitiwa.

Upande wa mashtaka uliiomba mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine wenye kufanya vitendo kama hivyo.

Upande wa utetezi uliongozwa na Wakili Deogratias Sanga huku mtuhumiwa akiwa hana mashahidi na alipopewa nafasi ya kujitetea aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa hilo ni kosa la kwanza kwake, pia ana familia inayomtegemea.

Jaji Mwenempazi alisema kuwa kwa kuzingatia kifungu cha namba 196 hadi namba 197 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, mahakama inamuhukumu kunyongwa hadi kufa.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, akizungumza katika uzinduzi wa mpango mkakati wa kuwawezesha madereva wa vyombo vya moto kupata huduma ya mafuta kwa bei nafuu zaidi hapa nchini, ulioandaliwa na Taasisi ya Wese, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanafunzi wakatisha masomo kisa umbali

**Na Vitus Audax,** KWIMBA

ZAIDI ya wanafunzi 90 wa Shule ya Sekondari Bupamwa, Kata ya Bupamwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza, wamekatisha masomo yao wakihofia usalama na vikwazo vingine kutokana na kutembea umbali mrefu kuifuata shule hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Bupamwa, Herman Daud, alisema licha ya serikali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa vinayokidhi idadi ya wanafunzi shuleni hapo, wanafunzi wanakumbwa na kikwazo cha kutembea umbali mrefu, hatua inayosababishia wengi wao katisha masomo.

Alisema katika mwaka wa masomo 2022, ni wanafunzi 61 tu waliohitimu masomo yao kati ya wanafunzi 153 walioanza kidato cha kwanza, hivyo wanafunzi 92 walisitisha masomo yao kwa nyakati tofauti.

Alibainisha kuwa wapo wanafunzi wanaotoka katika kijiji kilichoko umbali mrefu, hivyo kutumia muda mwingi kwa safari ya kwenda shuleni na kurejea majumbani.

"Waathirika wakubwa hapa ni wanafunzi wa kike huku wale wanaobahatika kuendelea na masomo hufika shuleni wakiwa wamechoka na kusinzia darasani wakati vipindi vikiendelea," alisema.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walieleza kuwa licha ya kuwapo shida ya umbali mrefu kufika shuleni, shule hiyo pia ina uhaba wa miundombinu ya kuhifadhia maji kwa ajili ya matumizi ya shuleni.

"Hatuna matangi ya kuhifadhia maji, hali inayosababisha kutumia muda mrefu katika shughuli za kuchota maji ambayo tunayafuata katika mabwawa mbalimbali yaliyoko umbali kidogo na shule yetu," alisema Debora Marango mwanafunzi wa kidato cha nne.

"Kuna ujenzi wa mabweni lakini yatakuwa kwa ajili ya wanafunzi wa kike pekee, hivyo na sisi tunaomba serikali pamoja na wadau mbalimbali wa elimu tusaidia hata kwa kuweka basi la shule, ili kutupunguzia adha hii ya kutembea umbali mrefu," alisema mwanafunzi Sylivester Machaina.

Diwani wa Bupamwa, Stephania Cheo, alisema mbali na serikali ya kata hiyo kwa kushirikiana na wananchi kufanikiwa kuanzisha ujenzi wa mabweni wanaiomba, serikali pia iongeze fedha katika ujenzi wa mabweni hayo kusaidia kukamilika kwake, ili wanafunzi wa kike waanze kuishi shuleni na kupunguza kasi ya wanafunzi kuacha shule.

"Zinahitajika Sh. milioni 40 kwa kila bweni ili kuweza kukamilika tunaomba serikali itazame pia katika adha hii ili waweze kusoma wakiwa shuleni wakati wote," alisema Diwani Cheo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI**
**Mkoa D,SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na 2036/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NURU WA ATHUMANI TUKUYU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AZALY JUMA SELEMANI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na husiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 Mwezi 11 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 10 mwaka 2022

---

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 845 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PIUS AUGUSTINO MTABAZI**
**And**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SARAH ENEAH MFINANGA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration)is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of NOVEMBER 2022
Dated at DAR ES SALAAM this 07th day of OCTOBER 2022

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

**IN THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA**
**AT SUMBAWANGA**
**CIVIL APPEAL NO.........OF 2022**
**IN THE MATTER OF AN INTENDED CIVIL APPEAL NO.....OF 20..**
**BETWEEN**
**BUSAD IBRAHIM (Administratrix of the Estate of the late Issa Mohamed Doon)...............APPELLANT**
**VERSUS**
**TREASURY GENERAL (FORMERLY CONSOLIDATED HOLDING CONSOLIDATED CORPORATION......1st RESPONDENT , WEMA H.LUMULIKO...4TH RESPONDENT**
**VIOVENA & CO.LTD...2nd RESPONDENT, GRACE H.LUMULIKO...5TH RESPONDENT**
**GODWIN E.NZINYANGWA...3rd RESPONDENT ,NEHEMIA PANYA...6TH RESPONDENT**
**AND**
**HON.ATTORNEY GENERAL...............NECESSARY PARTY**
**(Originating from the High Court of Tanzania in the District Registry of Sumbawanga at Sumbawanga Land case No.02 of 2010)**

**NOTICE OF APPEAL**
**(Under Rule 83 (1) of the Tanzania Court of Appeal Rules,GN,No.368 of 2009 as amended by GN No.344 of 2019)**

**TAKE NOTICE THAT,BUSAD IBRAHIM** (Administratix of the estate of the late Issa Mohamed Doon) being dissatisfied with the whole decision of Honorable Hon.K.N. Nyangarika,J,given at Sumbawanga on 04th day of December,2015 intends to appeal to the Court of Appeal of Tanzania against the whole of the said decision as decided.

**COPIES TO THE RESPONDENTS**
Dated this 30th day of September,2022

Signed...............................Advocate of Appellant.
To the Deputy Registrar of the High Court of Tanzania at Sumbawanga
Lodged in the High Court of Tanzania at Sumbawanga,this 3rd day of October,2022.

......................................
**DEPUTY REGISTRAR**

---

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF SUMBAWANGA**
**AT SUMBAWANGA**
**MISC LAND APPLICATION NO.07 OF 2021**
**(From the High Court of Tanzania at Sumbawanga Land Case No.02 of 2010)**
**BUSAD IBRAHIM (Administrix of the estate of the late Issa Mohamed Doon)...........APPLICANT**
**VERSUS**
**TREASURY GENERAL (FORMERLY CONSOLIDATED HOLDING CONSOLIDATED CORPORATION...1ST RESPONDENT, VIOVENA & CO.LTD...2ND RESPONDENT,**
**GODWIN E.NZINYANGWA...3RD RESPONDENT,WEMA H.LUMULIKO...4TH RESPONDENT,**
**GRACE H.LUMULIKO.....5TH RESPONDENT,NEHEMIA PANYA.......6TH RESPONDENT**
**AND**
**HON.ATTORNEY GENERAL...........................NECESSARY PARTY**
**APPLICATION FOR CERTIFIED COPIES OF RULING,DRAWN ORDER AND PROCEEDINGS**

**The above captioned matter refers.**
Kindly furnish us with certified Ruling,and proceedings delivered on 29th day of September,2022 by Hon.Ndunguru,J.for preparing a notice of appeal to the court of appeal of Tanzania and a letter applying for judgment ,decree and proceedings before this Court for appeal purpose.

**Yours faithfully,**
**COPIES TO THE RESPONDENTS**

......................................
**SIMON T.M.MWAKOLO**
**(ADVOCATE FOR THE APPLICANT)**

---

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF SUMBAWANGA**
**AT SUMBAWANGA**
**LAND CASE NO.02 OF 2010**
**BUSAD IBRAHIM (Administratix of The estate of the late Issa Mohamed Doon)...............PLAINTIFF**
**VERSUS**
**TREASURY GENERAL (FORMERLY CONSOLIDATED HOLDING CONSOLIDATED CORPORATION...1ST DEFENDANT,VIOVENA & CO.LTD....2ND DEFENDANT**
**GODWIN E.NZINYANGWA...3RD DEFENDANT,WEMA H.LUMULIKO...4TH DEFENDANT**
**GRACCE LUMULIKO......5TH DEFENDANT,NEHEMIA PANYA......6TH DEFENDANT**
**AND**
**HON.ATTORNEY GENERAL...................................NECESSARY PARTY**
**APPLICATION FOR CERTIFIED COPIES JUDGMENT,DECREE AND PROCEEDINGS FOR APPEAL PURPOSE**

**The above captioned matter refers,**
The plaintiff aggrieved with the whole decision of Hon.K.N.Nyangarika,J.dated 04th day of December,2015 in the above Land Case No.02 of 2010 applies to be furnished with certified copies of Judgment,decree and proceedings for appeal purpose after being granted leave to lodge a notice of appeal and a letter applying the above documents and serve the respondents in Misc.Land Application no.07 of 2021,intends to appeal to the Court of Appeal of Tanzania at Sumbawanga against the whole of the said decision as decided.
Kindly furnish us with certified copies of judgment,decree and proceedings for appeal purpose.
**Yours faithfully,**
**COPIES TO THE RESPONDENTS**

................................
**SIMON T.M.MWAKOLO**
**(ADVOCATE FOR THE PLAINTIFF)**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN CELESTINE MTEY** wa Majengo mjini Kahama,anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.126 DPC.** Yeyote atakayeiona ataoe taarifa kituo cha polisi kilicho jirani yake.
Taarifa ya polisi.
**KAH/RB/719/2022.**

---

**(Substituted Service)**
**IN THE DISTRICK LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR KAHAMA AT KAHAMA**
**LAND APPLICATION NO.01/2022.**
**JUAKALI SHIJA..........................APPLICANT**
**VERSUS**
**SALEHE NZINGULA AND LUCAS NZINGULA....................................RESPONDENT**

**TO; NDG, LUCAS NZINGULA.**

**TAKE** notice that, the above matter is coming for Mention on **01ST day of NOV, 2022** at 09:00 am Before Hon. **PAULOS L.S LEKAMOI** Chairman of the Tribunal. You are hereby commanded to appear in this Tribunal in Person or by Advocate or agent bully authorized when the case will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** that, in default of your appearance on the date and time above mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVEN under my HAND and the SEAL of this tribunal this 26 day of 10, 2022.**

CHAIRMAN

---

**Kwa Habari Motomoto Usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji ya matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# NMB yatoa samani kwa shule Mtwara

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

BENKI ya NMB mkoani Mtwara imetoa msaada wa madawati, viti na meza kwa shule tatu za msingi na mbili za sekondari zilizoko katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba vyenye thamani ya Sh. milioni 22.

Msaada huo ulikabidhiwa juzi na Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango kwa Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya katika Shule ya Msingi Dinyecha.

Samani hizo zitagawiwa kwa shule za msingi tatu za Kiwengulo, Mibobo na Dinyecha na shule za sekondari za Mnima na Nitekela, zote za Halmashauri ya Mji wa Nanyamba.

Akizungumza baada ya kupokea vifaa hivyo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Dinyecha, Shafii Moto, ambaye shule yake imepata madawati 50, alisema kuwa msaada huo utamaliza shida ya madawati miongoni mwa wanafunzi wake wa kawaida ambao mahitaji kwa ujumla ni madawati 205 kwa wanafunzi 594. Shule hii pia ina kitengo cha watoto wenye ulemavu.

"Madawati 50 yataondoa kabisa tatizo la vifaa hivyo shuleni kwetu na hii itawafanya wanafunzi kujielekeza katika masomo yao," alisema Moto.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, alisema kuwa Halmashauri ya Nanyamba ina shule za msingi 67, mahitaji ya madawati 8,167 lakini yaliyopo ni 7,121, hivyo kuna upungufu wa madawati 1,044.

"Msaada huu mlioutoa unaenda kupunguza kero tuliyonayo ya upungufu wa madawati katika halmashauri hii," alisema Kyobya.

Kyobya alisema halmashauri hiyo ina mahitaji ya viti na meza 4,687 katika shule zake za sekondari 12, upungufu wa viti 150 na meza 150, kwa hiyo msaada wa NMB umepunguza kero hiyo.

Shango alisema kuwa benki hiyo inawajibika kushirikiana na jamii kutatua shida ambazo zinawakabili wanajamii zikiwamo za sekta ya elimu, afya na majanga.

Alisema katika elimu benki hiyo inaamini kuwa ndio litapatikana taifa lililo bora na makini.

"Naipongeza serikali ya awamu ya sita ya Samia Suluhu Hassan kwa kuleta maendeleo bora kwa watoto kusoma vizuri na sisi kama wadau tunao wajibu wa kushirikiana na serikali ndio maana tumefika hapa leo," alsiema Shango.

Mwanafunzi wa darasa la sita, Yumna Ramadhani, aliishukuru Benki ya NMB kwa msaada wa madawati na kueleza kuwa sasa watakaa kwa utulivu na kuandika vizuri tofauti na mwanzo.

# Walioshtakiwa kesi ya mauaji waachiwa huru

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imewaachia huru washtakiwa watatu wanaotuhumiwa kumuua Charles Patrick baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) kuwasilisha mahakamani nia ya kutokuendelea na kesi hiyo.

Washtakiwa hao ni Mussa Malatu, Amon Joram na Joseph Wambura, walioachiwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Ferdinadri Kiwonde.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Faraja George, alidai kuwa DPP amewasilisha hati hiyo chini ya Kifungu 91 (1) cha Mwenendo wa Mkosa ya Jinai (CPA) kwamba hana nia ya kuendelea na mashtaka dhidi yao.

Hakimu Kiwonde alisema anakubaliana na kifungu hicho na ombi la DPP na ana waachia huru washtakiwa, lakini aliwaeleza kuwa kifungu hicho walichoachiliwa nacho upande wa mashtaka wanaweza kuwakamata tena na kuwashtaki.

Baada ya kauli ya hakimu, mawakili wa upande wa utetezi walidai kuwa hawana pingamizi na kuiomba mahakama isiruhusu washtakiwa kukamatwa tena.

Hakimu alisema kuwa upande wa mashtaka wana haki ya kuwakamata tena na kuwafungulia mashtaka hayo hayo washtakiwa hao kutokana na kifungu hicho.

Washtakiwa hao wanadaiwa kumuua Charles Patrick, Julai 8, 2015 Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Kesi hiyo imeondolewa wakati mashahidi wanaendelea kutoa ushahidi wao na shahidi wa kwanza alidai alikabidhiwa mshtakiwa Malatu na pia alifanikiwa kumkamata mtuhumiwa wa tatu Wambura.




Mkurugenzi wa Kiwanda cha Bia (TBL), Jose Moran (kushoto), akijadiliana jambo na Mkurugenzi Mkazi wa Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori na Mazingira Duniani (WWF), Dk. Amani Ngusaru, katika mkutano wa kujadili usalama wa maji jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mwinyi: TEHAMA inafungua ukurasa ukuaji mawasiliano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema kukamilika kwa kituo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na uzinduzi wa minara ya mawasiliano kutaleta manufaa makubwa kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana baada ya kuzindua kituo hicho katika eneo la Kisakasaka, Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Alisema hatua hiyo inafungua ukurasa mpya wa maendeleo ya mawasiliano na kuipaisha nchi kwenda sambamba na ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia ambao sekta ya mawasiliano ina umuhimu mkubwa.

Alisema kituo hicho kitasadia kuchochea huduma za uhakika za TEHAMA ambazo zinagusa maisha ya wananchi kiuchumi.

"Wito wangu kwa wananchi kuwa waangalizi wa miundombinu na kuzitumia huduma za kituo hiki kwa lengo lilokusudiwa," alisema.

Aidha, alisema katika kufungua ukurasa mpya wa mawasiliano visiwani humo ana upongeza Mfuko wa mawasiliano kwa wote kwa kushirikiana na kampuni ya simu ya Tigo na Zantel kutekeleza mradi wa ujenzi wa minara 42 katika shehia 38 Zanzibar.

Alisema ushirikiano wa aina hiyo una umuhimu mkubwa na haja ya kuendelezwa hasa katika miradi ya kimkakati.

Naye Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa mawasiliano kwa wote (UCSAF), Justina Mashiba, alisema wamejenga minara 42 ya mawasiliano Zanzibar ambayo imegharimu Sh. bilioni 6.9. Alisema pia vituo vya TEHAMA 11 vimejengwa, Unguja saba na Pemba vinne, lengo ni kuhakikisha hakuna Mtanzania anayeachwa nyuma katika teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mawasiliano, Suleiman Kakoso, aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuharakisha kutoa kibali cha ujenzi wa minara hiyo.

Aliiomba Serikali ya Tanzania kupitia Waziri Nape Nnauye, kufuata mwenendo wa Zanzibar kuharakisha upatikanaji kibali kwa sababu urasimu unakwamisha miradi ya maendeleo.

"Kule Tanzania bara ukiomba kibali cha ujenzi wa minara huchukua takriban mwaka mzima kitu ambacho kinakwamisha miradi mingine kufanyika," alisema.

Naye Waziri wa Habari, Teknolojia na Mawasiliano, Nape Nnauye alisema katika kuhakikisha huduma hizo zinafika kila pahala nia ya serikali ni kuchochea maendeleo na nchi inaingia katika uchumi wa kidigitali na uchumi wa buluu.

Alimpongeza Rais Mwinyi kwa hatua ya ujenzi wa minara na vituo hivyo vya TEHAMA kwa sababu kitendo alichokifanya ni cha kiungwana, kutatua changamoto ya mawasiliano.

Alisema katika upatikanaji wa mawasiliano bora wizara yake kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wizara ya Ujenzi Zanzibar na wadau wa mawasiliano walifanya zoezi la kuangalia changamoto ya mawasiliano na shehia 38 zilibainika na kujenga minara ili kupata huduma za mawasiliano.

Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano Zanzibar, Dk Khalid Salum Muhammed alisema, kasi ya maendeleo ya mawasiliano ni kubwa. Alisema chimbuko hilo la minara linatokana na kazi ya Dk Mwinyi baada ya kupokea malalamiko ya changamoto ya mawasiliano kwa wananchi na kulipatia ufumbuzi.

Pia Dk Mwinyi alifungua kongamano la TEHAMA litakalofanyika kwa siku tatu.

# M-BET SASA YAIGEUKIA SIMBA QUEENS, YAIMWAGIA BILIONI 1/-

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umeingia mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya shilingi bilioni moja na Kampuni ya Kubashiri Michezo ya M-Bet, huo ukiwa ni udhamini wa timu ya wanawake pekee, Simba Queens, inayoshiriki Ligi Kuu Wanawake Tanzania na kwa sasa ikiwa nchini Morocco kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, alisema walianza mazungumzo na makampuni mbalimbali, lakini M-Bet ndiyo iliyoonyesha dhamira ya kweli katika kuidhamini Simba Queens. Mtendaji huyo alisema udhamini wa mkataba huo hauhusiana na ule wa timu kubwa ya wanaume ambao waliingia Agosti Mosi, mwaka huu.

Alisema udhamini huo unaanza kufanya kazi rasmi kwa timu hiyo kuonekana na jezi zenye nembo ya M-bet katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo Jumamosi wiki hii itashuka dimbani nchini Morocco dhidi ya wenyeji, ASFAR FC .

"Mkataba huu tutapata Sh. milioni 200 kila mwaka pamoja na mahitaji mengine muhimu kwa timu, ikiwamo mishahara, bonasi na mechi za Simba kuonyeshwa mubashara, michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kikosi kipo Morocco na mechi ya Jumamosi dhidi ya ASFAR katika michuano hiyo itaonyeshwa mubashara," alisema Barbara.

Alisema kampuni hiyo imegeukia timu ya Wanawake ya Simba Queens kwa kudhamini ili iendelee kufanya vizuri katika michezo mbalimbali inayoendelea kushiriki.

Naye Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet ambao pia ni wadhamini wakuu wa timu ya wanaume ya Simba, Allen Mushi, alisema M-Bet inafaraja kubwa kuwekeza katika michezo kwenye soka la wanawake kupitia Simba Queens.

"Namba ziko wazi kwa Simba Queens, hasa kwenye soka la wanawake, kwetu sisi imekuwa nafasi ya kukuza soka la wanawake iwe na uwiano mzuri na soka la wanaume," alisema Allen.

Agosti Mosi, mwaka huu M-Bet iliingia mkataba wa miaka mitano na Klabu ya Simba kwa timu kubwa ya wanaume wenye thamani ya Sh. bilioni 26.1.

Katika mkataba huo Simba inapokea Sh. bilioni 4.6 kwa mwaka wa kwanza, mwaka wa pili Sh. bilioni 4.9, wa tatu Sh. bilioni 5.2, wa nne Sh. bilioni 5.5 na mwaka wa mwisho Sh. bilioni 5.8.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022.

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2022 | Robo Mwaka iliopita 31 Juni 2022 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,035.91 | 533.23 |
| 2 | Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 5,700.62 | 5,905.93 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za serikali | 43,397.06 | 41,322.94 |
| 4 | Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,872.40 | 1,579.50 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 44.68 | 11.61 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 5,333.24 | 24,548.82 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 47,624.19 | 47,341.87 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,499.65 | 1,249.05 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 532.62 | 614.20 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **107,040.38** | **123,107.15** |
| B | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 11,595.00 | 23,150.00 |
| 18 | Amana za Wateja | 52,432.17 | 56,818.67 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,551.67 | 1,709.94 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 620.20 | 417.02 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **66,199.04** | **82,095.63** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | **40,841.33** | **41,011.52** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 1,367.28 | 1,335.35 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 5,549.14 | 6,073.52 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,094.91 | 772.64 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **40,841.33** | **41,011.52** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 5,476.54 | 4,355.43 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,707.74 | 1,634.45 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 441.08 | 426.67 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 38.16% | 33.31% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.55% | 3.42% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 75.05% | 59.71% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 44.49% | 38.46% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 91.77% | 93.25% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -19.93% | 1.89% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -13.05% | 0.48% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2022 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30 Septemba 2021 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,079.17 | 2,484.38 | 6,667.88 | 7,201.42 |
| 2 | Gharama za Riba | 851.73 | 811.26 | 2,536.19 | 2,431.70 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,227.43** | **1,673.12** | **4,131.69** | **4,769.72** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 14.41 | (50.75) | 3.16 | 87.72 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **140.15** | **230.15** | **463.59** | **575.76** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 24.19 | 32.64 | 141.63 | 97.99 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 115.96 | 197.51 | 321.96 | 477.77 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **916.84** | **827.73** | **2,849.82** | **2,455.44** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 389.05 | 334.90 | 1,239.45 | 1,034.27 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 9.53 | 9.57 | 21.29 | 21.43 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 518.27 | 483.26 | 1,589.07 | 1,399.74 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **436.33** | **1,126.29** | **1,742.31** | **2,802.32** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 114.06 | 270.00 | 647.40 | 810.00 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **322.26** | **856.29** | **1,094.91** | **1,992.32** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 26 | 25 | 26 | 25 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 10 | 26 | 33 | 61 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 10 | 26 | 33 | 61 |
| 14 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.12% | 2.73% | 1.19% | 2.17% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.15% | 8.71% | 3.57% | 6.88% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 67.04% | 43.49% | 62.02% | 45.93% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 4.61% | 5.75% | 4.89% | 5.56% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2022 | Robo Mwaka iliopita 31 Juni 2022 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 322.26 | 164.89 | 1,094.91 | 1,992.32 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| | Hasara katika mali | 97.76 | 93.81 | (119.13) | 301.84 |
| | -Badiliko halisi katika Mikopo | (282.33) | (199.50) | 3,491.20 | (3,387.61) |
| | Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika Amana | (15,941.50) | 1,481.44 | (29,057.44) | 2,727.61 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 229.99 | (755.60) | 1,040.87 | 1,245.24 |
| | Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 2,159.75 | 363.49 | (95.21) | (1,082.07) |
| | Kodi iliyolipwa | (114.06) | (233.33) | (647.40) | (810.00) |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(13,528.12)** | **915.20** | **(24,292.19)** | **987.32** |
| II | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | (16.18) | (73.18) | 312.89 | (6.03) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 2,651.94 | (9,851.94) | (7,770.60) | (2,171.58) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **2,635.76** | **(9,925.12)** | **(7,457.71)** | **(2,177.61)** |
| III | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | (492.45) | - | (492.45) | - |
| | Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo(bainisha) | (70.98) | (69.25) | (207.78) | (188.24) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(563.43)** | **(69.25)** | **(700.23)** | **(188.24)** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (11,455.79) | (9,079.17) | (32,450.13) | (1,378.53) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 26,106.96 | 35,186.13 | 47,101.31 | 36,896.83 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **14,651.18** | **26,106.96** | **14,651.18** | **35,518.30** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 30/09/2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **6,129.50** | **1,279.37** | **-** | **-** | **40,238.87** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,094.91 | - | - | - | **1,094.91** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (492.45) | - | - | - | **(492.45)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (87.91) | 87.91 | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **6,644.05** | **1,367.28** | **-** | **-** | **40,841.33** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **4,754.21** | **41.35** | **-** | **-** | **37,625.56** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,613.31 | - | - | - | **2,613.31** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,238.02) | 1,238.02 | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **6,129.50** | **1,279.37** | **-** | **-** | **40,238.87** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 Septemba 2022**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| ***Jina*** | ***Cheo*** | ***Sahihi*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 24-10-2022 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 24-10-2022 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 24-10-2022 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| ***Jina*** | ***Cheo*** | ***Sahihi*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| RAJAB S KAKUSA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 24-10-2022 |
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 24-10-2022 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 24-10-2022 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**


# Metacha, Farouk wala kifungo TFF

**Na Adam Fungamwango**

KAMATI ya Uendeshaji na Usimamisi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) imemfungia michezo mitatu na kulipa faini ya shilingi milioni moja, golikipa wa timu ya Singida Big Stars, Metacha Mnata kwa kosa la kumpiga kwa makusudi straika wa Mtibwa Sugar, Charles Ilamfya.

Katika kikao chake cha Oktoba 24, pamoja na kuamua mambo mbalimbali ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Championship, kamati hiyo imefanya maamuzi hayo kwa kuzingatia kanuni zinazoongoza mchezo huo.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, imesema kuwa kamati hiyo imemkuta na hatia kipa huyo kumpiga mchezaji wa timu pinzani kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa uwanja wa Manungu Complex, Oktoba 18, mwaka huu na Mtibwa ikashinda kwa bao 1-0.

Kamati hiyo pia imeipiga faini ya shilingi milioni moja Klabu ya Prisons baada ya mashabiki wake kuwatolea lugha ya matusi wasimamizi wa mchezo kati ya timu hizo mbili uliochezwa Oktoba 9, kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro.

Hali hiyo ilitokea baada ya mashabiki hao kutaka kuingia uwanjani bure, bila ya kukata tiketi, timu hizo zikitoka suhulu.

Pia, kamati hiyo imemfungia miezi mitatu na kumtoza shilingi laki tano kocha wa makipa wa Namungo FC, Farouk Ramadhani baada ya kuwatolea lugha ya matusi watoto waokota mipira wa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

Imedaiwa kuwa kipa huyo wa zamani wa Simba katikati ya miaka ya 1990, alikuwa akiwashutumu watoto hao kuwa walikuwa wanachelewesha kurudisha mipira uwanjani kwa makusudi.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa Oktoba 19, Polisi Tanzania ikiwa wenyeji, Namungo ilipoteza kwa bao 1-0.

## ZISIKUPITE

### GUNDOGAN AWANIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inafikiria msimu ujao kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan, mwenye umri wa miaka 32. (***90Min***)

### NEVES AWINDWA BARCA

BARCELONA wako kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, kutoka Wolves, na makubaliano yanaaminika huenda yakaafikiwa Januari. (Sport)

### RONALDO TATIZO MSHAHARA

KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim amesema kila mtu katika klabu hiyo "ana ndoto" ya mshambuliaji wa Ureno wa Manchester United, Cristiano Ronaldo, kurejea katika klabu hiyo. Hata hivyo, timu hiyo ya Ureno haiwezi kumudu mshahara wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37. (***Football London***)

### MESSI KUONGEZEWA MKATABA

KLABU ya Paris St-Germain inataka kuongeza mkataba wa Lionel Messi kwa miezi 12 zaidi. Mkataba wa sasa wa mshambuliaji huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 35, unatarajiwa kumalizika Juni 2023. (***Le Parisien***)

### LOKONGA, SAVIC KUPISHANA

ARSENAL wako tayari kumtoa kiungo wa Ubelgiji, Albert Sambi Lokonga mwenye umri wa miaka 23, kama sehemu ya makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Lazio na Serbia, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 27. (***Calciomercato***)

### KOVACIC NA MKATABA

CHELSEA wana nia ya kuanza mazungumzo ya mkataba mpya na kiungo wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic, mwenye umri wa miaka 28, baada ya Kombe la Dunia. Mkataba wake wa sasa umebakiza chini ya miaka miwili. (***Evening Standard***)

### CHELSEA KUIBOMOA BRIGHTON

CHELSEA wanamtaka mkuu wa masuala ya usajili wa Brighton, Paul Winstanley baada ya kuwaleta Wakurugenzi wa Ufundi, Laurence Stewart, kutoka Monaco, na Christopher Vivell, aliyekuwa RB Leipzig, pamoja na mkurugenzi mwenza wa zamani wa Southampton, Joe Shields. (***Guardian***)

### RONALDO AGEUKIA MAREKANI

CRISTIANO Ronaldo anaweza kufanya uchaguzi wa kuhamia Marekani katika moja ya Klabu ya Inter Miami, LA Galaxy na LAFC. (***Los Angeles Times***)

### EDWARDS KWENDA UNITED

MANCHESTER United wamefurahishwa na kazi inayofanywa na mkurugenzi wa soka, John Murtough huku kukiwa na tetesi kwamba wanakaribia kumteua Mkurugenzi wa zamani wa Liverpool, Michael Edwards katika nafasi hiyo. (***Express***)

### CITY ASILIMIA 40 KWA DIAZ

MANCHESTER City itapokea asilimia 40 ya ada yoyote ya uhamisho iwapo Real Madrid itaamua kumuuza kiungo wa kati wa Hispania, Brahim Diaz mwenye umri wa miaka 23 kwenda Manchester United. Kipengele hicho kilijumuishwa katika uhamisho wa Diaz wa pauni milioni 15.5 kutoka City kwenda Real mwaka 2019 na bado ni halali. (***Gazzetta dello Sport, via Star***)

### ABOUKHLAL KUTUA LEICESTER

KLABU ya Leicester City ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Morocco, Zakaria Aboukhlal, mwenye umri wa miaka 22 kutoka Toulouse. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI, MBAPPE, NEYMAR FAHARI PSG UEFA - HAKIMI

### ●●● Kila mtu anajua ubora wa kiufundi wa watatu hawa, lakini tunatambua kwamba...

**PARIS,** UFARANSA

KLABU ya Paris Saint-Germain inaweza "kufanya mambo makubwa" katika Ligi ya Mabingwa ULaya ikiwa washambuliaji watatu Kylian Mbappe, Lionel Messi na Neymar wataendelea na kiwango chao kizuri, kwa mujibu wa beki, Achraf Hakimi.

Huku Neymar akifanya kazi nyuma ya Mbappe na Messi, wote watatu walifunga wakati kikosi hicho cha kocha Christophe Galtier, kikifuzu hatua ya mtoano kwa ushindi wa mabao 7-2 dhidi ya Maccabi Haifa pale Parc des Princes, Jumanne.

Wakiungwa mkono na safu ya kiungo inayoongozwa na Fabian Ruiz, Renato Sanches na Vitinha, watatu hao wa mbele walikuwa na uhuru zaidi wa kufunga mabao saba katika mchezo huo.

"Tulicheza mchezo mzuri, tulitimiza lengo la kufuzu," alisema Hakimi akiiambia RMC Sport 1.

"Tulifunga mabao mengi. Kocha alichagua mfumo kujaribu mambo.

"Kocha anapenda kucheza na safu hii ya kiungo, tunatumaini uwezekano mzuri kwa timu. Ikiwa watatu wa mbele watakaa hivyo, inawezekana kufanya mambo makubwa. Tunafurahi wote walifunga."

**Naye kocha Galtier aliongeza: "Itakuwa inatufanya tufikiri kwamba tuna timu bora zaidi duniani. Kuna timu za ubora wa juu katika mashindano haya.**

"Lakini nina wachezaji watatu wa ajabu mbele, tulilazimika kutafuta mfumo ili waweze kucheza kwa uhuru zaidi.

"Kila mtu anajua ubora wa kiufundi wa watatu hawa, lakini tunatambua kwamba, katika mashindano haya. Inafurahisha sana kuona, wanacheza kwa pamoja."

Ingawa waliruhusu mabao mawili, Galtier alifurahishwa na uchezaji wa jumla wa wachezaji wake, ambao amewahimiza kujihakikishia nafasi ya kwanza katika Kundi H watakapomenyana na Juventus wiki ijayo.

"Ninajutia bao la pili. Tulikosa mahitaji na ukakamavu mwanzoni mwa kipindi cha pili ili kuepuka kufufua timu," alisema.

"Mbali na hayo, nimefurahishwa na mchezo huo. Kwa ujumla, timu imekuwa ya ajabu. Tulicheza soka la kusisimua, la tahadhari, na uhusiano mwingi wa kiufundi na uhusiano kati ya mistari. Nimeridhika.

"Tumefuzu; ni nzuri sana, ni muhimu zaidi. Mashindano hayajaisha, tunapaswa kutafuta nafasi ya kwanza dhidi ya Juventus. Matarajio ya PSG ni kumaliza wa kwanza. Tunabaki na lengo hili."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,044,3

MECHI KALI

AZAM
VERSUS
SIMBA

1 | 4.10
X | 3.03
2 | 1.90

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom | m-pesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HENRY AMKINGIA KIFUA ALLEGRI JUVENTUS



**LONDON,** England

THIERRY Henry anahisi Juventus wana matatizo "kutoka juu hadi chini" na kumtimua Massimiliano Allegri hakutabadilisha chochote.

Kichapo cha mabao 4-3 kutoka kwa Benfica Jumanne kiliifanya Juve kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, na hawataweza kuangukia kwenye Ligi ya Europa kama Maccabi Haifa watashinda mchezo wao wa mwisho wa makundi.

Kipigo cha 'The Bianconeri' hao mjini Lisbon kilikuwa cha tatu katika michezo mitano iliyopita kwenye mashindano yote, huku kikosi hicho cha kocha Allegri kikiwa nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A na kikipitwa pointi 10 na vinara Napoli.

Hiyo ni mara ya kwanza kwa Juve kuondolewa hatua ya makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu msimu wa 2013-14 na kumeongeza shinikizo kwa Allegri, lakini mshambuliaji wa zamani wa Bianconeri hao, Henry anaamini kumfukuza kocha huyo hakutabadilisha hali yao.

"Wakifikiri hivyo wanakosea, nadhani kuna matatizo mengi kutoka juu hadi chini na uwanjani mambo hayaendi sawa pale," alisema akiiambia CBS Sports.

"Nilisema wakati (Andrea) Pirlo anaondoka, nilisema wakati (Maurizio) Sarri anaondoka, yeye si kocha mbaya.

"Ni nini kinaendelea nyuma ya milango iliyofungwa, hatujui. Inachukua muda wakati mwingine. Si kwamba ukimleta tu Allegri, mambo yatakuwa tofauti.

"Tumemuona (Mikel) Arteta (akiwa Arsenal); ilimchukua miaka miwili kuweka timu nzuri uwanjani.



# Di Maria kumalizia soka klabu yake ya utotoni

**TURIN,** Italia

WINGA wa Juventus, Angel Di Maria, anataka kumalizia maisha yake ya uchezaji soka sehemu aliyoanzia katika Klabu ya Rosario Central ya nyumbani kwao nchini Argentina.

Di Maria mwenye umri wa miaka 34, alijiunga na Rosario akiwa na umri wa miaka minne, akitumia miaka 15 iliyofuata na klabu hiyo kabla ya kucheza kama nyota katika Kombe la Dunia la Vijana chini ya umri wa miaka 20 na baadaye kutua Benfica.

Kuhamia kwake Benfica ulikuwa mwanzo wa maisha mazuri ya Ulaya, ambapo akazichezea kwa nyakati tofauti Real Madrid, Manchester United na Paris Saint-Germain kabla ya kutua Juventus.

Licha ya mafanikio yake yote barani Ulaya, Di Maria amezungumza kuhusu nia yake ya kurejea kwenye mizi yake katika mahojian na mchezaji wa zaman Ezequiel Lavezzi, an baye aliiwakilisha Arge tina kwenye michuan ya kimataifa mara 51 ka ya 2007 na 2016.

"Ningependa kuru Rosario," alisema. "N jua ni vigumu... laki ni kama ninavyosem siku zote ndoto ya wo walioko Argentina kuja kucheza Ulay yangu ni kurejea sik moja kuichezea Rosar Central.

## HABARI MICHEZO


# 303,118/-

# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/10/22 | 17:00 | Hull City vs Blackburn | 2.59 | 3.19 | 2.74 |
| 02. 29/10/22 | 17:00 | Wigan vs Watford | 2.93 | 3.28 | 2.39 |
| 03. 29/10/22 | 17:00 | Preston vs Middlesbrough | 2.68 | 3.13 | 2.68 |
| 04. 29/10/22 | 17:00 | Huddersfield vs Millwall | 2.99 | 3.24 | 2.37 |
| 05. 29/10/22 | 17:00 | Brighton vs Chelsea | 2.94 | 3.29 | 2.38 |
| 06. 29/10/22 | 19:30 | Fulham vs Everton | 2.29 | 3.42 | 2.97 |
| 07. 29/10/22 | 19:30 | Eintracht Frankfurt vs Borussia Dortmund | 2.93 | 3.52 | 2.25 |
| 08. 29/10/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.53 | 3.53 | 2.58 |
| 09. 30/10/22 | 15:00 | AJ Auxerre vs AC Ajaccio | 2.45 | 3.07 | 2.97 |
| 10. 30/10/22 | 15:30 | Hannover vs Karlsruher SC | 2.41 | 3.43 | 2.79 |
| 11. 30/10/22 | 15:30 | Sandhausen vs Eintracht Braunschweig | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 12. 30/10/22 | 15:30 | Paderborn vs Hamburger SV | 2.28 | 3.73 | 2.79 |
| 13. 30/10/22 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 14. 30/10/22 | 17:00 | Brest vs Reims | 2.40 | 3.33 | 2.83 |
| 15. 30/10/22 | 18:30 | Boavista vs Vizela | 2.50 | 3.25 | 2.80 |
| 16. 30/10/22 | 19:00 | Sandefjord vs Ham-Kam | 2.58 | 3.37 | 2.63 |
| 17. 30/10/22 | 19:05 | Lorient vs Nice | 2.57 | 3.26 | 2.67 |

# MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 27/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 3415 | Barito Putera vs PS Tni | 3.40 | 3.16 | 2.04 |
| 12:00 | 3855 | Hyundai Steel W vs Daejeon Sportstoto W | 1.14 | 6.80 | 13.61 |
| 13:00 | 2208 | Welayta Dicha FC vs Hadiya Hosahina FC | 3.40 | 2.82 | 2.22 |
| 13:00 | 4077 | FC Seoul vs Jeonbuk Hyundai | 3.21 | 3.21 | 2.09 |
| 14:30 | 4011 | Teraktor Sazi vs Malavan Bandar Anzali | 1.81 | 2.97 | 4.76 |
| 16:00 | 1888 | Ethiopia Bunna SC vs Arba Minch Kenema | 2.54 | 2.83 | 2.83 |
| 16:30 | 2319 | Sanat Naft Abadan vs Peykan FC | 2.86 | 2.62 | 2.71 |
| 16:30 | 2485 | Persepolis FC vs Sanat Mes Kerman FC | 1.44 | 3.65 | 7.59 |
| 16:30 | 4923 | Rans Nusantara vs Bhayangkara Surabaya Utd | 3.69 | 3.26 | 1.92 |
| 17:00 | 3220 | Dinamo Bucuresti vs CSM Slatina | 1.74 | 3.45 | 4.27 |
| 17:00 | 3642 | Delhi Dynamos FC vs Bengaluru FC | 2.29 | 3.36 | 2.73 |
| 17:00 | 5263 | AL Salt vs Sahab Club | 2.74 | 2.93 | 2.54 |
| 18:30 | 1330 | Foolad Khuzestan vs Gol Gohar | 2.40 | 2.52 | 3.49 |
| 19:00 | 5043 | Azam vs Simba | 4.10 | 3.03 | 1.90 |
| 19:45 | 1042 | PSV Eindhoven vs Arsenal | 2.69 | 3.47 | 2.44 |
| 19:45 | 1175 | FC Zurich vs Bodo Glimt | 3.40 | 3.70 | 1.98 |
| 19:45 | 1560 | FC Vaduz vs AZ Alkmaar | 5.61 | 4.51 | 1.49 |
| 19:45 | 1577 | Slovacko vs FC Koln | 3.44 | 3.69 | 1.97 |
| 19:45 | 1846 | Fenerbahce vs Rennes | 2.59 | 3.19 | 2.69 |
| 19:45 | 1918 | Anderlecht vs Steaua Bucuresti | 1.31 | 5.20 | 8.79 |
| 19:45 | 1959 | Ludogorets Razgrad vs Betis | 3.09 | 3.39 | 2.21 |
| 19:45 | 2065 | Lazio vs Midtjylland | 1.58 | 4.20 | 5.00 |
| 19:45 | 2268 | Nice vs Partizan | 1.70 | 3.70 | 4.71 |
| 19:45 | 2592 | Union Berlin vs Sporting Braga | 1.80 | 3.64 | 4.19 |
| 19:45 | 3500 | Villarreal vs Hapoel Beer Sheva | 1.38 | 4.91 | 7.01 |
| 19:45 | 4556 | Fiorentina vs Basaksehir | 1.76 | 3.70 | 4.30 |
| 19:45 | 4785 | Austria Vienna vs Lech Poznan | 2.50 | 3.35 | 2.70 |
| 19:45 | 5778 | AEK Larnaca vs Dynamo Kiev | 3.20 | 3.30 | 2.20 |
| 19:45 | 5822 | Malmo vs Union Saint Gilloise | 3.49 | 3.44 | 2.03 |
| 20:15 | 2450 | FAR Rabat vs Hassania Agadir | 1.97 | 3.35 | 3.80 |
| 22:00 | 1039 | Molde vs Djurgardens IF | 1.76 | 3.79 | 4.19 |
| 22:00 | 1145 | Slovan Bratislava vs Pyunik Yerevan | 1.48 | 4.20 | 6.40 |
| 22:00 | 1171 | Sturm Graz vs Feyenoord | 3.35 | 3.65 | 2.01 |
| 22:00 | 1684 | Nantes vs Karabakh | 2.29 | 3.46 | 2.91 |
| 22:00 | 1740 | HJK Helsinki vs Roma | 8.75 | 5.17 | 1.31 |
| 22:00 | 1748 | Red Star Belgrade vs Trabzonspor | 2.09 | 3.45 | 3.30 |
| 22:00 | 2107 | Shamrock Rovers vs KAA Gent | 5.00 | 3.85 | 1.64 |
| 22:00 | 2586 | FC Basel vs Zalgiris | 1.38 | 4.81 | 7.21 |
| 22:00 | 3059 | KF Ballkani vs Slavia Prague | 5.44 | 4.03 | 1.59 |
| 22:00 | 3265 | West Ham vs Silkeborg | 1.41 | 4.70 | 6.79 |
| 22:00 | 3534 | Omonia Nicosia vs Real Sociedad | 6.39 | 4.30 | 1.47 |
| 22:00 | 3581 | Sivasspor vs CFR Cluj | 2.24 | 3.18 | 3.33 |
| 22:00 | 4047 | Hearts vs Rigas Futbola Skola | 1.70 | 3.80 | 4.59 |
| 22:00 | 4293 | Manchester Utd vs Sheriff Tiraspol | 1.13 | 7.27 | 21.11 |
| 22:00 | 4518 | Ferencvaros TC vs Monaco | 3.55 | 3.60 | 1.96 |
| 22:00 | 4778 | SC Freiburg vs Olympiakos | 1.48 | 4.30 | 6.20 |
| 22:00 | 5291 | SC Dnipro 1 vs Apollon Limassol | 1.96 | 3.50 | 3.65 |
| 22:30 | 4598 | RS Berkane vs Olympique Khouribga | 1.83 | 3.25 | 4.07 |
| 23:00 | 3987 | Nacional Asuncion vs Guairena FC | 1.78 | 3.35 | 4.18 |
| 23:00 | 5095 | Club Guarani vs Libertad Asuncion | 4.48 | 3.66 | 1.66 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# POLISI TANZANIA YATIMUA KOCHA, BARAZA NAYE AKALIA KUTI KAVU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI timu ya Polisi Tanzania, ikitangaza rasmi kuachana na Kocha Mkuu, Joslin Sharif, kutokana na mwendelezo wa timu hiyo kufanya vibaya Ligi Kuu Bara, Kagera Sugar nayo ipo hoi kwenye ligi hiyo, huku kukiwa na taarifa za Kocha Mkuu, Francis Baraza kukalia kuti kavu.

**Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, Frank Lukwaro, imesema klabu hiyo imefikia makubaliano ya pande zote mbili kuvunja mkataba na Kocha Mkuu, Sharif kutokana na mwenendo usioridhisha.**

Hivi karibuni klabu hiyo ilimwita kocha huyo, msaidizi wake, Agustine Damina na kocha wa magolikipa, Emmanuel Mwansule, makao makuu ya klabu hiyo, Moshi, Kilimanjaro ili kwenda kuzungumza na uongozi kuhusiana na mwenendo mbaya wa timu.

"Vile vile, kocha msaidizi Augustine na kocha wa makipa, Mwansile wao watapangiwa majukumu mengine na katika kipindi hiki kigumu, timu itaendelea kuongozwa na John Tamba," iliandika sehemu ya taarifa hiyo.

Polisi Tanzania juzi ilikutana na kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Prisons, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya. Ni matokeo mabaya zaidi kuwahi kutokea kwenye timu hiyo tangu zipande Ligi Kuu.

Kwingineko, upande wa Kagera Sugar, taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zimedai huenda ikamtimua kocha huyo raia wa Kenya na kumrejesha kocha wa zamani, Mecky Mexime, baada ya timu hiyo kutokuwa na matokeo mazuri tangu kuanza kwa msimu huu.

Hata hivyo, Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Ali Masoud, amesema hawajampa idadi ya mechi kocha huyo, badala yake wapo kwenye tathmini ni kwa nini timu yao haifanyi vizuri.

Kagera Sugar ilichapwa mabao 2-1 dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi juzi.

"Si kweli kwamba tumemuacha kocha wetu au tunatarajia kumuacha Baraza, ila tutakaa na yeye pamoja na benchi la ufundi ili kujua tatizo ni nini, huwezi kumuacha mwalimu wakati hujajua tatizo ni nini, unaweza baadaye kukuta tatizo siyo yeye halafu umeshamuacha, utafanyaje?" Alisema Masoud.




Makocha wa Azam FC, Kaimu Kocha Mkuu, Kali Ongalla (katikati), akijadili jambo mazoezini jana na wasaidizi wake, Kocha wa Makipa, Daniel Cadena (kulia), pamoja na mchezaji mwandamizi, Aggrey Morris. Azam FC itaikaribisha Simba kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa leo usiku. **MPIGAPICHA WETU**

# *Simba, Azam mechi ya viwango, ufundi*

INATOKA UKURASA 32

Kabla ya mchezo wa jana usiku kati ya Yanga na KMC FC, Mtibwa Sugar iliyoshuka dimbani mara tisa, ilikuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 15, moja mbele ya Simba na Yanga, lakini zenyewe zikicheza mechi sita kila moja.

Azam FC iliyoshuka dimbani mara saba, ipo nafasi ya nane na pointi 11 baada ya kushinda mechi tatu, sare mbili na kupoteza michezo miwili.

Hadi jana kabla ya Yanga kushuka dimbani dhidi ya KMC FC, mabingwa hao watetezi pamoja na Simba, ni timu pekee msimu huu ambazo hazijapoteza mechi yoyote kwenye ligi hiyo inayoshirikisha miamba 16.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 27, 2022

Nipashe




‘Messi, Mbappe, Neymar fahari PSG Uefa’ UKURASA 29

## UDHAMINI ZAIDI...




Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet, Allen Mushi (katikati) na Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally (kushoto), wakionyesha mfano wa hundi ya Sh. bilioni moja baada ya kampuni hiyo ya kubashiri matokeo ya michezo kuingia mkataba wa miaka mitano wa kuidhamini Timu ya Wanawake ya Simba Queens. Hafla ya kutangaza udhamini huo ilifanyika jijini Dar es Salaam jana. **Habari zaidi Uk. 28. NA MPIGAPICHA WETU**

## Metacha, Farouk wala kifungo TFF

**Na Adam Fungamwango**



KAMATI ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB)...

HABARI UK. 28

## Henry amkingia kifua Allegri



**LONDON,** England

THIERRY Henry anahisi Juventus wana matatizo “kutoka...

HABARI UK. 30

# SIMBA, AZAM MECHI YA VIWANGO, UFUNDI

## ●●● Makocha wakiri kila upande upo vizuri, safu za ushambuliaji moto, mabeki Wanalambalamba...

**Na Saada Akida**

WAKATI miamba ya soka, Simba na Azam FC, ikishuka dimbani leo kuwania pointi tatu muhimu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, makocha wa timu hizo kila mmoja amekiri mpinzani wake kuwa na kikosi imara, lakini wakiahidi kucheza soka safi litakalotawaliwa na viwango na ufundi mwingi.

**Azam FC itakakuwa mwenyeji katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa leo saa moja usiku huku ikitoka kupoteza mechi iliyopita kwa mabao 2-1 dhidi ya KMC FC, wakati Simba mchezo uliopita dhidi ya Yanga ikibeba pointi moja baada ya sare ya bao 1-1.**

Katika mcheo huo wa leo, Simba itawakosa nyota wake wanne, Sadio Kanoute, Israel Mwenda na Jimmyson Mwanuke, ambao ni majeruhi wakati Kiungo ‘Punda’ Mzamiru Yassin akikosekana kutokana na kulazimika kuwa nje ya uwanja akitumikia adhabu ya kadi tatu za njano.

Hata hivyo, taarifa njema kwa Simba ni kurejea kwa beki wa kulia, Shomari Kapombe, ambaye yupo tayari kwa mchezo huo, hivyo itategemea na chaguo la kocha nani aanze kwenye nafasi hiyo.

Akizungumzia mchezo huo jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema maandalizi yamekamili na wanajua wanaenda kukutana na timu ya aina gani kwa kuwa wanaifahamu vizuri Azam FC inavyocheza.

Alisema kikubwa Wanasimba ni kuwaombea wachezaji wao kuamka na afya njema kwa sababu kiufundi na mbinu kila kitu kimekamili na kuwa tayari kwa ajili ya kupata matokeo mazuri leo.

“Baada ya kukamilika kwa mchezo wa ‘dabi’, umekuwa maandalizi mazuri kwa mchezo wetu dhidi ya Azam FC, tutawakosa nyota wetu wanne lakini waliobakia wote wako fiti na tayari kwa ajili ya mchezo wa kesho (leo).

“Taarifa njema ni kurejea kwa Kapombe na tayari amerejea kikosini na kuendelea na mazoezi, suala la kucheza litakuwa jukumu langu la nani kucheza katika mchezo wetu dhidi ya Azam FC,” alisema Mgunda.

Alisema wanaifahamu Azam FC watacheza kwa tahadhari kubwa na kuwaheshimu wapinzani kutokana na kikosi chao kuwa imara na bora kulingana na wachezaji walikuwa nao.

Nahodha wa Simba, Gadiel Michael, alisema wamejianda vizuri kuelekea mchezo wao dhidi ya Azam FC, watacheza kwa nidhamu ya hali ya juu kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu.

Alisema benchi la ufundi limefanya majukumu yao, kazi kubwa iliyobaki ni wao wachezaji kutimiza majukumu yao ya kuwafurahisha mashabiki kwa kupata ushindi.

“Tumejiandaa vizuri, kikosi kipo imara na tunaenda kucheza kwa kuwaheshimu wapinzani wetu kwa kupata ushindi na alama tatu ili kufikia malengo yetu kwa msimu huu,” alisema Gadiel.

Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Kalimangonga Ongala, alisema wamejiandaa vizuri na wachezaji wapo tayari na wanaari kubwa ya kutafuta ushindi dhidi ya Simba.

Alisema Simba ina benchi nzuri la ufundi na wachezaji wazuri, mechi ni kubwa na haitakuwa rahisi kwa sababu ya wapinzani wao.

“Ni mechi muhimu sana, tunahitaji pointi tatu ili kujiweka katika mazingira mazuri na tutacheza kwa tahadhari kubwa sana kulingana na ubora na madhaifu ya Simba ili kufikia malengo yetu ya kupata ushindi,” alisema Kalimangonga.

Mwakilishi wa wachezaji wa Azam, Lusajo Mwaikenda, alisema wamejiandaa vema na wapo tayari kupambana kwa ajili ya kupata matokeo mazuri, hivyo watacheza kwa tahadhari kubwa ili kupata ushindi.

Msimu uliopita raundi ya kwanza timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 kabla ya mchezo wa mzunguko wa pili, Simba kushinda 2-1.

Kadhalika, Simba itaivaa Azam safu yake ya ulinzi na ushambuliaji zikionekana kuwa imara zaidi ya timu zote 16 msimu huu, kutokana na kufumania nyavu mara 12 katika mechi sita ilizocheza huku mabeki wakiruhusu nyavu zao kutikiswa mara tatu tu.

Ni Yanga pekee inayoikaribia Simba kwa ubora wa safu ya ushambuliaji kuwa sawa kwani nayo kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya KMC FC, ilikuwa imecheka na nyavu mara 12, lakini ikipitwa kwa ubora kwenye ulinzi kutokana na mabeki wake kuruhusu mabao matano.

Azam yenyewe imefunga mabao saba na kuruhusu nane, jambo ambalo linaonyesha ipo shida katika safu ya ulinzi.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >